

ZAIDI YA NAKALA MILLION 3 ZIMECHAPISHWA
KATIKA LUGHA 59 KOTE DUNIANI



Kiu Cha Kumtafuta Mungu

Huduma ya Daktari Richard A. Bennett ilianza katika mabaraza ya miji. Akiwa mwanafunzi chuoni, alikumbana na nguvu za Mungu ambazo zilimbadilisha. Baada ya hapo akajiuзу kutoka kazi yake katika baraza moja la mji Uingereza na akaelekea Marekani kupokea masomo ya Biblia.

Alianza huduma yake ya ya kueneza injili na bidii katika ngazi ya chini, na tangu mwaka wa 1946, Dr Richard Bennett amekuwa akishiriki kweli za biblia na wengi ambao wamezipokea kwa furaha. Kwa miaka 20 za sauti yake ilisikika Uropa, Afrika, Asia, Amerika ya Kati na Amerika Kusini kupitia Trans World Radio na Far East Broadcasting Corporation.

Tangu wafunge ndoa yao mwaka wa 1958, Richard na Dorothy wamemtumikia Mungu pamoja kwa furaha, bega kwa bega na Richard, lakini pia kama mhudumu aliye na mahali pake pa kipekee, Dorothy amekuwa na huduma ya kufana kwa kina mama.

Kwa miaka ya hivi karibuni, huduma ya Richard na Dorothy ya kunena katika kongamano kadhaa imeenea na kufikia watu na nchi ambazo mbeleni zilikuwa hazijatembelewa. Katika safari zao kwa nchi zinazoendelea, wamejawa na furaha isiyu kifani kukutana na wengi katika nchi hizi walio na njaa kuu ya kiroho. Lakini furaha hii imekuwa ni ya kuchanganywa na huzuni kwa sababu wameona wanadamu wenzao wengi ambao maisha yao yamefedheheshwa na umaskini, njaa na ukosefu. Upendo wa Mungu kwa ajili ya watu hawa uliwatia motisha Richard na Dorothy kuwapelekea msaada wa kiroho na kimwili.

Hata katika nchi zilizostawi, si kwa nchi zinazoendelea tu, Richard na Dorothy Bennett wanafurahi kukutana na watu wengi ambao hutamani ndani yao kuwa na uhusimo wa karibu na Mungu. Watu wengi kama hawa huwa na maswali.

Je, kuna majibu kwa maswali muhimu kabisa maishani? Richard Bennett anahakika kwamba Mungu mwenyewe ametoa majibu haya. Ndio sababu aliandiaka kitabu hiki, *Kiu Cha Kumtafuta Mungu*.

"Kiu Cha Kumtafuta Mungu... kitawasaidia wasomaji kujiimarisha kiKristo."

*Mch. Stephen Boakye-Yiadom
Trans World Radio, Africa*

CROSS CURRENTS
INTERNATIONAL MINISTRIES
www.ccim-media.com

*Endapo ungependa nakala ya
kitabu hiki, andika kwa:*

Trans World Radio – Kenya
P.O. Box 21514 (00505)
Nairobi, Kenya
Tel: 020-2679842

ISBN 9966-7074-4-1



CROSS CURRENTS INTERNATIONAL MINISTRIES

Bennett

Kiu Cha Kumtafuta Mungu

Kiu Cha Kumtafuta Mungu



*Richard
A. Bennett*

CCIM

*Y Kiu Cha
Tumtafuta
Mungu*



Y Kiu Cha Kumtafuta Mungu

Richard A. Bennett

CROSS CURRENTS
INTERNATIONAL MINISTRIES
www.ccim-media.com

*Endapo ungependa nakala zaidi ya
kitabu hiki andika kwa:*

Trans World Radio - Kenya
PO Box 21514 - 00505
Nairobi, Kenya
e-mail: twr@twr.co.ke
tel: 020-2679842

Kiu Cha Kumtafuta Mungu

Kimeandikwa na Richard A. Bennett

Your Quest for God – Swahili version

By Richard A. Bennett

Kitabu kimetafsiriwa na David M. Angango

ISBN: 9966-7074-4-1

Copyright ©2005, 2009 Cross Currents International Ministries
www.ccim-media.com

Maandiko Matakatifu yamenukuliwa kutoka Biblia: Kiswahili Union Bible
©Bible Society of Kenya and Bible Society of Tanzania

Endapo ungependa nakala zaidi ya kitabu hiki, andika kwa:

Mkurugenzi
Trans World Radio - Kenya
P. O. Box 21514 code 00505
NAIROBI
Tel: 020-2697842

Kama singewekwa moyo, na kuonyeshwa upendo,
na hata kuwekwa mbele ya Mungu kwa njia ya
maombi kutoka kwa mke wangu Dorothy,
singeweza kuandika kitabu hiki.
Sawa na jinsi vile mtume Paulo
alivyomtaja Phoebe, nami nase-ma hivi:
*Yeye Dorothy amekuwa ni msaada kwa wengi,
nami nikiwa mmoja wao.*



Yaliyomo

Utangulizi	ix
Dibaji	xi
Sura Ya 1 <i>Je, Kweli Mungu Yupu?</i>	1
Sura Ya 2 <i>Je, Anayekuongoza Kiroho Aweza Kutegemewa?</i>	11
Sura Ya 3 <i>Mungu ni Nani?</i>	29
Sura Ya 4 <i>Ni Nini Kinachowagawanya Wanadamu?</i>	41
Sura Ya 5 <i>Shida Yenyewe ni Ipi?</i>	59
Sura Ya 6 <i>Mbona Watu Wamekubali Kudanganywa?</i>	71
Sura Ya 7 <i>Je, Kweli Mungu Ananipenda?</i>	85
Sura Ya 8 <i>Ni Wapi Nitapata Maisha?</i>	117
Sura Ya 9 <i>Nawezaje Kujiunga na Jamii ya Mungu?</i>	133
Sura Ya 10 <i>Nini Kitafuata?</i>	147
Uamuzi Wangu	158



Utangulizi

*K*una sababu mbili zinanifanya nisome kitabu hiki, *Kiu Cha Kumtafuta Mungu*, kinafaa sana msomaji. Sababu ya kwanza nikwamba namfahamu vyema mwandishi wa kitabu hiki. Yeye ni mwanangu wa kiroho. Tunasoma katika Maandiko Matakatifu 3 Yoh. 4.

Sina furaha iliyo kuu kuliko hii, kusikia ya kwamba watoto wangu wanakwenda katika kweli.

Mimi linalonifurahisha sana ni kuiskia kwamba watoto wangu wanatembea katika kweli.

Sababu ya pili inahusu uandishi wa kitabu hiki. Kwa kweli, Daktari Richard Bennett amefanya kazi nzuri sana ya kufafanua wazi na kwa ufasaha, na kwa njia inayoeleweka mambo ya muhimu yanayohusu uhusiano kati ya wanadamu na Mungu.

Katika Mhubiri 3:11 tunasoma hivi:

Kila kitu amekifanya kizuri kwa wakati wake; tena ameiweka hiyo milele ndani ya mioyo yao (Mhu. 3:11).

Biblia inasema wazi kwamba Mungu ametengeneza nafasi ya maisha ya milele katika mioyo ya wanadamu. Kwa hivyo, ni wazi kwamba kwa vile sisi wanadamu tumeumbwa tuwe na maisha ya milele, vile vilivyo

Kiu Cha Kumtafuta Mungu

vya muda mfupi haviwezi vikatosheleza mahi-taji yetu milele. Kuna nafasi katika mioyo yetu; nafasi ambayo yaweza kujazwa tu na Mungu mwenyewe. Mtakatifu Augustine alielewa haya vyema kabisa aliposema haya: Mungu wetu ume-tumba kwa ajili ya kuwa wako milele na katika nafsi zetu kuna upweke ambao ni wewe tu unayeweza kuondoa.

Katika kitabu hiki yanapatikana maelezo ya kukuongoza na kukusaidia ili uweze kupata njia ya kutosheleza *Kiu cha Kumtafuta Mungu*. Pia kitabu hiki kitakuwezesha kujenga uhu-siano bora na Mungu aishiye milele, Mungu wa kweli.

Ni ombi langu kwamba wengi wa wale watakaosoma kitabu hiki, na kutilia maanani mafunzo na maelezo yaliyomo watapokea msaada kwa ajili ya utukufu wa Mungu wetu.

Dr. Stephen F. Olford

“*Kiu Cha Kumtafuta Mungu* ni kitabu ambacho nakushauri ewe ambaye una tafuta kwa hamu na nia ya kujua ukweli halisi wa maisha. Hiki ni kitabu cha mafunzo yanayofaa ya dini na kitakusaidia kujijenga kiKristo. Kitabu kinakufaa ewe msomaji!”

Mch. Stephen Boakye-Yiadom
Trans World Radio, Africa

Dibaji

*K*atika safari zetu za hapa na pale, mimi pamoja na mke wangu Dorothy tumekutana na wengi; kila mmoja akiwa katika hali inayotofautiana na ile ya mwenzake maishani. Wengi wametoka katika asili mbali mbali, hali ya maisha ya kila mmoja wao ikiwa ni tofauti na ile ya mwenzake. Hata viwango vya masomo vinatofautiana.

Sisi tunajua wazi kwamba mikutano yetu na hawa ambao tumetaja huwa si tukeo la ghafla, sawa na ajali. Pia tukio hili hapa ambapo wewe msomaji unajikuta kuwa na kitabu hiki mkononi si tukio sawa na ajali. Kwa mda wa miaka mingi, kiasi kikubwa cha majadiliano yetu na wenzetu yamehusu kiu chetu sisi wanadamu kumjua Mungu. Kati ya yale tumejadili yako kati-ka kitabu hiki.

Uchapishaji wa toleo la kwanza na la pili la kitabu *Your Quest for God*, ambacho tafsiri yake ni, “Kiu Cha Kumtafuta Mungu” ni mradi wa shukrani. Tulipokuwa tunakaribia miaka 25 tangu tufunge ndoa, na hapa tukawa tunawaza kuhusu lile ambalo tungefanya kumshukuru Mungu kwa ajili ya mapenzi yake kwetu kwa muda huo wote. Kama njia ya kumshukuru Mungu, tuliamua kuchapisha kitabu hiki. Lengo letu

wakati huo lilikuwa kuandika, na kuchapisha nakala 25,000 kitabu chenye ujumbe na kuleta amani katika roho za wasomaji. Hii ilikuwa ni sawa na kuchapisha vitabu 1,000 kwa ajili ya kila mwaka wa maisha yetu pamoja katika ndoa-jumla, nakala 25,000.

Mungu amebariki kazi hii tulijitoa kufanya kwa ajili ya upendo: kitabu hiki sasa kimefika kila pembe ya dunia. Nakala 25,000 za kwanza zilipewa watu katika mataifa mbali mbali duniani. Lile ambalo lilitufurahisha wakati ule na hata hivi leo ni kupokea barua kutoka kwa wale ambao baada ya kusoma kitabu hikiwamepata muelekeo mpya maishani.

Baada ya hapo, tulipokea maombi ya kutaka kitabu hiki kitafsiriwe katika lugha mbali mbali. Hapo basi tukaamua kubadili sehemu fulani katika kitabu hiki na hata kuongeza mambo fulani kabla kitabu hakijatafsiriwa. Lengo letu ni kwamba wasomaji wataweza kufaidika zaidi na kupata msaada unaofaa wakati wa kujaribu kutosheleza Kiu Cha Kumtafuta Mungu. Tangu mabadi-liko hayo, karibu nakala milioni tatu katika lugha 50 zimechapishwa.

Huenda sura za kwanza mbili zikawa si za msaada kwa kila msomaji. Sura wa kwanza inafaa sana kwa msomaji ambaye hana uhakika kwamba kweli Mungu yupo. Ingawa sura ya pili inawalenga wale ambao wamezoea kuuliza maswali kuhusu kila jambo, sura hii inafaa kila msomaji kwa vile yale yaliyomo yatakusaidia na kuamsha ile hamu ya kuchungunza na kuelewa vyema imani uliyo nayo.

Sura hizi za mwanzo ni za msaada katika kuandaa yale ya muhimu zaidi ya yote katika kitabu hiki.

Dibaji

Katika sura ya 3 hadi ya 10 kuna ukweli ambao utakusaidia katika shughuli yako ya kutosheleza kiu ulicho nacho cha kumjua Mungu.

Kwa hivyo, twakiweka kitabu hiki mikononi mwake Mungu, aweze kukibariki na kuendeleza yale ambayo yanalingana na mapenzi yake.

Mimi pamoja na mke wangu Dorothy tunachukua nafasi hii kumshukuru sana Mungu kwa ajili ya msaada, maombi na hata mawazo ya watu wengi ambao wamekubali kutushirikisha katika yale yanagusia uhusiano wao na Mungu. Kwa kweli, idadi yao ni kubwa mno hivi kiasi kwamba hatuwezi kuandika majina yao hapa. Yetu hapa ni kusema hivi: “Ahsante sana nyote, na Mungu awabariki!”

Dkt Richard A. Bennett



*I Kiu Cha
Tumtafuta
Mungu*

*Somo la Jiolojia linahusu kuilewa dunia
kulingana na inavyojieleza yenyewe, na
sawa na vitabu vinginevyo vinavyohusu
habari za maisha ya watu jinsi
wanavyojieleza wenyewe, habari hizi
hazianzi mwanzoni.*

SIR CHARLES LYELL

Je, Kweli Mungu Yupo?

*H*uenda kuna wakati katika maisha yako ambapo mambo yamekuwa magumu kwako kiasi kwamba umejikuta huna uhakika kama kwamba kweli Mungu yuko. Hata labda huna uhakika kwamba Mungu yuko.

Katika Maandiko Matakatifu, Biblia, kuwako Mungu ni jambo ambalo halielezwi. Hili ni jambo ambalo huchukuliwa kuwa la kuaminiwa na kwamba halihitaji maelezo wala ufafanuzi zaidi. Sentensi ya kwanza kabisa katika Biblia inasema: *Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi (Mwa. 1:1)*. Haya ni maneno ambayo ni rahisi kuyaelewa, na yenye uzito mkubwa. Hapa tunaambiwa wazi kwamba Mungu yupo nani yeye aliyeumba mbingu na nchi.

Katika miaka ya hapo nyuma, mke wangu Dorothy aliwahi kufanya kazi kama muuguzi katika hospitali moja ya maradhi ya akili. Hospitali hii ilikuwa yenye sifa kuu huko ulaya. Siku moja, daktari ambaye alikuwa mtaalam wa maradhi ya akili na ambaye

hakuwa na imani ya dini yeyote alimjia Dorothy na maswali kuhusu imani. “Daktari,” Dorothy akamjibu baada ya swali, “nakuheshimu sanakwa ajili ya ujuzi wako kazini. Wewe ni mwalimu anayeheshimiwa sana hata kule unakofunza kwenye chuo kikuu. Hata hivyo, nakushauri kabla hujasema tena kwamba huamini Mungu yupo, soma Biblia kwa makini jinsi vile wewe husoma vitabu vinavyohusu kazi yako ya udaktari.”

Baada ya kusema hayo, Dorothy alimkumbusha kwamba wako wagonjwa ambao walionekana kuwa hawangeweza kupona na daktari alikuwa amewahudumia, wakapona na kutoka vyumba vya wagonjwa mahututi. Dorothy alimueleza kwamba ni Mungu alikuwa amewawezesha kutoka hali yao hiyo mahututi. Dorothy aliendelea kwa kutaja majina ya wagonjwa wawili hivi ambao walikuwa wamepata nafuu baada ya kuamini kwamba Mungu ana uwezo wakuwasaidia. Hawa walikuwa wagonjwa ambao daktari mwenyewe alikuwa ameshuhudia kwamba ujuzi wake ulikuwa umeshindwa kuwaletea nafuu. Akiwa mtaalamu wa maradhi ya akili, na pia mtu ambaye haamini kwamba kuna Mungu, daktari huyu hakuweza kuelewa jinsi vile mabadiliko haya yalivyotoke a.

Walipofika mwisho wa mazungumzo yao, daktari huyu alimsihi Dorothy amuombe! Akatoa ahadi kuanza kusoma Biblia bila kujiwekea pingamizi katika mawazo yake.

Baada ya kusoma Biblia kwa muda wa wiki saba hivi, daktari alimwendea Dorothy, akamumabia alikuwa ametupilia mbali imani yake ya hapo awali

Je, Kweli Mungu Yupo?

kwamba Mungu hayupo. Hata hivyo, alikiri kwamba alikuwa yungali ana shida moja: kwamba hakuwa tayari kuweka imani yake kwake Mungu. Sababu ya kutotaka kujitoa vikamilifu ni, ilikuwa uamuzi kama huu ungemhitaji abadili mienendo yake Alieleza shida yake hivi: “Shida yangu sio ya mawazo-ila shida yangu ni kwamba sitaki kukubali mabadiliko yatakatotokea katika maisha yangu pale nitakapokuwa mwaminio.”

Tuliamua kumuomba daktari huyu. Baada ya miaka kumi ya kuomba pasipo kuchoka, tulipokea barua kutoka kwake na katika barua hii akatueleza kwamba alikuwa amekubali wokovu. Tulijawa na furaha isiokuwa na kifani. Hata hivyo, hatukushangazwa na ujumbe huu kwa vile tulijua kutoka maandiko Matakatifu kwamba *Imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo (Rum. 10:17)*.

Ili kutusaidia tuweze kumjua Mungu vyema, yeye ameweka ndani ya nafsi zetu ufahamu unaotufunulia kuwepo kwake.

Wa ko wale ambao wamechagua kutoamini kwamba Mungu yupo. Hata hivyo, hakujawahi kutokea yeyote duniani ambaye hawezi kuamini kwamba Mungu yupo.

Hata katika ulimwengu huu tunaouona na macho, Mungu ameweka ushahidi wa namna unaoonyesha kwamba yeye yupo. Hata tunapoingia katika utafiti wa ndani wa kisayansi; katika karne hii, ni jambo lisilokuwa na msingi kusema kwamba yote yaliyomo hapa duniani yalitokea pasipo mpangilio maalum. Na sio mpangilio wa kawaida: huu ni mpangilio

ulioandaliwa kwa makini kabisa! Hakuna yeyote anayeweza kusema tunaweza kuwa na chombo cha kwenda angani, kikazunguka dunia, kikaru-di na kutua ardhini mahali paliochaguliwa pasipo ujuzi wa wataalamu mbali mbali kama wale wa hesabu, sayansi, mafundi na wengineo. Vivyo hivyo kucha na kuchwa kwa jua, majira ya hali ya hewa, nyota za angani, nguvu za asili za uzito, nguvu zin-zowavuta wanadamu kupendana: haya yote hayawezi yakawako pasipo mpangilio na uumbaji wake Mungu.

Kwa kweli unahitaji kuwa na imani ya kiwango cha juu sana (imani iliyojumulishwa mara milioni kadha) kuamini kwamba vyote vilivyo duniani, vimeumbwa kulingana na utaratibu na mpangilio maalum. Sio kwamba vimetokana na ‘mlipuko’ au ‘mgongano’ wa nguvu. Kwa kweli ni rahisi kuamini kwamba vyote duniani vimetokana na uumbaji wake Mungu kuliko kuwa na imani tofauti. Kwa kweli, hatuwezi tukawa na chochote kilicho na umbo maalum pasipo yule aliyekiumba.

Hata serikali ambazo husema kwamba Mungu hayupo huamini mpangilio na utaratibu fulani katika ulimwengu huu unaowawezesha wao kuwatuma wanaanga juu hewani. Ni pale tuu wanapopanga mambo yao kulingana na utaratibu fulani katika ulimwengu huu kimaumbile ndipo wanaweza kuwatumawanaanga hawa juu na kutarajia kwamba wao watarudi salama. La kushangaza ni kwamba, hawa ambao hupanga mambo yao kulingana na sheria fulani za kimaumbile; ni wao husema hakuna yeyote mwenye kuandaa na kuweka sheria hizo.

Je, Kweli Mungu Yupu?

Sote twaelewa vyema hasara kuu inayotokana na mlipuko wa bomu ya atomiki. Utafiti umeonyesha kwamba kila sekunde, jua hutoa nguvu yenye kipimo sawa na mlipuko wa mabomu bilioni 5,000. Jua nalo likilinganishwa na nyota ambazo ziko angani na hutoa nguvu na joto; jua ni ndogo, na bado hatujui ni nyota ngapi zilizoko huko juu. Ingawa hesabu zaonyesha kwamba kuna karibu mabilioni ya nyota huko juu, kuna uwezekano kwamba nyota hizi ambazo zaonekana ni zile ambazo ziko karibu. Hatujui ni ngapi ziko mbali kabisa kule juu. Ingawa hivi sasa wataalamu wa sayari wanasema kwamba nguvu zinazotokana na joto katika sayari ni mara bilioni kadha zaidi ya nguvu kutoka kwa jua, je, nguvu kama hizi zitatoka wapi pasipo muumba aliye na kipawa cha kuumba kisicho na kipimo?

Uumbaji wa ulimwengu watuonyesha wazi kwamba kuna Mungu aliye na mpango na anayefuata kanuni; Mungu aliye na sheria, na aliye na nguvu zisizo na kipimo. Katika Biblia twasoma hivi:

*Mbingu zauhubiri utukufu wa mungu,
Na anga yaitangaza kazi ya mikono yake.
Mchana husemezana na mchana, usiku hutolea
usiku maarifa.*

*Hakuna lugha wala maneno,
Sauti yao haisikilikani
Sauti yao imeenea duniani mwote,
Na maneno yao hata miisho ya ulimwengu.
Katika hizo ameliwekea jua hema (Zab. 19:1-4).*

Kwa sababu mambo yake yasio onekana tangu kuumbwa ulimengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uwezo wake wa milele na Ungu wake; hata wasiwe na udhuru (Rum. 1:20).

Kwa hivyo basi, hakuna sababu ya kumfanya yeyote aseme kwamba Mungu hayupo.

Ukiwaza kuhusu ukubwa, mpangilio wa nguvu ambazo Mungu ameumba, watu wengi hujiona kuwa wanyonge, na wasio na umuhimu.

Hata mfalme Daudi wa agano la kale alisema hivi katika Zaburi:

*Nikiziangalia mbingu zako, kazi
Ya vidole vyako
Mwezi na nyota ulizoziratibisha;
Mtu ni kitu gani hata umkumbuke,
Na binadamu hata umwangelie (Zab. 8:3,4).*

Leo hii, ujuzi wetu kuhusu sayari na mambo ya anga za juu umepanuka sana. Kuna mitambo mikubwa ya kutazama anga za juu, na hata kuwezesha vile vilivyo kuonekana kuwa vikubwa kwa kiwango cha hata nusu milioni. Hata tuna mitambo ya satellite ambayo hutumwa kule juu, na kutuletea picha hapa ardhini kutoka huko juu. Kwa hivyo, sawa na mfalme Daudi, twaweza kujiuliza: “ni kwa nini Mungu aliyeumba hivi vyote awe na hamunami; hata anishughulikie mimi niliye mnyonge?”

Je, Kweli Mungu Yupo?

La kutia moyo ni kwamba Mungu aliyetupatia chombo cha kuangalia vile vilivyo mbali (telescope) ndiye Mungu ambaye pia ametupatia chombo cha kuangalia vile vilivyo vidogo kabisa nacho ni darubini (microscope).

Sawa na jinsi vile yako maajabu makubwa katika anga za juu, darubini nayo yaweza kutufichulia maajabu yaliyoko katika vile ambavyo ni vidogo sana. Hata mwanga hauna uwezo wa kutufichulia vyote vilivyo vidogo kiasi kwamba haviwezi kuonekana na macho ya mwanadamu. Na vile ambavyo haviwezi kuonekana kupitia darubini ya kawaida, kuna darubini ya nguvu zaidi iitwayo **electronic microscope** (katika lugha ya kiingereza). Na kila mara darubini hizi hutumiwa, hufichua siri nyingi kuhusu mpangilio na uhusiono ulioko kwenye sehemu hizi ndogo kabisa.

Kwa hivyo, ikiwa unawaza na hujui kama kweli Mungu yumo katika vile vilivyo vidogo sana, basi ni bora umsikilize mtaalamu wa Fisikia akueleze umuhimu wa vile vilivyo vidogo kabisa vina umuhimu katika kustawisha mazingira yetu. Ukichukua sehemu ndogo sana ya kitu, sehemu iitwayo **neutron**, uitoe na iwe mbali na sehemu ingine ndogo iitwayo **proton**, umbali wa urefu 1/12 trilioni ya kipimo cha inchi, kazi hii yaweza kufanya dunia yote ilipuke. Kile kilicho kidogo ni cha muhimu sawa na kile kilicho kikubwa. Vyote ni sawa mbele yake yeye aliyetuumba, Mungu

Ni jambo la kutia moyo kwamba tunapojiuliza: mtu ni kitu gani hata umkumbuke; na binadamu hata umwangalie, Mungu hamaanishi ukubwa au udogo

Kiu Cha Kumtafuta Mungu

wetu. Kipimo chake ni tofauti kabisa na vipimo vyetu sisi wanadamu.

Mungu ametufichulia ni kwa nini anatumia sana. Ingawa kazi ya uumbaji yaonyesha wazi jinsi vile Mungu hupanga, huumba, na mwenye nguvu; yeye mwenyewe amechagua nia ya kutuonyesha upendo na rehema zake. Ametuonyesha kwamba yeye anatumia mema

Ukitaka kumjua Mungu huyu, basi ni sharti ufuate utaratibu fulani wa kiroho. Utaratibu huu ni lazima uwe bora na wa kuaminika.

Je, Kweli Mungu Yupo?

Hebu Fikiria

1. Ikiwa utarusha chembe cha chuma hewani, je, zaweza zikabadili kapale utakapozishika na zikawa tuseme saa ya bei kubwa kama zile kutoka Uswisi?
2. Je, yawezekana kwamba ulimwengu huu, pamoja na maajabu ya kimaumbile yaliomo yalitokea tu pasipo Mungu muumbaji?
3. Ingawa uumbaji waweza kuelekeza kwake Mungu muumbaji, ambaye uwezo wake unaonekana kupitia mpangilio wa vyote vilivyoko duniani, sheria za kimaumbile duniani, na nguvu zilizowezesha uumbaji. Je, haya yote yanaweza yakakusaidia kuelewa upendo na rehema zake mungu?

*Pango lenye giza laweza kupitika na
yule aliye na tochi.*

PLATO

*Maumbile ya asili ni kama mwanga
kutoka mlangoni mwa pango; tochi yake
ni Maandiko Matakatiifu.*

A.H. STRONG

Je, Anayekuongoza Kiroho Aweza Kutegemewa?

*J*uzi, magazeti yalichapisha habari kuhusu ajali mbaya ya ndege ambayo watu wengi sana walipoteza maisha yao. Ajali hii ilitokana na kasoro katika mitambo ya kuongoza ndege iitwayo radar. Hata hivyo, ajali hii haiwezi kulinganishwa na maafa yanayoto kea pale watu wanapokubali kuongozwa kiroho kwa njia iliyo na kasoro kama mtambo huu wa radar. Matokeo hapa ni kwamba wenye kuongozwa kiroho kwa njia mbaya watajikuta katika maafa makubwa.

Siku hizi, yako mambo mengi yanayojitokeza na yanawaongoza watu wake Mungu. Sauti ni nyingi mno, kila moja inajitokeza na kusema yaweza kumwongoza mwanadamu kwa Mungu. Je, utajuaje sauti ya kuamini? Unapomtafuta Mungu, usikubali kuongozwa na sauti isiyofaa kwa sababu haya ni mambo yanayohusu uzima wa milele.

Waziri mkuu wa uingereza wakati mmoja W.E. Gladstone aliwahi kuandika hivi: “Biblia ina asili maalum; na tofauti kati yake na maandishi yanayofanana nayo ni urefu usioweza kupimika.”

Naye Rais wa Marekani wakati mmoja, Abraham Lincoln aliwahi kusema: “Naamini Biblia ndio zawadi bora zaidi Mungu amewahi kuwapa wanadamu.”

Hata ingawa ni wengi walio na sifa wamewahi kutoa ushuhuda kwamba Biblia ni kitabu kilicho tofauti na vitabu vingine, Biblia ina maandishi yanayoweza kujisimamia.

Mfalme Daudi alitambua ni nani anayefaa kumwongoza kiroho. Naye alisema hivi: *Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu (Zab. 119:105).*

Hata leo watu wengi wanazidi kutambua kwamba Biblia inaweza kuaminika na kuongoza mtu hadi kwa Mungu. Hata ingawa wako wale ambao wamejaribu kushusha heshima na uwezo wa maandiko matakatifu, Biblia ingali inasimama wima na kwa imani leo jinsi vile ilivyokuwa miaka iliyopita. Bado Biblia ni maandishi maalum kabisa duniani.

Na kwa vile watu wengi wanahitaji uhakika kabisa kwamba Biblia ni maandiko maalum na pia ya ukweli, Mungu ameweka kwenye haya maandishi mihuri mbali mbali inayothibitisha ukweli wa maneno yaliyomo, na kuonyesha kwamba kweli haya yalioko ni maneno yake Mungu mwenyewe. Yule anayetafuta ukweli, akisoma maandiko matakatifu yenyewe, na hata kufanya utafiti wa kihistoria atagundua kwamba kweli kuna ushahidi kwamba: *Kila andiko lenye*

Je, Anayekuongoza Kiroho Aweza Kutegemewa?

pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kuwaadibisha katika haki (2 Tim. 3:16).

Kama maandiko matakatifu yangukuwa yameandikwa na mtu mmoja, hatungestaajabu kukuta kwamba kuna utaratibu fulani katika mtindo wa maandiko.

Hata hivyo, kitabu hiki ambacho ni maandiko matakatifu kimeandikwa na watu wengi kutoka mataifa na tamaduni mbali mbali. Pia kimeandukwa kwa muda mrefu ambao ni karne nyingi. Na kando na tofauti hizi zote za ajabu ni kwamba kitabu hiki kinafuata utaratibu na orodha ya ajabu nay a kimiujiza. Na isitoshe, watafiti wa mambo ya kale wamezidi kugindua ushahidi ambao umeonyesha uhakika na ukweli wa maandiko haya matakatifu. Yale ambayo yalichukuliwa kuwa kama hadithi ya kubuni sasa yana weza kudhibitishwa na ushahidi ambao umetokana na utafiti wa kitalaam.*

Kwa kweli, Biblia ni kitabu cha Mungu kina ujumbe wa Mungu kwa watu wote.

* Mfano ni kwamba mwaka wa 1868 msafiri mjerumani kwa jina Klein alitembelea mji wa kale wa Moabu ambao hivi sasa unaitwa Jordan. Na hapa aliweza kupata chombo ambacho kilikuwa na maandishi yenye mistari 34 yaliyoandikwa na mfalme Meshu wa Moabu. Maandiko haya yalikuwa kama kumbukumbu baadaya uasi wake katika taifa la Israeli. Omri na Ahabu wote wanatajwa katika wafalme 11kifungu cha kwanza na pia kwenye maandishi haya ambayo ni kumbukumbu katika maandishi haya yote, tunaalezwa kwamba wafalme hawa waliwanyasya wenyeji wa Moabu. Uvumbuzi kama huu wa siku hizi ni thibitisho la ukweli wa kihistoria way ale ambayo yameandikwa katika Biblia.

Hata ingawa Biblia ni kitabu cha Mungu, wako wengine ambao wameshindwa kusoma kitabu hiki kwa ajili ya imani kwamba dunia ina vikundi viwili vya watu. Kwanza kabisa ni kikundi cha wataalamu wa sayansi ambao huamini tu kile wanachokiona na macho yao. Wa pili ni wale wenye imani ambao huamini hata kile ambacho hawajakiona. Wazo kama hili lina maana kwamba mwana sayansi halisi hawezi kuwa na imani katika kile ambacho hajaona na macho yake.

Hivi leo, wako wataalamu wa sayansi wengi duniani ambao wanapinga wazo kama hili. Ingawa Biblia si kitabu cha sayansi, kinapogusia mambo ya sayansi, hakuna anayeweza kuko soa Biblia. Badala ya kutoa makosa katika Biblia, lengo na mpangilio katika Maandiko haya Matakatifu unazidi hata viwango vya juu kabisa katika sayansi. Kwa mfano, sayansi haielezi kinaga ubaga ni kwa nini mwanadamu yuko hapa duniani. Sayansi haielezi ni wapi tutaele kea baada ya kifo. Katika sayansi, hatuelezwi ni kwa nini mwanadamu awe na uhai. Hata thamani halisi ya mwandamu haina kipimo katika sayansi. Na hata awe na akili ya kiwango cha juu, au chini, kila mwanadamu anahitaji usaidizi maalum wa kiroho ndipo aweze kumjua Mungu. Mtaalamu wa hesabu na Filosofia kutoka Ufaransa kwa jina Blaise Pascal alisema hivi: “Ufanisi mkuu katika kutafakari ni kuonyesha kwamba mawazo ya mwanadamu yana kikomo.” Hatungeweza kuwa na majibu yanayostahili kuhusu maswali fulani magumu maishani kama hatungekuwa na Maandiko Matakatifu.

Je, Anayekuongoza Kiroho Aweza Kutegemewa?

Na sasa hebu tuangalie sababu mbili kuu ambazo ni thibitisho kwamba Biblia ni Kitabu cha Mungu:

Kwanza kabisa ni usahihi unaohusu yale yaliyotajwa na manabii. Na pili ni umaarufu na uwezo ambao Maandiko Matakatifu yamekuwa nayo katika maisha ya watu ambao wametilia maanani yale yanayopatikana humo.

Usahihi wa Unabii katika Biblia

Katika kila mmoja wetu, kuna kiwango fulani cha hamu ya kutaka kujua ni yapi yatatokea kesho na hata siku za baadaye. Biblia ina maelezo kuhusu mambo yatakayotokea katika siku za baadaye. Biblia inafichua mengi ya siku za baadaye. Nayo inafanya hivyo kwa njia maalum. Huenda ukajiuliza: “Nawezaje kuwa na uhakika kuhusu haya yote yaliyo katika Biblia?”

Ili kujibu swali kama hili, hebu waza hivi: umechukua likizo na kwenda safarini nchi ambayo hujawahi kutembelea. Kile cha kukuongoza safarini ni ramani tu! Katika safari kwingineko mbeleni, ramani hii ilikusaidia sana na hata pale ilipoonyesha mto; kweli ulipata mto hapo.

Na ramani ilipoonyesha kuwa kuna kijiji, kweli ulipata kijiji hapo, hata ukalala hapo usiku huo. Leo hii, ni lazima uamue barabara mpya utakayofuata. Na bado mbele yako ni sehemu ambayo hufahamu kamwe. Ramani yako yaonyesha kwamba ukieleke a sehemu ya kushoto, utapitia sehemu yenye msitu na hapa utakuta ziwa kubwa. Sasa una hamu ya kuona

ziwa lile. Je, utawezaje kuona ziwa lile? Ni nini utafanya ili uweze kuona ziwa lile?

Sina shaka utafuata mkono wa kushoto jinsi vile ramani imeonyesha. Sina shaka pia sababu yako kuwa na uhakika ni kwamba jana ramani hii ilikuwezesha kufika mahali ulikuwa ukielekea. Rami ile ilikueleza ni nini utakutana nacho, na kweli ramani ile ilikuwa sahihi.

Jambo la ajabu kabisa ambalo ni thibitisho kwamba Biblia ni Neno la Bwana, lahusu jinsi vile unabii ulioko kwenye Maandiko Matakatifu umetimia.

Ya ko mengi ya unabii ambayo hivi leo tunajua yametimia. Mengi haya ya unabii yanahusu watu wote duniani na mambo tofauti tofauti. Unabii huu unahusu taifa la Israeli na mataifa ya mashariki ya kati.

Na la muhimu kabisa ni kwamba kuna yale yaliotabiriwa zamani kuhusu kuja kwake Masihi. Na kwa vile yanayohusu kuja kwake Masihi ni kama historia, tunaweza kuona jinsi vile utabiri na maneno ya unabii yalivyokuwa sahihi. Yote yalikuwa sahihi sana na hasa kuhusu kuzaliwa kwa Masihi, maisha yake na hata kifo chake huyu ambaye ni Mwokozi wetu.

Kwa hivyo, kutokana na haya ambayo tumeyaona na kuyasikia, tunaweza kuamini mbele yetu yako yatakayotokea ambayo ni sawa kabisa na jinsi vile Biblia imetabiri. Kwa hakika, kusoma Biblia ni sawa na kusoma gazeti la kesho hivi leo.

Daktari Wilbur Smith alitumia muda mrefu kusoma mengi kuhusu Biblia. Yeye alitilia mkazo sana umuhimu wa kuonyesha wazi usahihi wa unabii

Je, Anayekuongoza Kiroho Aweza Kutegemewa?

ulioko katika Biblia. Alipokuwa akifananisha maneno ya unabii katika Agano la kale kuhusu Masihi na mafunzo ya wale wanaosema kwamba wanafunza ukweli, yeye alisema hivi: “Waanzilishi wa vikundi fulani vya kidini hawawezi wakatuonyesha nyaraka za kale zilizotangaza kuzaliwa kwa waanzilishi wa vikundi vyao.”

Na hapa ni lazima tufahamu kwamba kuna unabii fulani ambao hauhitaji chochote ili kutimbia.

Kwa mfano, kupitia matumizi ya mtambo kama komputa, mahojiano na historia, vyombo vya habari vyaweza kutabiri vyema kabisa ni nani atashinda katika uchaguzi fulani hata kabla kura kuhesabiwa. Wakitumia hesabu walizo nazo, hakuna jambo gumu na la ajabu kuhusu utabiri wao kuhusu matokeo ya kura. Na hebu jaribu umwulize mwandishi wa habari ni nani atakayesimama kugombea kiti fulani miaka ishirini au hamsini kutoka hivi leo. Muulize nani ataibuka mshindi; naye huyu mshindi amezaliwa na kulelewa wapi; maisha yake yamekuwa ni yapi na ataaaga dunia kwa njia gani. Endelea ukamwulize mwandishi huyu wa habari ni yapi yatatokea mashariki ya kati yapata miaka 1000 kutoka leo. Pia mwulize ni mji gani utatoweka wakati huu. Bila shaka ni wazi kwamba utakapozidi kuliza maswali, ndipo mwandishi huyo atazidi kupata ugumu wa kukujibu. Yeye atapata ugumu sana kutabiri yale ya baadaye. Hii ni kwa sababu Mungu aishiye milele hajamfunulia maneno haya ya unabii. Na matukio sawa na haya amabyo tumeuliza juu ni mambo ambayo Maandiko Matakatifu yameweza kuyataja katika sehemu za Unabii.

Historia ya mji wa kale wa Tiro ni mfano bora sana unaoonyesha jinsi utabiri uliotolewa na Mungu ulivyotimizika.

Nakusihi soma unabii ulioko Ezekiel 26:3-21 na baada ya hapo, soma pia *Encyclopaedia Britannica* kuhusu Tiro. Chagua kitabu chochote na usome zaidi kuhusu Tiro. Utakaposoma Ezekiel na baadaye usome *Encyclopaedia Britannica*, utagundua mara moja kwamba yale unayosoma yanafanana. Yaliyo katika Ezekiel ni unabii, nayo yale katika *Encyclopaedia Britannica* ni kumbukumbu ya kiHistoria.

Unabii: Miaka mingi kabla matukio yenyewe kutokea, Mungu kupitia nabii wake alitabiri kwamba kutatokea misukosuko mjini Tiro. Haya ndio nabii alisema:

Basi Bwana Mungu asema hivi; tazama mimi ni juu yako, Ee Tiro, nami niatleta mataifa mengi kupigana nawe, kama bahari iinuavyo mawimbi yake. Nao wataziharibu kuta za Tiro, na kuibomoa minara yake; tena nitakwangua hata mavumbi yake yamtoke, na kumfanya kuwa jabali tupu. Nao wataufanya utajiri wako kuwa mateka, na bidhaa yako kuwa mawindo; nao watazibomoa kuta zako, na kuziharibu nyumba zako zipendezazo; nao watweka mawe yako, na miti yako, na mavumbi yako kati ya maji. Nami nitakufanya kuwa jabali tupu; utakuwa mahali pa kutandaza nyavu za wavuvi; hutajengwa tena; maana mimi BWANA, nimenena neno hili, asema Bwana Mungu (Eze. 26:3,4,12,14).

Je, Anayekuongoza Kiroho Aweza Kutegemewa?

Historia: Ukisoma kumbukumbu za historia, utaona wazi kwamba wakati mfalme Nebukadneza alipoharibu mji wa kale wa Tiro, yeye kwa kweli alivunjavunja na kuharibu kuta za mji huu na hata minara jinsi vile ilivyotabiriwa. Na baadaye mafundi wa mfalme Alexander walifagia mji huu na kuacha Tiro ikiwa safi kama jabali tupu.

Na walipotupa mabaki haya katika bahari ili mabaki yatumiwe kutengeneza barabara katika maji kuelekea kisiwani, hii ilikuwa sawa kabisa na jinsi vile unabii ulivyotabiri. Mawe, mbao na kadhalika vyote vilitupwa katika maji. Hata leo, mabaki ya mji wa Tiro yako ndani ya maji baharini. Mungu alisema haya ndiyo yatakayotokea, na kweli yalitokea.

Ingawa kuna mji mkubwa uitwao Tiro mashariki ya kati, huu sio mji ule wa Tiro wa zamani. Mji huo wa zamani ulibomolewa na kuharibiwa kabisa mwaka wa 1291.

Ukitembelea pale ambapo palikuwa ni mji wa Tiro wa zama hizo, utajionea mengi ya ajabu ambayo ni kutimia kwa yale yaliyoko katika unabii. Huko utaweza kuona nyumba ndogo za wavuvi katika vijiji. Pia utaona mashua ndogo za wavuvi pamoja na nyavu zao zimewekwa kwenye mawe kando ya bahari ili zikauke. Je, ni ujasiri gani wa mwanadamu ungeweza kutabiri haya kuhusu mji ambao ulikuwa ni wenye utajiri wa biashara na ulionekana kuwa utazidi kustawi milele na milele?

Mtaalamu kwa jina Peter Stoner aliwahi kufananisha unabii kuhusu Tiro ya zamani na yale yanayopatikana katika kumbukumbu za historia.

Baada ya kufanya hesabu kuhusu matukio hapa Tiro na unabii wa Ezekieli, yeye alisema hivi:

“Kama Ezekieli angeutazama mji wa Tiro wakati wake, na atabiri mara saba jinsi vile utakavyofanywa akitumia akili ya mwanadamu, uwezekano wa utabiri huu kuwa kweli ungetoke a mara moja kila baada ya matukio milioni sabini na tano. Hapa utabiri wote umetokea kwa njia iliyo sahihi bila kosa hata moja tu.”

Na sasa hebu tuangazie utabiri unaohusu kuzaliwa kwa mtoto.

Mathayo ambaye alikuwa ofisa wa ushuru serikalini baada ya kustaaifu alitaja visa vinne vya unabii ambavyo vilitimizwa wakati Kristo alipozaliwa. Moja ya maneno ya unabii huo yalihusu nabii Mika ambaye aliwashutumu viongozi wa siku hizo na maneno yenye ukali. Mika alikuwa nabii aliyehuzunishwa sana na uovu wa viongozi hao. Hata hivyo, Mika aliweza kuonyesha na Mungu kupitia njia ya unabii kwamba baadaye mambo yangebadilika. Mungu alimuonyesha kupitia unabii kwamba siku moja, kiongozi maarufu angezaliwa. Mika hata aliweza kuambiwa ni mji gani angezaliwa kiongozi huyu.

*Bali wewe Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa **matawala** katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele (Mik. 5:2).*

Mungu aliwafichulia kwamba kiongozi aliyehitajika katika taifa la Israeli angezaliwa katika mji wa Bethlehemu Efrata.

Je, Anayekuongoza Kiroho Aweza Kutegemewa?

Sawa na jinsi vile matamshi yake nabii Mika yanavyoeleza, ukweli ni kwamba Kristo alizaliwa Bethlehemu Efrata, mbali kutoka nyumbani Nazareti. Alizaliwa hapa kwa ajili ya amri iliyokuwa imetolewa na mfalme wa Warumi. Ilikuwa ni wakati wa watu kuhesabiwa. Wazazi wake Kristo walifunga safari kutoka nyumbani Nazareti hadi Bethlehemu Efrata ili wahesabiwe.

Kwa kweli, hakuna yeyote ambaye angemtafuta kiongozi katika mji kama huu wa Bethlehemu ambao ulikuwa ni mji mdogo katika taifa la Yuda. Bethlehemu Efrata ulikuwa mji mdogo sana na wengi hawakuamini kwamba mji mdogo kama huu ungeweza kuwa mahali ambapo atazaliwa kiongozi. Hata hivyo, Mika alitabiri tukio hili, na likatokea. Nao huu ni mfano mmoja tu wa utabiri unaohusu Maandiko Matakatifu. Nao umetimia. Kuna mifano zaidi ya mia moja kama huu unaohusu maisha ya Kristo.

Mungu alisema hivi:

Nitangazaye mwisho hadi mwanzo, na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado; nikisema, shauri langu litasimama nami nitatenda mapenzi yangu yote (Isa. 46:10).

Mimi nimehubiri mambo ya kale tangu zamani; naam, yaliotoka katika kinywa changu, nikayadhihirisha; naliyatenda kwa ghafla yakatokea (Isa. 48:3).

Basi nimekuonyesha tangu zamani; kabla hayajatukia nalikuonyesha; usije ukasema,

sanamu yangu imetenda haya; sanamu yangu ya kuchonga, na sanamu yangu ya kuyeyusha, imeyaamuru (Isa. 48:5).

Historia imeonyesha kwamba maneno haya ya unabii kutoka kwake Mungu, na kuandikwa katika Biblia yametimia asilimia mia moja.

Uwezo Mkubwa wa Biblia

Sababu ya pili kuu inayoonyesha kwamba kweli Biblia ni Maandiko Matakatifu kutoka kwa Mungu ni kwamba Kitabu hiki kimeweza kuwa na ushawishi mkuu katika maisha ya wale wanaosikiliza yale yaliyoko katika Biblia, ama kuyasoma. Katika jamii, mila na kwa watu wengi, Maandiko Matakatifu yamewaletea wengi heshima katika mataifa mbali mbali duniani.

Kabla ya nakala mpya ya kitabu hiki *Kiu Cha Kumtafuta Mungu* haijapelekwa kwa wachapishaji, rafiki mmoja alitutembelea nyumbani. Pamoja tulipitia yaliyomo kwenye kitabu hiki. Ingawa huyu alikuwa ni mtu ambaye kawaida hakuwa mwepesi wa kutokwa na machozi, tulipofika sura ya saba, yeye alianza kububujikwa na majonzi. Ilitubidi tuache kusoma kitabu hiki mara mbili na badala yake tuanze kuomba maombi ya kumshukuru Mungu kwa ajili ya upendo wake uliokuwa unatajwa hapa.

Kwa pamoja, tulimshukuru Mungu kwa ajili ya upendo wake, na ustahimilivu, na pia uvumilivu na huruma anayoielekeza kwetu sisi wanadamu ambao ni viumbe visivyofaa kwa ajili ya dhambi zetu. Na

Je, Anayekuongoza Kiroho Aweza Kutegemewa?

tukiwa katika hali hii, tulijawa na furaha sana kwa kuwa Mungu alikuwa yuko pamoja nasi.

Siku ile ilikuwa maalum sana kwake huyu rafiki yetu. Ni mwaka mmoja ulikuwa umepita, alikuwa amekaa peke yake kwenye chumba cha kupumzika cha hali ya juu kikilinganishwa na chumba chetu. Uzuri wa chumba chake cha bei haukuweza kumjaza na furaha.

Kwa kweli, yeye alikuwa katika hali mbaya sana kimawazo hivi kwamba hata hakuona haja ya kuendelea kuishi. Na katika hali ile ya kutafuta furaha, na kujitimizia haja zake, yeye alijiingiza katika mambo mengi ambayo yalimfanya aishi kama mnyama.

Matumizi ya madawa ya kulevywa yalimfanya apoteze pesa nyingi mno. Pombe za aina mbali mbali zilifanya kila siku iwe ni sawa na mzigo mkubwa kwake. Kwa muda wa miaka mingi, yeye alikuwa ameshiriki katika karamu kubwa kubwa na watu maarufu sehemu mbali mbali Ulaya na kwingineko duniani. Hali hii ya upweke ilimfanya ajione kuwa katika dunia ambayo ni ya kutisha. Hakuona jinsi angeweza kujittoa katika hali hii.

Alijitoa siku moja, akaweka risasi katika bunduki yake, akailekeza kwenye kichwa chake tayari kujiua. “Niko umbali wa inchi 1/8 kutoka kusahaulika, na uchungu wangu utakuwa hauko tena.”

Na alipokuwa anajiandaa kwa njia hii kwa ajili ya kujiua, kipindi ambacho kilikuwa hewani katika runinga kilibadilishwa na mahali pake pakaletwa kipindi cha mafunzo kutoka maandiko Matakatifu. Funzo katika kipindi hiki lilikuwa na ujumbe wa

uliohusu siku za baadaye. Ilipokuwa inakaribia saa sita usiku, huyu ambaye alitaka kujiua alianguka sakafuni kwa ajili ya kumheshimu Mungu wake na kuomba kwamba asamehewe dhambi zake.

Na kwa vile nguvu za Bwana zilikuwa ndani yake wakati huu, yeye aliyekuwa mbele yangu wakati ule ni tofauti sana na huyu ambaye nimemtaja hapo. Kabla ya kuzaliwa, wazazi wake walikuwa wamemuomba. Na ingawa hata wakati wa utoto wa ujana wake alikuwa amesoma maandiko matakatifu, yeye alikuwa amekataa kutilia ujumbe wa maandiko haya maanani. Katika maisha ya utajiri na raha, yeye alikuwa amekataa kutilia maanani yale ambayo aliyuhusu Mungu. Aliasi yote ambayo ni ya kiroho na kufanya mengi ambayo ni dhambi kuu.

Miaka kumi na saba kabla ya usiku ule alipomjua Mungu, rafiki yangu huyu alikuwa amenunua kitabu mardiadai ambacho sehemu yake ya juu ilikuwa imetengenezwa na ngozi. Kitabu hiki kilikuwa na karatasi nyeupe ambazo zilikuwa hazina maandishi. Lengo lake lilikuwa kwamba ataandika ndani ya kitabu hiki matukio yote makuu maishani mwake. Ajabu ni kwamba katika muda huo wote wa miaka kumi na saba hakuwa hata na kisa kimoja ambacho aliona kilifaa kuandikwa katika kitabu hiki.

Ukweli ni kwamba katika miaka hiyo yote, baada ya kumuasi Mungu alikuwa sawa na msafiri ambaye amepitia barabara ndefu akitafuta jinsi ya kujitosheleza kiroho pasipo kufanikiwa. Yeye alianza na mtindo ule kusoma nyota kwenye magazeti, na kufurahia nyimbo za *rock*. Baadaye akajiingiza katika

Je, Anayekuongoza Kiroho Aweza Kutegemewa?

dini za kishetani. Na baadaye akaanza kujifunza mengi kuhusu dini fulani kutoka bara Asia na kwingineko huko mashariki ya mbali. Kati ya hayo yote, hakuna hata moja aliona kuwa lastahili kuandikwa katika kitabu chake kile cha bei. Hakuna hata karatasi moja ilikuwa na maandishi katika kitabu hiki. Ni hadi pale usiku alipokuja kumtambua Mungu ndipo aliona hamu ya kuandika kile ambacho ni tukio aliloliona kwamba lafaa kuandikwa katika kitabu hiki.

Niliwahi kupata nafasi ya kusoma kile ambacho aliniandikia. Yote aliyoyaandika yalikuwa maneno kutoka kwa mtu ambaye alikuwa na kiu kikubwa sana cha kumjua Mungu. Yale yaliyoandikwa yalikuwa maneno ya mtu ambaye kwa kweli amepokea wokovu kamili kutoka kwa Mungu mwenye upendo. Ni jambo lenye umaridadi kuliwaza kwani huyu ambaye alikuwa mbali na Mungu sasa alikuwa ameletwa karibu na kusamehewa dhambi zake. Kwa ajili ya upendo wake, Mungu alikuwa amepenyeza hali ile ya kutojua ukweli na kumfikia na hata kumuondolea hali ile ya kutowezakuona. Mungu alikuwa amemuondoa kutoka mauti kupitia njia ya kumonyesha ukweli na pia kumpa upendo wa ajabu.

Ni kwa ajili ya hali yetu ya kutojua sawa na hali ya rafiki huyu ndio sababu Mungu amejionyesha wazi kwetu **kupitia** Maandiko Matakatifu ambayo ni Biblia. Ukitupilia mbali Maandiko Matakatifu, ukafuata mwongozo tofauti wa kiroho mbali na maandiko haya, wewe utakuwa umejiweka mfungwa katika uongo na kuwa mtu aliyekosa. Hata hivyo ikiwa unatafuta Mungu, wewe **utayarudia** Maandiko

Kiu Cha Kumtafuta Mungu

Matakatifu, utakuta kwamba hapa panapatikana mwanga wa kiroho, na ishara ya kukuonyesha njia inayofaa.

Ni Maandiko Matakatifu yatatuwezesha kumjua Mungu jinsi vile yeye alivyojijulisha kwetu sisi wanadamu. Katika kitabu kitakatifu, sisi tunaelezwa na kujulishwa ukweli kuhusu neno lake hili, ambalo ni taa ya dunia.

Mungu wetu, neno lako litazidi kusimama
Neno hili litazidi kuongoza mienendo yetu;
Hasa kwa wale walio na imani
Wao watapata mwanga wa kuwaongoza na
furaha.

Je, Anayekuongoza Kiroho Aweza Kutegemewa?

Hebu Fikiria

1. Je, yako maandiko yeyote ambayo yaweza kulinganishwa na Maandiko yetu matakatifu katika kutabiri matukio ya baadaye?
2. Je, unamjua yeyote ambaye maisha yake yamebadilishwa kwa ajili ya kutii neno la Mungu jinsi vile linavyoptikana katika Maandiko Matakatifu, Biblia?
3. Je, umewahi kuyadharau mafunzo maalum katika Maandiko Matakatifu, na hata ukakosa kusoma maandiko haya?

*Shida katika dunia na mbingu zote
zikutujia kwa pamoja, haziwezi zikawa
na madhara makuu sawa na ile shida
inayohusu Kumjua Mungu. Je, Mungu ni
nani? Na je, sisi wanadamu wa kawaida
twafaa tuhusiane na Mungu wetu kwa
njia gani?*

A.W. TOZER

Mungu ni Nani?

*W*akati fulani maishani, wengi wetu huuliza: “Mungu ana maumbile gani?” Ingawa Mungu amejibu swali hili, wako wale ambao bado wanategemea mawazo yao wenyewe kujibu swali hili. Badala ya kusoma Biblia ambayo ina jibu la swali hili, wao wanatumia mawazo na akili yao kujibu swali hili la muhimu ambalo Mungu mwenyewe amelijibu katika Biblia.

Watu kama hawa huchukua kinyume kabisa wazo kuu ambalo limeandikwa katika Biblia ambapo Mungu anasema: *na tumfanye mtu kwa mfano wetu (Mwa. 1:26)*. Wameugeza usemi huu kuwa: “na tumfanye Mungu kwa mfano wetu.” Na kwa usemi huu, wao wamebadili mengi jinsi vile tunavyosoma katika Warumi 1:23, *Wakaubadili utukufu wa Mungu asiye na uharibifu kwa mfano wa sura ya binadamu aliye na uharibifu, na ya ndege, na ya wanyama, na vitaambaavyo (Rum. 1:23)*. Miungu yote ile ambayo mwanadamu amewahi kujitengenezea imekuwa miungu isiyo na nguvu. Ni miungu ya kuchekesha.

Haijalishi ni akili na ujuzi wa kiasi gani mtu anao. Ukweli ni kwamba mwanadamau hawezi akagundua Mungu kwa kupitia matumizi ya ujuzi wa

dunia. Katika wakorintho twasoma hivi: *Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile neno linalohuburiwa (1 Kor. 1:21). Kama Mungu angeweza kujulikana kupitia akili ya wanadamu, yeye angekuwa Mungu wa ujuzi wa kiwango cha chini sana. Na kama akili ya mwanadamu ndio ingekuwa kitu cha kumwezesha mtu kumjua Mungu, basi wale wasio na akili nyingi hawataweza kumjua Mungu vilivyo.*

Lakini mambo sio hivyo. Ukweli ni kwamba akili ya kiroho iko kwa kila mtu anyetaka kupokea roho huyu. Akili ya kumwezesha mtu kumjua Mungu iko naye mama mzee anayetembea kwa kutumia fimbo sawa na jinsi vile aliyo nayo mkufunzi wa chuo kikuu. Ujuzi na akili za kiroho hazipatikani kupitia masomo ya shule na kadhalika. Wanaopata akili ya kiroho ni wale wanyeynyekevu na wako tayari kutambua wanahitaji usaidizi wake Mungu wanapomtafuta Mungu.

Lakini mtu wa kwetu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa (Yak. 1:5).

Akili kama hii siyo ya dunia ila ni akili kutoka mbinguni. Hii ni akili ambayo wenye kuitawala dunia hii hawajui hata mmoja; maana kama wangalijua, wasingamsulubisha Bwana wa utukufu (1 Kor. 2:8).

Mungu ni Nani?

Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kujua tuliyokarimiwa na Mungu (1 Kor. 2:12).

Biblia sio tu maandishi ya kidini ya kubishaniwa. Biblia ni maandishi yanayoeleza jinsi vile Mungu amejifichua kwa wanadamu. Ni Mungu mwenyewe anayeweza kukupatia ujuzi wa kiroho kukuwezesha kuelewa yeye ni nani, na ni yapi anataka ufanye maishani. Ukitaka uwe na hamu ya kumwuliza, basi yeye atajijulisha kwako kupitia Neno lake Takatifu.

Unapoomba na kutaka basi Mungu atajidhishisha mwenyewe kwako kupitia neno lake takatifu.

Katika safari zetu, tumepata ufahamu na ujuzi sehemu ambapo wengi wetu hatuwezi kutarajia lolote la busara, na pia kutoka kwa watu ambao hatukutarajia mambo mengi. Kwa mfano, siku moja, tulikutana na vijana chipukizi vichakani nchini Kenya, nao walionekana kuwa na hamu ya kutueleza jinsi vile walivyo na imani. Pia walionyesha hamu kuu ya kumjua Mungu zaidi.

Jua kali la sehemu hii lilikua laelekea kutua. Nami nikaamua kukaa chini kwenye mawe sehemu ya vumbi ili nikapumzike na hapo nikasikia miguu ya mtu akinikaribia kutoka kichakani. Nilipinduka nyuma kuangalia na hapo nikayaona macho ya kijana mwafrika yakimeta meta kwenye mwanga wa mwezi jioni hiyo. Baada ya muda mfupi, kijana huyu wa umri wa kama miaka kumi hivi akanikaribia, na kukaa

kando yangu. Baada ya muda mfupi, tukawa marafiki. Na punde si punde, vijana wengine wakasikia sauti zetu. Nao wakajitokeza, na wakakaribia ili washiriki pia katika majadiliano yetu. Ujuzi wao wa Biblia ulinishangaza sana.

“Mbona Mungu hakumkubalia Musa aone uso wake,” kijana mdogo sana kati yao akaniuliza.

Nikashikwa na mshangao kwa ajili ya swali hili. Na nikamwuliza kijana huyu ambaye kwa jina aliitwa Yoeli. Nikataka kujua kama angekumbuka ombi lake Musa kabla Mungu hajamwambia yafuatayo: *nawe utaniona nyuma yangu, bali uso wangu hautaonekana (Kut. 33:23).*

Kijana huyu hakuweza kukumbuka ombi hili. Basi nikamkumbusha kwamba ombi lake Musa lilikuwa hili: *nakusihii unionyeshe utukufu wako (Kut. 33:18).*

Maana ya tamshi hili ni kwamba Musa alimwomba Mungu amuonyeshe yeye yuko na umbo gani. Hata hivyo, Mungu alijua kwamba ombi hili lilikuwa na shida, kwa vile utukufu wa Mungu ulikuwa zaidi ya yote ambayo Musa angeweza kuelewa. Utukufu wa Mungu ambao mng'aro, uweza wake na mwanga wa yote yanayomhusu ni wa nguvu kiasi kwamba yeye mwenyewe amesema: *Huwezi kuniona uso wangu, maana mwandamu hataniona akaishi (Kut. 33:20).*

Musa hakua anajua jinsi utukufu wa Mungu ulivyo na jinsi utukufu huu unawezamzidi akiuona na macho yake. Hata hivyo, Mungu wetu ni Mungu ambaye hujifichua. Kwa ajili ya sababu hiyo, alimkubalia Musa aweze kuuona utukufu wake hadi kiwango fulani kilichomfaa.

Mungu ni Nani?

Na kama angejitoa kuoenekana wazi kabisa, basi mwanga wa utukufu wake ungemzidi Musa. Hata ingawa Mungu aliuficha utukufu wake, alimkubalia Musa kujificha mahali maalum: *Kisha itakuwa wakati uanpopita utukufu wangu, nitakutia katika ufa wa ule mwamba, na kukufunika kwa mkono wangu hata nitakapokuwa nimekwisha kupita (Kut. 33:22).*

Wakiwa watu wanaoishi katika sehemu yenye jua kali, Equator, marafiki wangu hawa chipukizi walielewa vyema jinsi vilivyo vigumu kutazama na macho jua kali la mchana. Vijana hawa pia walijua kwamba vipepeo hukimbilia kwenye mwanga wakati wa giza. Nilipowauliza ni nini hutokea pale vipepeo hukaribia kabisa mwanga, wao walinijibu kwa sauti moja: “Vipepeo huchomeka na kufa.” Ni wazi vijana hawa walifahamu hatari ya kukaribia mwanga.

Basi nikaanza kufikiria juu ya mfano tofauti ambao ungewasaidia kuelewa vyema jibu la swali lao kuhusu Musa. Sikuwa na shaka kwamba vijana hawa walielewa vyema jinsi vile ndugu na dada wao wachanga hufungwa na nguo vyema karibu na mama ili wasidhuriwe na baridi na kadhalika.

Watoto huwekwa karibu kabisa na moyo wa mama mzazi kwa ajili ya upendo wake kwao na utunzi bora. Basi niliwaeleza marafiki wangu hawa kuhusu jinsi vile Mungu ametuweka karibu kabisa na roho yake jinsi tunavyosoma katika kitabu cha Ayubu.

Nilipolifanya wingu kuwa vazi lake, na giza zito kuwa nguo ya kuifungia (Ayu. 38:9).

(Kuna gesi iitwayo ozone ambayo huzingira dunia yetu ili tusidhuriwe na miali ya joto kutoka kwa jua. Kama hatungekuwa na jua, hatungekuwa na uhai ardhini. Lakini kwa vile jua laweza kutudhuru, Mungu mwenyewe kwa njia ya ajabu amepanga jinsi ya kutuinga tusidhuriwe na miali ya jua ambayo hata huweza kusababisha maradhi ya saratani.)

Marafiki wangu hawa chipukizi walikuwa na hamu kuu ya kujua mengi kuhusu jinsi vile Mungu hutuepusha na shida kwa kutuinga. Sina uhakika kwamba walielewa vyema yale niliyokuwa nawaeleza, ila sina shaka kwamba mioyo yao changa iliweza kupokea upendo na utukufu wa Mungu. Baadaye tuliomba pamoja na vijana hawa. Ni wazi kwamba vijana hawa waliweza kuhisi na kujua kwamba Mungu anawapenda na yuko anawalinda ili wasidhuriwe na mengi yanayowazingira jinsi vile alivyomlinda Musa wakati wa kumtafuta Mungu. Mungu ametupatia jina lake ili hii iwe njia moja ya kutusaidia tuweze kumjua na kumuelewa vyema. Msingi kamili wa maoni yetu na kuhusu maumbile ya Mungu wetu katika Biblia kitabu cha Walawi 6:4 kwamba Mungu ni utatu katika **umoja** ni msingi kamili wa imani.

Na ili kutuwezesha kuelewa vyema yeye ni nani, Mungu ametupa majina yake.

Katika Biblia, jina ni kitu cha muhimu sana kwa vile jina huwa na uhusiano fulani na tabia ya yule aliye na jina hilo. Kila jina la Mungu lina maana maalum. Nalo jina pia hufichua mambo fulani yanayohusu utukufu wa Mungu.

Mungu ni Nani?

Katika Agano la kale, haya ndiyo majina ya Mungu: Yehova, Elohim, Adonai. Kila jina lina umaarufu wake. Elohimu ndilo jina la kwanza la Mungu kuwahi kutumiwa. Nalo jina hili limetumiwa zaidi ya mara elfu mbili. Ingawa jina Yehova ndilo la muhimu kabisa, jina Elohimu lina umuhimu fulani ambao Mungu anataka tuutilie maanani.

Katika kiingereza, yako maneno fulani yanayotumiwa tunapotaja vitu vingi. Pia yako maneno yanayotumiwa kutaja kitu kimoja. Lakini katika lugha ya Kiebrania, yako maneno yanayotumiwa kutaja vitu viwili, na hata zaidi ya viwili. Tofauti ya matamshi haya ni yaa maana sana kwa sababu jina hili Elohimu ni jina la vitu zaidi ya viwili.

Hata hivyo, katika Kumbukumbu la Torati, tunasoma hivi: *Bwana Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja (Kum. 6:4).*

Kwa hivyo, katika msitari wa kwanza wa biblia, ambayo ni mkusanyiko wa maneno ambayo Mungu mwenyewe ametufichulia ili tuweze kumjua twamawona Mungu ambaye ni Mugu katika utatu; na watatu katika mmoja ambaye ni Mungu. Hapo mwanzo (Elohimu) aliziumba mbingu na nchi (Mwa. 1:1).

Kwa hivyo, Mungu wetu ni Mungu aliye katika utatu.

Na tunapozidi kusoma mistari inyaofuata inayohusu utatu wake Mungu, tunafikia pale ambapo Mungu anamwumba mwanadamu. Na hapa utatu wa Mungu wajitokeza wazi kabisa, wakati wa kumwumba mwanadamu, Mungu akasema: *na tumfanye mtu kwa*

*mfano wetu, kwa sura yetu (Mwa. 1:26).**

Ni wazi kwamba tamshi hili, “tumfanye” lamaanisha Mungu anashirikiana na wengine kumuumba mwanadamu. Tukiendelea, tunasoma hivi: “...mwanamume na mwanamke aliwaumba” (Mwa. 1:27).

Na hapa tunasoma, “aliwaumba” yaani yeye mmoja tu ndiye aliyafanya haya. Kwa hivyo basi, tunaona hapa kwamba, wakati fulani yeye ni mmoja, na uko wakati ambapo ni zaidi ya mmoja. Hata hivyo, kila mara yule anayetajwa ni Mungu, Elohimu.

Mungu kama huyu ni Mungu ambaye wanadamu wa kawaida hawawezi kumuelewa. Na hii ndio sababu Mungu amewapa wanadamu Roho Mtakatifu awasaidie. “*Lakini sisi hatukuipoke a roho ya dunia, bali roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu*” (1 Kor. 2:12).

Na tukianza na haya kuhusu Mungu, yeye anaendelea kufichua mengi kuhusu utatu wake na utukufu wake wa milele. Tukielewa utatu huu wa Mungu, hii itakusaidia kuweza kumjua Mungu zaidi, na urefu na upana wa upendo wake Mungu.

Na kweli kabisa ili kumjua Mungu na kuelewa ukuu wake, Mungu mwenyewe ajitoa katika Maandiko Matakatifu Biblia. Hapa tunajulishwa kwake Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu. Hata hivyo, yeye bado ni Mungu mmoja.

* Ni jambo la muhimu kuelewa kwamba kuumbwa kwa mwanaume na mwanamke hakuwezi kufananishwa na jinsi vile mimea, na chochote kimeumbwa duniani. Wanadamu wameumbwa mfano wa Mungu kwa hivyo, mwanadamu ni kiembe cha ajabu.

Mungu ni Nani?

Akili zetu za kibinadamu haziwezi kuelewa vyema haya, ila huelewa kwa umbali haya yote. Na kwa vile mwanadamu hakuweza kumjua Mungu jinsi vile alivyo kupitia uwezo wake mwenyewe, basi ndipo Mungu akajitoa na kujieleza mwenyewe k w a ke mwandamu.

Ukweli wote kumhusu Mungu na utukufu haukuonekana mbele ya macho yake Musa. Hata hivyo, kupitia Mungu Mwana (Elohimu) yeye amejifichua hadi kiwango cha kumtoshia na kinachostahili mwandamu.

Kwa kuwa Mungu, aliyesema, nuru itang'aa toka gizani, ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo (2 Kor. 4:6).

Hebu fikiria: wakati Yohana alipotazama uso wake Yesu Kristo, alisema hivi: *Nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa mwana pekee atokaye kwa baba; amejaa neema na kweli (Yn. 1:14).*

Yohana aliandika jinsi vile alivyokutana na Mungu kwa ajili alikuwa amekutana na Elohim ambaye ni Kristo, aliweza kueleza wengi wetu yale yaliyotokea. Hata hivyo, yeye alifafanua kwamba yeye alikuwa amemuona Mungu wa Milele, Mungu muumabji, na Mungu wake Musa. Mkutano huu ulikuwa ni mkutano uliosikika, na ukaonekana ulio wazi, dhahiri na hakika.

Lile lililokuwako tangu mwanzo, tulilolisikia (KUSIKIKA) tuliloliona (KUONEKANA) kwa

macho yetu, tulilolitazama, na mikono yetu ikalipapasa (DHAHIRI), kwa habari ya Neno la Uzima (1 Yoh. 1:1).

Haya aliyoandika Yohana ni Ushuhuda wake mwenyewe baada ya kukutana na Mungu aliye hai.

Huenda ukawa unajiuliza: “Je, haya yatanisadia kwa njia gani?” Yohana mwenyewe anajibu hivi: *na haya twayaandika ili furaha yetu itimizwe (1 Yoh. 1:4).* Kitabu hiki unacho mkononi kwa sababu rafiki yako mpendwa ana hamu kwamba upokee furaha ya kumjua Mungu na ndio sababu rafiki huyu amechangia gharama ya uchapishaji kitabu hiki.

Yohana anafafanua zaidi:

Hilo tuliloliona na kuliskia, twahubiria na na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na mwana wake Yesu Kristo, na haya twayaandika ili furaha yetu itimizwe (1 Yoh. 1:3,4).

Sawa na jinsi vile mwanga huwa kitu chenye umaridadi kwenye giza, mwanga wa utukufu wa Mungu nao pia huwavutia watu kwake yeye mwenyewe. Leo, katika hamu yako ya Kumjua Mungu, waweza pia kuomba ombi sawa na lile la Musa: “Nionyeshe utukufu wako!”

Hebu Fikiria

1. Katika harakati ya kutafuta jinsi ya kumjua Yesu, umesoma Biblia kwa makini?
2. Je, utamuomba Mungu ajifichue kwako unaposoma Biblia?

Waweza kuomba hivi: “Mungu wangu, kama wewe ni Mungu aliyeumba anga na dunia, na anayenipenda, jifichue kwangu na unionyeshe kama kweli Yesu Kristo ni mwana wa Mungu na Masihi naye anayetarajiwa.”

3. Je, unatambua kwamba ikiwa kweli unataka kusali, basi Mungu huyu lazima: awe mkuu kuliko uwezo wako wa kumjua mwenyewe kupitia utafiti; na pia uwe na uwezo ambao huwezi kuuelewa wewe mwenyewe ukitumia akili na mawazo yako ya kibinadamu.

*Nafikiri naelewa maumbile ya
mwanadamu, na nakujulisha kwamba
mashujaa wa zamani walikuwa
wanadamu nami pia ni mwanadamu;
hata hivyo hakuna hata mmoja aliye
kama yeye, Yesu Kristo ni zaidi ya
mwanadamu.*

NAPOLEON

Ni Nini Kinachowagawanya Wanadamu?

Dunia yetu ya leo inaweza kufananishwa na kijiji ambacho ni mkusanyiko wa mataifa yote, yaani, “global village”. Hata hivyo, ingawa dunia ni sawa na kijiji, wenyeji katika kijiji hiki ni maadui. Kijiji hiki sasa kimekuwa ni mahali pa ugomvi na uhasama wa aina mbali mbali.

Ukiangalia juu juu, sababu ya migawanyiko huwa ni siasa, uchumi, kutoelewana katika jamii moja na ugomvi viwandani. Ingawa kweli shida hizi tumetaja hapa ndizo huwa chanzo cha migawanyiko, kuna sababu moja kuu ambayo watu wengi hawajaitambua.

Hebu tuchunguze sababu hizi kwa undani.

Sababu zilizo wazi

Siasa: Kila mwanasiasa huandama mwenzake na woga na moyo wa kutoaminiana. Na wanapokosa kukubaliana, wanasiasa wengi huamini kwamba

majeshi yao ndio yatawahakikishia usalama wa siku za baadaye.

Nao wananchi wa kawaida wanaohusika wanaposema na sauti za juu kwamba wanataka amani, wanataka silaha hatari za niuklia ziondolewe na mengine mengi. La kustajabisha ni kwamba wengi wetu ambao hushuhudia maandamano haya huwaona kuwa na hasira sawa na wale ambao wako tayari kwa ajili ya vita.

Uchumi: Mikasa ya kimaumbile kama vile ukame, njaa, mitetemeko ya ardhi huzidisha shida zilizoko hasa katika nchi za ulimwengu wa tatu. Mikasa hizi huongeza maafa na pengo liliko kati ya mataifa tajiri na yale masikini. Na ingawa kuna wale wenye roho ya kutaka kuwasaidia masikini, wamejitoa na kujitahidi kufanya hivyo. La kusikitisha ni kuona kwamba matajiri wanazidi kutajirika; nao masikini wanazidi kuwa masikini.

Jamii: Si jambo la siri kwamba siku hizi ndoa nyingi zinavunjika. Familia nyingi zina shida. Huku machozi yakimdondoka, Letsoale alisema hivi: “Nyumba yangu imevunjwa.” Nilidhani kile alichomaanisha ni kwamba nyumba yake ya kuta nne mjengo wa kiafrika, ilikuwa imebomolewa. Lakini haikuwa hivyo: kile Letsoale alimaanisha ni kwamba mke wake alikuwa amemwacha na kwenda zake. Leo hii, ni nyumba nyingi sana zinabomoka. Mienendo ya uchoyo inavunja nyumba nyingi mno. (Lakutia moyo ni kwamba katika sura moja baadaye, tutaangalia jinsi

vile upendo wa Mungu unaweza kuweka walioona pamoja daima.)

Viwandani: Katika sehemu nyingi za kazi, habari ambayo hujitokeza kila mara ni kwamba kuna migomo na ugomvi. Mnamo mwanzo wa mwaka wa '85, ugomvi mkali sana kabisa karne hii kazini ulifikia kikomo chake Uingereza. Ingawa migomo na maandamano barabarani yalikoma, uchungu na hali ya kutoaminiana iliendelea kati ya waajiri na walioajiriwa. Hii ni tofauti sana na matokeo ya ugomvi wa viwandani katika migodi ya makaa ya kule Wales mwaka wa 1904. Niliwahi kuelezwa yaliyotokea na mhusika mmoja kwa jina John Pa r r y.

Mara yangu ya kwanza kukutana na John, yeye alikuwa na umri wa miaka 91, na tayari alikuwa amestaafu. Yeye alikuwa tayari amepoteza uwezo wa kuona. Mapafu yake nayo yalikuwa yakiugua maradhi yanayoitwa “miner’s disease.”

Kila tulipopata nafasi, mimi na mke wangu Dorothy tulimetembelea mzee huyu katika chumba chake kidogo kaskazini mwa Wales. Huku akiwa mwenye furaha tele, John alizoea kutueleza yale ambayo yalitokea Wales wakati Roho Mtakatifu alipoleta ufufuo sehemu hiyo mwaka wa 1904 na 1905. Wakati huo, wachimba mawe katika migodi pamoja na waajiri wao walikuwa wamekutana na Mungu aliye hai. Na kwa ajili ya tukio hilo, kulikuwa na umoja, hali ya kuelewana na hata kuheshimiana. Tofauti kati ya ugomvi wa 1904-5 na 1985 ulikuwa mkubwa.

Alipokuwa akitusimulia kuhusu mwaka huo, John alikuwa na furaha tele kwa ajili ya kukumbuka yale yaliyotokea. Alitudokezea kwamba sehemu za kuuzwa pombe nyingi zilifungwa kwa ajili ya kukosa wateja, wanywaji walikuwa ni wachache sana. Aliweza kukumbuka pia jinsi vile yeye na wafanyi kazi wenzake walivyokuwa na mtindo wa kushuka kwenye migodi hiyo huku wakiimba nyimbo za sifa.

“Watu bado huja kuniuliza uamsho huo ulitoka wapi.” Akipapasa kifua chake akisema, “Nami nawajibu, uamsho huo uko chini hapa na hivi sasa.”

Mchanganyiko Kamili

Hata ingawa tumetaja sababu zinazoleta migawanyiko, kuna kitu fulani ambacho kinawagawanya wanadamu kwa njia ya hatari isiyoweza kugeuzwa. Hatari ni ile inayotisha kuharibu na kuondoa amani sehemu nyingi. Watu wengi wamegawanyika kwa ajili ya kumuelewa Mungu kwa njia isiyo sahihi.

Katika kujifichua kwa wanadamu, Mungu hajawahi kutupilia mbali ukweli kuhusu utukufu wake. Kabla kuzaliwa kwake Kristo, Mungu alisema atatuma mwangaza utakaowasaidia watu ili waweze kumjua jinsi vile alivyo. Yeye alisema wenye kutembea kwenye giza wataona mwanga.

Watu wale waliokwenda katika giza, wameona nuru kuu; wale waliokaa katika nchi ya uvuli wa mauti, nuru imewaangaza (*Isa. 9:2*).

Pia Mungu alieleza jinsi vile nuru hii ingetambulikana:

Ni Nini Kinachowagawanya Wanadamu?

Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa. Tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wake wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, mfalme wa amani (Isa. 9:6).

Kwa kweli maneno haya hayangekuwa na umuhimu wowote ikiwa Mungu angesema tu kwamba mtoto atazaliwa, ni kawaida watoto kuzaliwa. Kwa kweli halingekuwa jambo la kutiliwa maanani kuzaliwa kwa mtoto pasipo ujumbe kwamba mtoto huyu tumepewa.

Sasa yale yaliyokuwa utabiri yametimia kwa hivyo yote sasa ni historia kwa vile yale Mungu alisema yatatokea yametokea. Hapa duniani, mtoto alizaliwa, na huko mbinguni, mtoto huyu tulipewa. Kupitia kuzaliwa kwa mtoto huyu, Mungu amewapa wanadamu nuru ambayo itawaangazia wale waliokuwa katika giza. Hata leo, nuru hii bado yaangaza kuondoa giza na roho ya kutoamini inayoweza kuwaficha watu kutoka machoni pa Mungu.

Ili kuzaliwa kwa mtoto huyu kuwe tofauti sana na kuzaliwa kwa watoto wa kawaida, Mungu aliagiza kwamba atakuwa na ishara maalum wakati wa kuzaliwa kwake. Katika Isaya twasoma hivi:

Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara. Tazama bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanuel (Isa. 7:14).

Ni jambo la kufurahisha sana kwamba jina lake mtoto huyu ni Imanuel ambalo maana yake ni:

“Mungu pamoja nasi.” Na ametuletea habari njema hata kupitia Biblia, na hii ndiyo sababu imani yetu inatofautiana kabisa na imani kutoka dini mbali mbali. Dini nyingi hufundisha jinsi vile mwanadamu anvyoweza kumfikia Mungu; Biblia inafundisha jinsi Mungu ametufikia sisi wanadamu hapa duniani.

Jinsi vile ilivyoandikwa katika Biblia, Mungu alipojenga makao hapa duniani, bikira alikuwa tayari ana mtoto tumboni mwake. Na siku ile ambapo muumba alikubali kuwa sehemu ya anga na saa, haya yote ni mambo ya kihistoria. Twasoma hivi: *Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusuifu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu (Mt. 1:20).* Na baada ya kukua, na kufikia umri wa mtu mzima, yeye alithibitisha kwamba ni Mungu mbele ya maadui wasioamini kwa kusema: *Mimi na Baba tu umoja (Jn. 10:30).*

Mwana anga Jim Irwin ambaye alisafiri hadi mwezi kwa kutumia chombo cha Apollo XV aliandika hivi: “Mungu kutembea ardhini ni jambo muhimu kuliko mwanadamu kutembea mwezini.”

Kwa kweli maajabu ambayo mwanadamu ameyatimiza mwezini hayawezi yakalinganishwa na ule muujiza uliotokea Mungu alipokubali kutoka kwenye ufalme wake wa milele na kuja kuwa nasi hapa duniani.

Baada ya unabii na utabiri kuhusu kuzaliwa kwa mtoto, na kwamba tutapewa mtoto huyu, maelezo zaidi yalifuata kumhusu:

Ni Nini Kinachowagawanya Wanadamu?

Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, mfalme wa amani. Maongeo ya enzi yake ya amani hayatakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele. Wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo (Isa. 9:6,7).

Kwa kweli, mchanganyiko huu wa nguvu na uweza unahitajika na mtu ambaye anastahili kutawala dunia yote. Hata leo, tunatafuta viongozi walio na ujuzi na uwezo wa kufanya mambo fulani. Wa ko viongozi ambao inawezekana walijua ni yapi wanastahili kufanya; hata hivyo hakuna kiongozi ambaye ameweza kuleta amani duniani.

Mfalme wa amani ana ujuzi na nguvu kuweza kuleta amani ya milele hapa duniani. Siku moja, Kristo atarudi kutawala duniani. Siku ile itakapofika, kila kiwanda cha kutengeneza silaha kitafungwa, kila bomu la hatari la niuklia litaharibiwa, naye kila askari wa mpakani, na wale wa majeshi wataamriwa kurudi nyumbani.

Tayari mwanadamu ameonyesha jinsi vile hana uwezo wa kutawala wanadamu wenzake. Amani na haki kwa wote itangoja mpaka pale mfalme wa amani mwenyewe atakaporudi duniani na upanga wa utawala.

Na hapo naye atafanya hukumu katika mataifa mengi, atawakemea watu wa kabila nyingi; nao

watafuata pango zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu; taifa halitainua upana juu ya taifa lingine, wala hawatajifunza vita tena kamwe (Isa. 2:4). Na siku hiyo: Kwa maana dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa BWANA, kama maji yaifunikavyo bahari (Hab. 2:14). Hakuna mengine ya kukamilisha historia yawezayo kumfurahisha Mungu milele yasiyo kama haya.

Lakini kabla ya amani hii itakayoletwa na Kristo kote duniani, hali ya mgawanyiko na kutoelewana kati ya watu itaonekana wazi. Ugomvi utakaozuka utamhusisha Kristo. Kwa hivyo, ni jambo la muhimu kabisa kumjua yeye ni nani, ni kwa nini amekuja, na ni nini alifanya kwa ajili yako alipokuwa hapa dunia ni.

Kwa hivyo ni jmabo la muhimu kwamba uelewe na uwe na uhakika kuhusu Yesu Kristo ni nani, ni kwa nini alikuja hapa duniani na yapi alifanya kwa ajili yako hapa duniani.

Kitabu cha Mwanzo na kitabu cha Yohana vinaanza kwa njia inayofanana. Katika Mwanzo tunasoma hivi: *Hapo mwanzo Mungu alizimuba mbingu na nchi (Mwa. 1:1).*

Na katika Yohana tunasoma hivi:

Hapo mwanzo kulikuwako neno, naye neno alikuwako kwa Mungu, naye alikuwa Mungu (Yn. 1:1). Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika (Yn. 1:3).

Mungu anayeitwa Elohimu katika Mwanzo, ni yeye anayeitwa “Neno” katika waraka wa Mtume

Ni Nini Kinachowagawanya Wanadamu?

Yohane. “Elohim” ni neno, naye alivaa neno hili kama vazi, akatembea nalo kati yetu. Neno lilikuwa kama miili yetu na kuishi kati yetu. Haya yote twayasoma hapa:

Hapo mwanzo kulikuwako neno, naye neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyu mwanzo alikuwako. Vyote vilifanyika kw huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika (Yn. 1:1-3).

Alikuwako ulimwenguni, hata kwa yeye ulimwengu ulipata kuwako, wala ulimwengu haukumtambua. Alikuwa kwake, wale walio wake hawakumpokea. Bali waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake; waliozaliwa sio kwa damu wala sio kwa mapenzi ya mwili, wala sio l kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu. Naye neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli (Yn. 1:11-12).

Naye neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama mwana pekee atiokaye kw Baba; amejaa neema na kweli (Yn. 1:14).

Sawa na Musa wa karne za hapo zamani, Filipino naye alitaka kujua Mungu yuko je.

Filipo alimisihi Mungu na matamshi haya: *Bwana tuonyeshe baba (Yn. 14:8)*. La ajabu ni kwamba Kristo alimjibu, *Yeye ambaye ameniona, ameona Baba (Yn.*

14:9). Jibu kama hili lingemfanya Yesu aonekane kuwa kama mtu mwenye akili pungufu ama mwongo kama hangekuwa ni Mungu mwenyewe. Hakuna yule angeweza kusema kwamba yeye ni punguani; wala kwamba yeye ni mwongo. Kama hangekuwa Mungu, basi yeye angekuwa ni mtu wa kujiwekea mamlaka ambaye hayajawahi kuonekana duniani. Kwa hivyo, ni lazima tukubali kwamba tunapomuangalia Yesu, tunamuona Mungu.

Ni wakati huu tunapokiri haya kuhusu Kristo ndipo migawanyiko hutokea. Si ajabu kwamba Yesu aliposema *Mimi na Baba tu kitu kimoja (Yn. 10:30)* w a ko waliopata jibu la kuwasaidia katika harakati zao za kumtafuta Mungu. Hata hivyo wale ambao hawakuamini na kukubali kwamba Mungu anaweza akajihusisha kiasi hiki walipinga haya na ukali. Kristo aliwavutia watu wengi; wengi nao wakasonga mbali naye. Ingawa kulikuwa na wale ambao walimfuata Kristo, wako wale ambao nao walipinga jinsi ya kumuua.

Hata alipokuwa hapa duniani, Yesu alikuwa chanzo cha mgawanyiko.

Yeye ambaye hayuko nami hanitaki, hayo ndiyo aliyoyasema katika (Mt. 12:30).

Hata hivyo jinsi vile wewe utakichukua jambo kama hili haifai kuwa ndio njia yako ya pekee ya kuthibiti hali kama hii.

Hata hivyo, jinsi vile unavyopokea ujumbe huu mara ya kwanza kabisa haifai iwe ndio njia yako ya

kuupokea ujumbe huu milele.

Na hebu sasa tuchunguze hali ya mtu mmoja ambaye mwanzoni alimchukia Kristo, na baadaye akawa mfuasi halisi kabisa wa Mwokozi wetu.

Katika ujana wake, yeye aliitwa Saulo, mwalimu wa Wayahudi. Yeye aliwachukia sana wafuasi wa Kristo akawa hata anawatesa na kuwaweka katika shida nyingi sana. Wa ko wale ambao waliaga dunia kutokana na mateso yake. Jina lake hapo mwanzo lilikuwa ni Saulo. Saulo alibadilika, akaitwa Paulo, na katika maisha yake ya baadaye, akawa anamshukuru na kumsifu Kristo na kushuhudia kwamba yeye ni Mungu.

Mwishowe, alipitia taabu na mateso kwa ajili ya imani yake.

Je, ni nini kilileta mabadiliko haya katika Saulo?

Wakati Saulo alipokuwa yuko safarini kuelekea Dameski, aliona nuru kuu ya mwanga wa rangi ya kijani kibichi. Nuru ilikuwa na mwanga mkubwa hata ukamfanya apoteze uwezo wa kutumia macho yake. Hata hivyo, Saulo alijua kwamba yuko mbele ya Mungu.

Kwa kutumia jina la Kiyunani la Yahweh, akauliza: *Wewe ni nani?* Mungu naye akamjibu: *Mimi ni Yesu unayemtesa (Mdo. 9:5)*. Na siku hiyo Saulo akagundua kwamba Yahweh na Yesu ni mmoja.

Kufichuliwa na kufunuliwa kwa siri hii kulimbakilisha Saulo akawa mtume Paulo. Tangu siku hiyo akaweka maisha yake mikononi mwa Yesu Kristo. Na ingawa alipitia mateso mengi, Paulo alitumia siku zote za maisha yake kueneza

habari njema kwamba Mungu alikuwa ametembelea ulimwengu wetu huu. Ukweli wa Kristo katika maisha yake Paulo ulimbadili na kumfanya awe mmoja wa wamishonari wakuu katika enzi zote. Nyaraka zake zote zimejaa maelezo kuhusu imani yake kwamba kila kiumbe kimeumbwa kwa ajili ya Mungu na Yesu Kristo (*Wa kolosai 1:16*).

Na jinsi tulivyoona tayari, Biblia inasema wazi kwamba Yesu Mnazaraeti **ni** Mungu mwana, sio **tu** mwana wa Mungu jinsi vile wafuasi wa dini kama “Mormons” au mashahidi wa Yehova na wengine wengi wanavyoaminini. Na isitoshe, yeye hakuwa nabii wa Mungu **tu** jinsi vile mafunzo ya kiislamu yanavyosisitiza. Na katika jitihada zao za kueneza mafunzo ambayo si sahihi, vikundi fulani havitilii maanani wala kutilia mkazo yale ambayo Mungu anasema kumhusu yeye mwenyewe. Mafunzo haya potovu yanaitwa “Syncretism”. Ufafanuzi wa neno hili “Syncretism” katika kamusi ya Webster ni: njia ya kuchanganya mafunzo ya dini yanayotofautiana kwa njia isiyo sahihi.

Wahindu kwa mfano humchukua Yesu na kumuweka kwenye orodha ya baadhi ya miungu wao wengi. Litakuwa jambo bora kukumbuka hapa kwamba Mungu wake Eliya katika agano la kale alipokumbana na miungu wengi wa Baal, yeye aliwagonga na kuwaangusha, nyuso zao zikashika mchanga. Na jinsi hii, mungu yeyote anayetengenezwa na wanadamu lazima aanguke na kupiga magoti mbele ya Mungu wetu Yesu Kristo, kwa vile yeye ni Mungu Mwana, milele, mmoja na Baba na Roho Mtakatifu.

Ni Nini Kinachowagawanya Wanadamu?

Tunapoelewa kwamba Yesu Kristo ni Mungu, basi hatupati shida kuamini kwamba alizaliwa na mama bikira, miujiza na maajabu aliyoyafanya, kifo chake cha kuhuzunisha, kufufuka kwake na baadaye kwenda juu mbinguni na kuja kwake mara ya pili, nguvu na utukufu-haya yote yatakuwa ni mambo ambayo tunaweza kuyaelewa vyema.

Na kwa ajili Kristo ni Mungu, aliyeyumba dunia na vyote vilivyomo; na sheria za kimaumbile duniani, yeye yuko juu zaidi ya sheria zote kwa ajili ni yeye mwenyewe aliyeziweka. Naye alifanya hivyo kwa ajili ya sababu zake za upendo na hamu yake kutuokoa sisi wanadamu.

Kwa ajili ya Yesu Kristo Mnazareti, dunia imegawanyika. Vikundi viliko sio vile vya matajiri na masikini, wala si vikundi vya wanasiasa wenye nguvu na wanyonge. Huu si mgawanyiko unaotokana na watu kutofautiana kisiasa. Mgawanyiko ulioko ni wa kimsingi kabisa na ulianza wakati Mungu mwenyewe alipokuja duniani. Mgawanyiko huu ni tofauti na migawanyiko ya kawaida kati yetu sisi wanadamu.

Tunayosema hapa hayajaaongezewa chumvi kwani Kristo mwenyewe alisema hivi:

Kama Mungu angekuwa baba yenu, mngenipenda mimi; kwa maana nalitoka kwa Mungu, nami nimekuja; wala sikuja kwa nafsi yangu, bali yeye ndiye aliyenituma. Mbona hamfahamu hayo niyasemayo? Ni kwa sababu ninyi hamuwezi kulisikia neno langu. Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda.

Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo; wala hakisimama katika kweli, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu yeye ni mwongo, na baba wa huo (Yn. 8:42-44).

Je, ni ajabu kwamba jinsi vile kuna familia ya wale wanaoamini kwamba baba yao ni Mungu; pia kuna familia ya wale ambao hawana imani, nao baba yao ni mwovu shetani. Kila mtu si mtoto wa Mungu. Kuwa kati ya wale ambao baba yao ni Mungu, au wale baba yao shetani ni uchaguzi wako. Lazima uwe katika kikundi kimoja, na ni jukumu lako wewe mwenyewe kuchagua utapatikana wapi.

Unaweza ukawa na uhakika kwamba umechagua kuwa mtoto wa Mungu. Waweza pia kumchagua shetani na huku unaamini kwamba umefanya uchaguzi unaofaa. Kwa hivyo, sio sahihi kusema kwamba kila mmoja wetu yuko huru kuchagua njia gani atakayofuata mradi tu awe na imani kabisa njia hiyo ndio inayofaa. Uchaguzi wako waweza kuwa makosa. Mfano mzuri hapa ni sumu: unaweza ukala sumu ukidhani sumu hiyo ni kitu ambacho hakiwezi kukudhuru. Na ingawa una uhakika kwamba sumu haiwezi kukudhuru, lazima itakudhuru mradi tu uinywe.

Kwa kweli, wanadamu tuko katika vikundi viwili. Kila mmoja wetu yuko katika kikundi kimoja kati ya hivi viwili. Lazima uwe katika kikundi kimoja: cha Mungu au kile cha shetani. Ni jambo muhimu sana kujua uko katika kikundi gani. Ukiwa katika kikundi cha Mungu basi wewe ni mmoja wa familia ya

Ni Nini Kinachowagawanya Wanadamu?

Mungu. Na ukiwa katika familia ya Mungu, ni sharti ujue yote yeye Mungu amefanya kwa ajili yetu hasa lile tendo la ajabu la kumtuma mwanawe wa pekee Kristo aje hapa duniani na kufa kwa ajili ya dhambi zetu.

Jina hili Yesu lina maana “Yahweh mkombozi”. Na hapa Malaika akamwambia Yusufu: *nawe utamuita jina la Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao (Mt. 1:21).*

Hebu Fikiria

1. Je, ni nini unadhamini sana maishani? Na je, hili ambalo unaamini, lina uhusiano wowote na Mungu?
2. Je, nini hasa kinaleta migawanyiko kati ya watu? Ni siasa, uchumi, shida za kinyumbani au shida viwandani na kazini? Na je, migawanyiko hii inaweza kuwa inatokana kiroho na iwe ni ya milele?
3. Je, kati ya familia hizi mbili: Familia ya Mungu na familia ya shetani, wewe ungependa kuwa katika familia gani?



*Kwa undani kabisa, kwenye uovu, zaidi
ya yote wokovu kupitia Kumjua Mungu
wapatikana.*

*DAKTARI ARNOLD
(MWALIMU MKUU, RIGBY PUBLIC SCHOOL)*

Shida Yenyewe ni Ipi?

*M*wanzoni mwa karne ya ishirini, watu wengi walikuwa na imani ya kwamba mazuri yatatokea katika siku za usoni hapa duniani.

Wao waliamini kwamba tunakaribia enzi ya amani na utajiri. Wengi waliamini pia kwamba baraka za karne hii zingeonekana katika kila nchi duniani; hata katika nchi zile ambako kumekuwa na dhiki, magonjwa na umaskini wa kupita kifani. Ulipofika mwaka wa 1914, kingora kililia mwanzo wa vita vikuu kote ulaya.

Hata leo, ingawa kumekuwa na maendeleo makubwa katika sayansi na ufundi, watu bado hawana uhakika kwamba mambo yatageuka na kuwa mazuri kesho na siku zijazo. Badala ya kuwa na tumaini, wasiwasi imewazidi mamilioni ya watu. Wasiwasi inayotokana na kwamba silaha hatari kama zile za niuklia huenda zikaangamiza watu. Ugumu wa mambo katika ngazi za kimataifa umewafanya wengi wanaowaza kwa undani kufikia uamuzi kwamba tunaishi nyakati mbaya na za hatari katika historia yetu sisi wanadamu. Je, ni nini kimeharibu mambo?

Wakiwa katika hali ya kutaka kujibu swali hili, viongozi hukutana pamoja kwa ajili ya majadiliano. Wanapokutana na kilammoja kutoa maoni yake huku wenzake wakimskiliza kwa makini, dunia inazidi kukumbwa na mizozo. Na hata pesa kiasi gani kikitengwa kando kutafuta suluhisho, dunia inazidi kuyumbayumba na hakuna awezaye kubadili mwelekeo huu. Viongozi mashuhuri, wanasiasa hodari, wanasayansi wenye sifa, waalimu, wafanya biashara mashuhuri na wafanya kazi katika benki kubwa, madaktari na wengine wote wanachangia juhudi hizi, na bado jawabu halijapatikana.

Kutoka kwa hawa wote wenye ujuzi, ni wachache ambao wanagusia yale Mungu amesema kuwa ni chanzo cha shida hizi-na ni lazima chanzo hiki kijulikane vyema ndipo suluhisho litaweza kupatikana. Ni Mungu tu anayeweza kutusaidia kutambua shida yetu. Ni hapa tutaweza kutambua tofauti kati ya wale wanomtafuta Mungu, na wale ambao wana hamu ya kujua yale yasiyo ya maana kabisa katika dini na imani.

Mungu alisema: *natutengeneze mwanadamu kwa mfano wetu (Mwa. 1:26)*. Labda unajiuliza, mwanadamu aliumbwa kufanana na Mungu kwa njia gani? Ni wazi hatufanani na Mungu kimaumbile. Kristo alisema: *Mungu ni roho (Yn. 4:24)*. Mungu hana mikono, miguu, au macho kama sisi. Mungu anaishi katika mwanga ambao hauwezi kukaribiwa. *Hakuna mwanadamu ambaye amewahi kuukaribia, wala kuuona (1 Tim. 6:16)*. Mwanadamu ambaye

hawezi kuonekana na macho hajawahi kutokea duniani. Kwa hivyo lazima kuna kitu cha thamani sana katika wanadamu kuliko miili yetu hii. Na utu huu ndio huzidi kuishi hata wakati mwili hauna uhai. Ni utu huu unaoishi baada ya mwili kuishi ndiye aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu.

Biblia inasema Mungu ana uwezo wa kufikiri, yeye ana hisia, na pia ana hiari. Ni katika fani tatu hizi mwanadamu ameumbwa kwa mfano wake Mungu. Na kwa ajili yeye ni Mungu, uwezo wa ke hauna kiwango au kipimo sawa na ule wa wanadamu wa kawaida. Hayo ndiyo maumbile ya Mungu: kwamba uwezo wake hauna kipimo.

Uwezo wa mwanadamu una kipimo. Hata mwanasayansi maalum sana kutokea duniani kama Einstein, akili na uwezo wake una kipimo; kuna kiwango ambacho hawezi kuzidi. Hakuna mwanadamu ambaye anaweza kujua yote, wala kuwa na upendo usio na kipimo. Pia mwanadamu hana uwezo wa yote yaliyoko ulimwenguni. Yeye hana uwezo wa kuinga wala kuzuia matukio yanayohusu maisha yake. Hajui mwelekeo wake wa baadaye ni kwenda wapi.

Hata hivyo, mwanadamu ana uwezo wa kiroho unaomwezesha kumjua na kushiriki pamoja na Mungu katika mambo ya kiroho. Hii ndiyo sababu Biblia inasema mwanadamu ana *nafsi... na roho... na mwili...* (1 The. 5:23).

Kupitia roho yake, mwanadamu amepewa uwezo na Mungu wa kiroho wa kumwezesha kuwa na uhusiano wa karibu sana na muumba wake. Kupitia

mwili wake na utu wake, mwanadamu ana uhusiano fulani na ulimwengu anakoishi. Na hii ni ikiwa tutafuata utaratibu ambapo roho ndiye wa kwanza. Tukifuata utaratibu huu, basi yote yatakuwa sawa.

Kuna kitu ambacho kimeharibu na kina kasoro. Kutokana na kuharibika huku, utaratibu umebadilika. Mwili ndiyo nambari moja. Nambari mbili ni utu wetu (soul). Na mwisho ni roho. La kusikitisha ni kwamba katika ulimwengu wetu wa leo, mahitaji yetu ya kimwili, kimawazo na kimafikira ndio unazidi kuchukua msitari wa mbele katika mawazo yetu. Tunashugulikia mahitaji yetu ya kimwili kwa makini sana kuliko mengine yote. Mambo ya kiroho yamewekwa kando na hata kutoweka kabisa. Uwezo wetu wa kiroho umekufa kabisa! Kwa hivyo, badala ya Mungu kupewa nafasi ya kumsimamia mwanadamu aliyemuumba, yeye amepewa nafasi ya mwisho kabisa maishani. Na hata wakati fulani, Mungu huyu huwa ametupwa mbali kabisa hivi kwamba hakuna hata ushirikiano wowote kati yake na mwanadamu waliopotoka ambao ni viumbe alivyoumba.

Yeyote aliye mbali na Mungu ni mtu ambaye amekufa kiroho. Naye yule ambaye yuko karibu na Mungu, yuko hai kiroho.

*Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehemu, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; **hata wakati ule tulipokuwa wafu** kwa sababu ya makosa yetu; akituhisha pamoja na Kristo; yaani tumeokolewa kwa neema (Efe. 2:4,5).*

Shida Yenyewe ni Ipi?

Shida hapa duniani zilianzishwa na mwanadamu. Mungu hakuumba wanadamu ili wawe kama vibonzo ambavyo havina uwezo wa kujisimamia.

Kwa kutumia nyuzi tu, yule anayecheza vibonzo aweza kuvifanya vitende mambo fulani ya ajabu na kuchekesha. Mungu naye amewapa wanadamu uhuru wa kuchagua mienendo ambayo inatupendeza: tuko huru kujichagulia. Lakini tukiwa na uhuru huu, kama zawadi kutoka kwa Mungu, tuna jukumu ambalo lina uhusiano na jinsi vile tunachagua kutumia uhuru tuliopewa. Madaktari wengi wa magonjwa ya akili huwa hawatilii maanani wazo kama hili kwa sababu hawajali ukweli unaopatikana katika maandishi matakatifu.

Mkasa wa kwanza ulitokea kwa mwanadamu mara tu alipoumbwa kati ya miti ilyokuwa katika shamba la Edeni, kulikuwa na miti aina mbili ya muhimu kabisa. Moja ulikuwa *mti wa maisha*; wa pili ukawa *mti wa ujuzi wa mema na mabaya* (*Mwa. 2:9*). Adamu na Hawa waliambiwa na Mungu wangeweza kula matunda kutoka miti yote katika bustani la Edeni isipokuwa kutoka kwa mti ule wa ujuzi wa mema na mabaya. Kupitia ujumbe huu, Mungu alikuwa anawapa ujumbe unaohusu utiifu na kutotii. Mungu hapa aliwaonyesha wazi kwamba amewaumba kuwa viumbe vilivyo huru kuamua na kuchagua la kufanya. Ilikuwa ni juu yao kuamua kumtii au kutomtii. Uamuzi ulikuwa wao.

La kusikitisha ni kwamba Adamu na Hawa waliamua kuasi Mungu; uasi uliohusu wema na uovu.

Mungu alijua mapema kwamba hawa wawaili wataasi; na kwamba uasi huu utawaletea maafu na uchungu wanadamu wote watakaokuja baada ya Adamu na Hawa. Hata hivyo, na kwa ajili ya upendo wake kwa wanadamu aliowaumba, na huku akiwa anafahamu vyema kwamba utukufu utawajia wale watakaofanya uchaguzi ulio bora, Mungu amempa kila mwanadamu uhuru wa kujichagulia.

Shetani alitumia ujanja wake kuwashawishi Adamu na Hawa kuchagua kutomtii Mungu. Aliwahadaa akasema kwamba ikiwa wangekula tunda hili, wangepanyika kuwa kama Mungu. (Hata hivi leo shetani anawadangnya wanadamu kwamba wanaweza kuwa kama Mungu. Lakini jinsi tu Mungu ni Mungu na hawezi kuwa wa kiwango cha chini kuliko Mungu, vivyo hivyo mwanadamu ni mwanadamu na hawezi kuwa zaidi ya mwanadamu). Shetani aliwashawishi Adamu na Hawa nao wakatenda yale yaliokuwa mapenzi yao. Sio mapenzi ya Mungu. Na kwa ajili ya hayo, kila mwanadamu aliye uzao wa Adamu akakatwa kutoka ushirika na muumba wake. *Kwa hayo kama kwa kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo, mauti; na hayo mauti ikawafikia watu wote, kwa sababu wote wamefanya dhambi (Rum. 5:12).*

Sehemu za makaburi, kila hospitali, kila jeshi na jela; yote haya ni matokeo ya ule uchaguzi usiofaa ambao mwanadamu aliufanya pale mwanzo wakati wa kuumbwa kwake. Uasi huu ambao tunauita “dhambi” ni ugonjwa ambao kila moja wetu anazaliwa nao, na dhambi huwa imekata ushirikiano kati ya mwanadamu

na Mungu. Pia huleta migawanyiko kati yetu sisi wanadamu.

Hata hivyo mimi na wewe hatuna dhambi tu kwa ajili ya uzao wetu, dhambi zetu pia zinatokana na matendo yetu.

Tukiangalia kuzaliwa kwetu, mwandishi wa Zaburi anasema ukweli kabisa hivi: *tazama, mimi naliumbwa katika hali ya uovu: mama yangu alinichukua mimba hatiani (Zab. 51:5)*. Hata hivyo dhambi tuliyo nayo inayotokana na uzao wetu haituruhusu tuendelee katika uovu. Biblia pia inasema: *Dhambi zenu ambazo mlizitendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfwata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendae kazi katika wana wa kuasi; ambao zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwiili yetu watoto wa hasira kama na hao wengine (Efe. 2:2,3)*.

Ni kweli, tunakiri makosa yetu mbele ya Mungu kwa ajili ya kutokuwa watiifu. Hakuna anayeweza kulaumiwa: awe mke, ndugu, rafiki wa karibu ama hata mzazi. Wewe ndiye mwenye dhambi, sawa na vile dhambi yangu ni mzigo wangu.

Sababu kubwa inayoleta ugomvi na kutoelewana kati ya watu ni dhambi. Dhambi inamfunga asiye amini pamoja na yule aliye na imani, awe Mwarabu au Myahudi, Mhindi au Mwafrika.

Dhambi ina wafunga pamoja wale waishio katika nchi zisizoendelea na wale waishio katika mataifa yaliyostawi yene viwanda. Dhambi inamfunga

mkomunisti pamoja na yule mwenye kiburi na maringo; pia inamfunga askari pamoja na mwenye kutenda makosa. Mwenye kutetea haki za wamama na yule wa kutetea haki za wanaume. Hata mtu awe kahaba ama mhubiri; awe tajiri au maskini, aliye na elimu au ambaye hajui kusoma wala kuandika, *wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu (Rum. 3:23).*

Hata hivyo, Kristo ndiye atakayemwoko mwenye dhambi. Alisema hivi: *lakini nendeni mkajifunze maana ya maneno haya, nataka rehema, wala si sadaka; kwa maana sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi (Mt. 9:13).* Labda kwa kiwango kidogo au kikubwa, ukweli ni kwamba tumekosa kupata utukufu wa Mungu. Neno hili dhambi, maana yake ni kwamba tumekosa kufikia kipimo. Sisi wenyewe hatuna la kufanya kusahihisha makosa haya. Ni kupoteza wakati kufikiri kwamba tunaweza kupata amani kupitia kuwa wazuri ama kutenda yale tunayoyachukua kuwa mazuri. *Wala si kwa matendo, mtu awe yote asije akajisifu (Efe. 2:9).* Na hii ndiyo sababu alipokuwa akizungumzia wokovu, Kristo alisema hivi: *nataka rehema, wala si sadaka kwa maana sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi (Mt. 9:13).*

Kuelewa vyema msamaha wake Mungu huleta hali ya utulivu kwao wale ambao wamezidiwa na dhambi zao.

Na hii ni kwa sababu Mungu ni *mwingi wa rehema (Efe. 2:4).* Kile anacho hitaji kutoka kwako ni upokee

Shida Yenyewe ni Ipi?

wokovu kama zawadi ya bure kutoka kwake. *Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu (Efe. 2:8).*

Mungu wa rehema sasa hivi ametoa uzima wa milele kupitia mwanawe Yesu Kristo. Na kwa ajili amekufungulia njia, yeye hatakulazimisha kupokea maisha haya ya milele. Jinsi vile utapokea wito huu wake Mungu ni jambo linalohitaji uamuzi wa haraka. Mungu anasema hivi: *wakati uliokubalika nalikusikia, siku ya wokovu nalikusaidia; tazama, wakati uliyo kubalika ndio sasa (2 Kor. 6:2).*

Huu ndio wakati wa kuamua, sio baadaye, au baada ya kujaribu kurekebisha maisha kwa kutumia nguvu zako mwenyewe. Kumbuka Kristo alisema hivi: *sikuja kuwaita wenye haki mbali wenye dhambi (Mt. 9:13).*

Kwa kweli, ukielewa kwamba shida yako ni dhambi, hii ndiyo hatua yako ya kwanza kuelekea suluhisho sahihi. Mikono yake Kristo iko wazi tayari kukupokea leo hii. Haijalishi ni wapi ulipo au hali yako. Yale anayotaka kusikia kutoka kwako ni haya: *Ee Mungu uniwie radhi mimi mwenye dhambi (Lk. 18:13).*

Kiu Cha Kumtafuta Mungu



Barua kutoka kwa Gereza kuu litwalo "C"

Barua ifuatayo ilitumuwa ketu kutoka kwa mfungwa katika jela kuu nchini Afrika Kusini. Maandishi yake huyu mfungwa yanakaririwa hapa jinsi yalivyo katika barua yake.

“Kitabu hiki Kiu Cha Kumtafuta Mungu kimenisaidia kuelewa vyema neno la Mungu. Kile namaanisha hapa ni kwamba kitabu hiki kimetusaidia kupata njia halisi na ya ukweli ya kufuata maishani. Naamini ewew unayesoma barua hii unaelewa yale ninayosema pale ninaposema kwamba kitabu hiki kimenisaidia kugubdua njia sawa ya kufuata maishani. Rfaiki yangu ndiye aliyenipa kitabu hiki... naamini Mungu ndiye aliyeyumba vyote vilivyoko duniani... Naamini pia Mungu ataendelea kunisaidia wakati huu nikiwa katika jela...”

– Barua hii ilitumwa namfungwa huyu Trans World Radio

Shida Yenyewe ni Ipi?

Hebu Fikiria

1. Je, umepata kuona kwamba kuna jambo lililoiondea mrama sana jamii ya walimwengu?
2. Unapokuwa unaugua, je, ni jambo la muhimu kwamba daktari aweze kukuchunguza na kugundua ni maradhi gani yanakusumbua kabla hajakupa dawa?
3. Je, Biblia inatambua shida yako? Na imetaja jinsi ya kutatua shida hiyo?

Palitokea mtu mmoja, Msamaria, jina lake Simoni; awali yeye alikuwa mchawi katika mji huo, aliyefanya mengi ya ajabu. Yeye alijifanya kuwa mtu asiye wa kawaida, na pia mkuu zaidi ya wote. Nao wote: wakubwa na wadogo walimtilia maanani wakisema, huyu mtu ndiye aliye na uwezo kutoka kwa Mungu.

DR LUKE

Mbona Watu Wamekubali Kudanganywa?

*W*akati wa ujana wangu, niliishi katika sehemu ya uingereza ambapo ndege za kivita zilipaa kila mara. Ulikuwa wakati wa vita na ndege hizi zilikuwa ziko safarini kuelekea katika sehemu ya kati nchini na kaskazini. Marafiki zangu walikuja kujifunza jinsi ya kutambua mlio wa ndege ya kivita kutokana na jinsi vile ndege zetu za kijeshi zilikuwa. Tulipoiona taa ya kuangaza ndege ya adui ikielekeza mwangaza wa ke hewani, tulishikwa na furaha kwa ajili ni wakati huo tungesikia mlio wa bunduki aina ya “Ack-Ack” ama makabiliano yanayoitwa “dogfight”. Wakati fulani, ndege ya kivita ilikuwa inaangushwa.

Na pale ndege inapoanguka, kulikuwa na uwezekano kwamba baadhi ya wana anga wangeruka na miavuli. Ili kuwafanya wana anga hawa wasiweze kupata njia ya kutoroka; na baadaye hata warudi na

ndege iliyo na mabomu, wakuu wetu walitoa vibao vyenye majina ya bara bara hasa katika sehemu za makutano. Kwa hivyo, hakukuweco na kibao cha kuelekeza msafiri popote barabarani.

Hata hivyo, sisi vijana tulijuwa kwamba inje ya mji wetu katika msitu wa Wootten, kulikuwa na kibao kwenye sehemu moja ya barabara muhimu kabisa ambacho kilikuwa hakijaondolewa. ulipobadili kule kibao hiki kilikuwa kinaelekea, sisi tulijiona kuwa watoto ambao tunasaidia katika kupigana vita. Sawa na maafisa wa utawala, sisi tulikuwa tuna jaribu kumpoteza mgeni yeyote kwenye ufuo wa bahari kwetu nyumbani.

Hata hivyo, kama mgeni huyu asiyetakikana angekuwa na ramani, basi hayo yote ambayo tulikuwa tukiyafanya hayangefaa. Yeye hangepotea njia hata kama kibao kimelekezwa sehemu isiyo sawa; yeye anaweza tu kupotea njia ikiwa hatatumia ramani aliyo nayo.

Mungu anataeleza juu ya watu ambao katika kumtafuta, watapotezwa njia na vibao vilivyo na makosa.

Mwanzo kabisa, yeyote ambaye hatatilia maanani kwamba yote ya ajabu ambayo yako ulimwenguni yatuelekeza kwake Mungu muumba wa vyote bila shaka atapotea.

Wakijinenea kuwa wenye hekima walipumbazika (Rum. 1:22). Na kama walivyokataa kuwa na Mungu katika fahamu zao, Mungu aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa, wafanye yasiyowapasa (Rum. 1:28).

Mbona Watu Wamekubali Kudanganywa?

Akili hiyo iliyopotoka inachukua viumbe vilivyoubwa kuwa Mungu badala ya yule ambaye ni muumba wa vyote. Mtu ambaye ana mawazo yaliyo sawa naye ataelekeza maombi yake kwa yule aliye muumba. Kwa hivyo, ukikataa kuamini kwamba Mungu ndiye aliyeumba dunia na anga, Mungu naye atakuwacha uchukuliwe na mawazo yaliyopotoka, na kukuacha pia uamini mawazo ya ajabu kuhusu jinsi vile dunia na anga vilivyoubwa. Akili iliyopotoka huwa na mawazo yaliyopotoka pia.

Mungu pia anaonya, watu ambao wanakataa kulikubali neno la Mungu kuwa ni kweli, watafuata barabara ya uovu, nayo itawaongoza kwenda kuangamia. Kwa kweli yeyote ambaye hatachagua kufuata na kupenda ukweli wa neno la Mungu anajiweka katika hali ya hatari sana.

Na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile ukweli, wapate kuokolewa. Kwa hivyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu (2 The. 2:10,11).

Mtu anapo ukataa au kutupilia mbali ukweli, yeye basi huiingia katika yale yaliyo potovu.

Nakumbuka siku moja nilipojaribu kutafuta njia ya kuelekea nyumbani katika ukungu mkuu katika mjini London. Ili nifike kando ya barabara, nilihitaji msaada mkubwa kutoka karibu kila upande. Hata mwanga kutoka tochi yangu haukuweza kuonekana umbali wa urefu wa mkono wangu. Mungu anawambia kwamba upotovu wa kimawazo mkuu ni sawa na ukungu ulioko kwenye bongo zetu; nao utaendelea katika ulimwengu

huu watu watazidi kukataa ukweli wa neno la Mungu. Wanafunzi wake Yesu walimuuliza: Nini itakuwa ishara ya kuja kwako mara ya pili, na mwisho ya haya yote? Kati ya majibu yake, alisema haya:

Kwa maana watatoke a makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza kama yamkini, hata walio wateule (Mt. 24:24).

Hata hivi sasa huenda unasema hivi: “Mimi sijadanganywa.” Labda hata unaweza kujivuna kwamba una uwezo wa kumjua kristo wa uongo ama nabii wa uongo. Lakini hebu subiri kidogo, na fikiria kwa makini kuhusu wazo hili. Ikiwa kwa ajili hupendi ukweli na Mungu amemkubalia shetani akuhadae, hutaweza kujua ukweli.

Kama kweli ungejua huyo ni nabii wa uongo, basi bila shaka hungedanganywa. Uwongo wote lazima uko katika mawazo yako, na yeyote anaye jiona kuwa mwerevu atapata ugumu sana kukubali kwamba amedanganywa.

Kuna watu aina mbili ambao hukataa ukweli wanaposoma Bibilia, na hapo kufungua njia ili wakadanganywe na dunia.

Mmoja ni yule mwerevu na mwenye maringo anayejiona kwamba anajiweza. Wa pili ni yule ambaye si mtiifu. Lakini kwa yule ambaye ana hamu kamili ya kufanya yale Mungu anamtaka afanye, Kristo anasema hivi: *mtu akitaka kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo, kwamba yatoka kwa*

Mungu, au kwamba mimi nanena kwa nafsi yangu ta (Yn. 7:17).

Ikiwa kweli una hamu ya kutenda mapenzi yake Mungu, yakupasa ufahamu kwamba kupitia Bibilia Mungu atakufunza ni nini unafaa kuamini. Pia atakufunza jinsi yakuhusiana na wale walio karibu.

Hata hivyo ni lazima tuwe chonjo na tuyatupilie mbali mafunzo ya wale waalimu ambao wamejibandika mamlaka ya kutoa mafunzo ya kidini; ambao hawafunzi neno halisi la Mungu, na badala yake wanafunza yale ambayo ni makosa.

Katika enzi hii tuishimo, wako maajenti wa shetani ambao wanawaongoza watu katika njia mbaya, nao ni wanachama wa vikundi ambavyo sio vya Kikristo halisi. Yeyote ambaye amekataa kukubali ukweli kwamba Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu, utatu katika moja na moja katika utatu, yeye ni nabii wa uongo. Na ingawa watu kama hawa huweza kutaja kurasa fulani kutoka Bibilia, wao hutumia maandishi hayo kwa njia isiyo sawa, na hapo kuendeleza dini ambayo si ya kibibilia. Unaweza kumjua mwalimu wa uongo kupitia swali moja tu: je, Yesu Kristo ni nani?

Na hiyo ndio sababu ni jambo la muhimu sana kujua Kristo ni nani.

Pale unapojua kwamba yesu ni Mungu mwana, hata mashirika ya kisiri ambayo yana urafiki wa kindugu, urafiki uliyo wa karibu sana kati ya wanachama yatajitokeza wazi kwako kuwa ni mashirika yaliyopotoka kiroho.* (*Maelezo zaidi soma ukurasa wa 76*)

Na hata ingawa Mungu hutajwa katika baadhi ya mashirika haya, wao hudharau mafunzo yake Kristo ambaye alisema *Mtu haji kwa Baba, ila kwa njia yangu mimi (Yn. 14:6)*. Bibilia ina maandiko yenye ukali kuhusu wale ambao wamekubali imani mbaya kumhusu Mungu. *Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda wema: Mashetani nao waamini na kutetemeka (Yak. 2:19)*.

Maandiko matakatifu yana maneno makali sana kuhusu wale ambao wana mawazo yaliyopotoka

* Freemasonry ni shirika kubwa sana la kimataifa ambalo la jigamba kwamba wakati huu lina wanachama karibu milioni 10. Kupitia msingi wake wa kueneza undugu, kusaidiana, na ukweli, shirika hili huwavutia wengi. Yule ambaye si mwanachama anaweza akafikiria kwamba hakuna hatari iliooko kuwa mwanachama wa shirika hili. Kabla ya kukubaliwa kuwa mwanachama, kila mmoja wa wanachama lazima akiri kwamba yeye yuko katika giza na anatafuta mwanga. Mfuasi wa Kristo anaamini kwamba amepata mwanga. Kristo alisema hivi: *Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima (Yn. 8:12)*. Shehe ya kukubaliwa katika shirika hili huwa ya kustajaabisha nayo inahusu mambo mengi ambayo maana yake si wazi. Na hapa yule ambaye anataka kuwa mwanachama huelekezwa mbali na Mungu wetu aliye katika Bibilia pale anapojulishwa kwake “Gauto”. Mgeni katika shirika hili huambiwa kwamba Gauto ni jina lililopotea la Mungu; na kwamba “Gauto” ndiye aliyepanga jinsi vile ulimwengu ulivyoumbwa. Kimsingi basi, mtu yeyote aliye na imani, awe ni mtu wa dini ya Kibudha, Hindu, Muislamu, Myahudi ama hata Mkristo anaweza kujiunga na kikundi hiki cha wa Freemason. Kwa hivyo huyu “Gauto” ambaye sasa ni kama mungu anayatoa mawazo yake mwanachama huyu mgeni kutoka kwake Kristo ambaye Bibilia inasema ni Mwanga (Yn. 1:9) na mwishowe, pale mwanachama huyu anapo panda ngazi na kuwa “master mason,” yeye hufunzwa kuwa jina lingine la Mungu ni “Jahbuloni”. Ukweli ni kwamba, jina hili ni mchanganyiko wa majina ya Mungu ya Kiyahudi na majina mbali mbali ya Mungu kutoka mashariki ya mbali. Jina hili linatokana na lile JAH ambalo ni sawa na YAHWEH, na BUL ambalo ni kama BAAL na ON ambalo ni jina la mungu la wa Wamisri wa jua. Huu ni mfano mkuu wa jinsi vile mawazo kutoka dini mbali mbali huchanganywa. Kristo mwenyewe alisema hivi: *lakini jicho lako likiwa bovu, mwili wako wote utakuwa na giza. Basi ili nuru iliyomo ndani y a ko ikiwa giza; si giza hilo! (Mt. 6:23)*.

kuhusu Mungu. Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; *watenda wema: Mashetani nao waamini na kutetemeka (Yak. 2:19).*

Leo hii, tunashuhudia ongezeko kubwa la shuguli za mashirika na dini ambazo haziamini Mungu wa Bibilia. Dini zenye misingi yake katika imani ya kihindi zimejitokeza na kuvutia wafuasi wengi. Katika mataifa mengi ambayo hapo awali yalijulikana kwa ajili ya misingi yao ya Kikristo, siku hizi madhehebu haya ya Kihindu yamejitokeza kupitia mafunzo kama yale ya Transcendental Meditation ama Yoga. Vikundi vidogo vidogo vimechipuka kutoka kwa kikundi kikubwa hiki cha Wahindu, nao wanawaabudu miungu wengi ambao wameumbwa badala ya kumwabudu Mungu aliyewaumba. La kuvunja moyo ni kwamba akili nyingi ambazo zimepotea njia humchukua “Guru” kuwa ni mtu wa muhimu kuliko Mungu aliyewaumba vyote, na ambaye alijishusha heshima yake ili kuja hapa duniani.

Waislamu nao wamejitokeza na nguvu sana katika kueneza imani yao. Kwa ajili ya utajiri wao unaotokana na mafuta, na uwezo wao wa kisiasa, wameweza kufanya yale ambayo yalionekana kuwa ni mambo hawawezi miaka chache tu iliyopita. Kutoka pale sehemu ya utukufu iitwayo The DOME OF THE ROCK ambayo iko kwenye hekalu mlimani Yerusalemu ambapo ni mahali maalum pa maombi, wao wanapinga habari njema ambayo ni maandishi kutoka kwake Mungu mwenyewe. Kwenye mwamba huu kuna maandishi haya:

Na jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, ndipo akamtoa mwanawe wa pekee ili yeyeyote amwaminie asipotee ili awe na uzima wa milele (Yn. 3:16).

Na hali hii ya kupotea kiroho haijatokezea tu katika mambo ya imani. Dunia ya sasa imekubali filofosia ya kiutu (Humanism) ambayo kiini chake ni kwamba mwanadamu ndiye kiumbe cha maana na mwanzo ya vyote ulimwenguni. Filofosia hii imengia hata katika vyo vikiu, magazetini, katika makongomano makubwa, redio na hata kwenye runinga. “Jipende na ujiendeleze,” hilo ndilo wazo kuu katika matangazo ya biashara siku hizi.

Filofosia hii ambayo yenyewe inahimiza kumwabudu mwanadamu kama Mungu sio filofosia mpya kamwe. Wakati wa mtume Paulo, Mungu alisema hivi: *Kwa maana walibadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakakisujudia kiumbe na kukiabudu badala ya muumba anayehimidiwa milele. Amina (Rum. 1:25).* Mungu anauliza swali ambalo ni la muhimu sana kwa wale wenye kuendeleza filofosia hii: *Ulikuwa wapi nilipoitweka msingi ya nchi? (Ayu. 38:4).* Hadithi hii ni ya zamani: wakati shetani alimjia Hawa, yeye alifanya kile ambacho kilikuwa kinaonekana hakiwezekani kuwa kitu kinachowezekana kwa kusema: *utakuwa kama Mungu (Mwa. 3:5).* Katika siku hizi, shetani anazidi kuendeleza kazi yake mbaya kupitia mafunzo yenye uovu kama haya yaliyo katika filofosia hii.

Labda wewe ni kijana chipukizi, na bado hujanaswa na mafunzo ya “kisasa” ama yale ya

kisiasa na hata kidini. Kwako wewe siasa ni kitu cha kushuku, nayo dini ni kitu ambacho si cha maana. Wewe unapenda kuungana na wenzako na kutafuta yale ya kukutosheleza kwingineko. Labda unafikiria kwamba mitindo ya kisasa ya muziki kama vile “Punk Rock,” ama “New wave,” ama “heavy metal,” na kadhalika itakuwezesha kuhepa katika dunia hii ya upweke inayokuzingira.

Bila shaka unaelewa maneno yaliyo kwenye muziki unaofurahia na kuucheza. Na labda hutaki kukubali, lakini lililo wazi ni kwamba muziki huu una mengi ya kishetani. Pia muziki huu hukuletea uchungu na huwa chanzo cha usherati. Wakati fulani hata yale ya kutisha ambayo yanapatikana jehnamu huwa yanawekwa katika muziki huu; na kuelekezwa kuwa ni njia moja ya kukwepa maisha ya siku hizi ambayo hayana maana. Katika mazingira haya ya mchanganyiko wa uovu na hata vita, vijana wengi huungana pamoja na kutiwa moyo kujiua wenyewe na wenzao.

Hebu nikusimulie kisa kimoja kutoka mji wa Los Angeles. Kwenyewe ni katika nyumba ya kuweka maiti iitwayo “The Refrigerator”. Pale kuna miili 600, na wengi wa maiti hizi ni za vijana. Nayo miili hii huwekwa hapa kwa muda wa miezi tatu ikitarajiwa kwamba mtu atajitokeza kuwatambua. Vitambulisho vyenye maandishi yasiyojulikana hufungwa kwenye vidole vya miguu. Idadi kubwa ya hawa ambao husemekana kwamba hawajulikani huzikwa kwenye makaburi ya wale maskini kabisa. Wengi wao huwa watu wanaotumia madawa ya kulevya, na wao huwa wamejiingiza katika matumizi haya baada ya kuskiliza

ujumbe kuhusu madawa haya katika majumba ya dansi na katika nyimbo kwenye vyombo matamshi yake Kristo aliyesema: *mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele (Yn. 10:10).*

Na sasa kuongeza katika uovu huu wote watu wengi wameanza kurudia mtindo ule wa zamani wa kuwa na imani katika sayari na mambo ya uchawi yanayohusu nyota na kadhalika. Haya yote yanafanyika enzi hii ambapo tumekuwa na maendeleo makubwa sana duniani.

Katika sehemu nyingi ambapo huwezi kuamini, kuna idadi kubwa sana ya watu wanaomuabudu shetani. Wataalamu na wafanyi kazi wa ngazi za juu mjini London hukutana Kensington kwa ajili ya ibada ya giza (Black mass). Sehemu maalum za wachawi zimejitokeza ulaya, na hata katika maeneo yanayoheshimika kama kisiwa cha Vancouver. Ibaada za kuabudu waliokufa kutoka barani Afrika zimetawanyika kila mahali duniani. Michezo ya kishetani kama vile “Parlour games,” na “Dragons” na pia “Ouija Board” inazidi kuwavutia wengi ambao wanahamu ya kujua mambo ya kishetani. Haya yote yanatokana na hamu ya watu kuelewa mengi ya kiroho. Kwa ajili ya hamu ya kumjua Mungu, wengi **wametoka** kwenye mwanga wake Mungu na **kujielekeza** katika giza nene la uchawi, na kujishibisha kiroho kwa njia isiyofaa. Haya yote yanaendelea ulimwengu huu ambao twachukua kuwa ulimwengu uliopiga hatua mbele kimaendeleo.

Ni jambo zuri kukumbuka hapa yale Mungu amesema kuhusu siku za mwisho. Ametuonya

Mbona Watu Wamekubali Kudanganywa?

kuhusu manabii wa uongo; pia ametoa onyo kuhusu ishara na maajabu yatakayotokea kuwahadaa watu siku za mwisho. Kwa kweli Mungu ametwambia kutatokea mtaalamu wa uwongo ambaye matendo yake ni ya uovu. Yule ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake shetani, kwa uwezo wote ni ishara na ajabu za uongo; na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa (*2The. 2:9,10*).

Kwa ajili ya hamu inayozidi kunawiri katika watu: hamu ya kupokea mafunzo ya uwongo, na vitendo vya uovu, si jambo gumu kuelewa ni kwa nini mataifa mengi na vikundi vya watu wamefunikwa na nguvu za kunyanyasa za kutokubali ukweli, na hali yakujisikia hawajiwezi. Vibao vyake shetani ni vingi mno. Lile lililo wazi ni kwamba hakuna hata kibao kimoja ambacho chaweza kumuelekeza mtu kwake Yesu Kristo.

Ujumbe wake Mungu, sio ujumbe wa kuhuzunisha, kuchanganya mawazo wala kuleta kifo. Ujumbe wake ni wa kutia moyo na unahusu maisha ya furaha yanayopatikana katika Kristo. Ili kumjua Mungu, Roho Mtakatifu atakuongoza nakukuelekeza kwake Kristo ambaye alisema hivi: *Mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi (Yn. 14:6)*.

Mungu amekuonya kuhusu ilani hizi za uongo ili usije ukapotea. Pia amekuonya juu ya uwongo unaoenea sasa hivi kuchafua mawazo yako. Na sasa anakupa ahadi hii:

Kiu Cha Kumtafuta Mungu

Maana nayajua mawazo ninayowazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si mabaya, kuwapa nyinyi tumaini siku zenu za mwisho. Nanyi mtaniita, mtakwenda na kuniomba, nami nitawasikiliza. Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote. Nami nitaonekana kwenu, Asema Bwana, nami nitawarudisha watu wenu waliofungwa, nami nitawakusanya ninyi, nikiwatoa katika mataifa yote, na katika mahali pote, nilipo wafukuza asema Bwana; nami nitawaleta tena, hata mahali ambapo kutoka hapo naliwafanya mchukuliwe mateka (Yer. 29:11-14).

Mbona Watu Wamekubali Kudanganywa?

Hebu Fikiria

1. Ni mawazo ya aina gani yataabudu viumbe badala ya yule aliyeviumba? (*Soma Rum. 1:22-28*)
2. Katika kumtafuta Mungu, ni kifunguo cha aina gani kitafungua mlango wa ufahamu wako unaokuletea shida kuelewa mambo ya Mungu? (*Soma Yn. 7:17*)

Je, nimawazo yako au la?

Ama hamu na mwelekeo wako?
3. Je Mungu amekupa ilani inayoeleweka vyema kukuongoza kwake? (*Soma Yn. 8:12*)

*Miaka mingi iliyopita kijana mmoja
katika shule ya jumapili Uingereza
alimuuliza mwalimu wake wa somo la
jumapili hivi: “Je, Mungu anawapenda
watoto watukutu?” Naye mwalimu
akajibu: “La hawapendi”
Oh! Kosa kuu kumwambia mtoto huyu
haya yaliyo sawa na kukufuru. Kama
Mungu hangewapenda watoto watukutu,
hangenipenda mimi pia. Shakespeare
anasema hivi:” mapenzi sio mapenzi
halisi pale yanapobadilika kwa ajili
yametakikana kubadilika.*

G. CAMPBELL MORGAN

Je, Kweli Mungu Ananipenda?

*J*e, umewahi kuwa na tashwishi kuhusu upendo wa yule mtu unayemthamini sana? Na je, umewahi kujaribu kumuonyesha mtu unayemthamini kwamba unampenda, naye haamini kwamba kwa kweli unampenda? Kwa kweli, kama umewahi kufanya haya, basi sina shaka unajua kuna wakati ambapo upendo hufaa kuonyeshwa kupitia matendo kuliko kupitia maneneo matupu.

Na kwa vile matendo ni ya muhimu sana kuliko maneno matupu; Mungu alionyesha upendo wake kwetu sisi wanadamu kupitia kifo cha Kristo pale msalabani. Ukielewa haya basi hakuna haja ya maelezo kwa vile kisa hiki ndicho kielelezo kamili kinachohusu jinsi vile Mungu anakupenda.

Mara tu baada ya kupokea wokovu, nilisoma habari iliyowahusu vijana wawili, mmoja aliyekuwa mchezaji wa tarumbeta hodari na mwingine aliyekuwa askari. Wakati wa kisa hiki, wao walikuwa wanapigana katika vita vikuu vya makaburu Afrika kusini. Kijana yule jina lake lilikuwa Willie Holt, na umri

wake ulikuwa miaka 12. Kijana huyu alipewa kazi katika hema la askari 12 ambao walikuwa bado hawajampokea Kristo kama Bwana na mwokozi. Mmoja wa askari hawa aliitwa Bill. Tofauti kuu kati ya Bill na Holt ilikuwa yeye Holt alikuwa amemkubali Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wa maisha yake. Kila jioni, kijana Holt alipiga magoti kando ya kitanda chake na kuomba kwa unyenyekevu. Pia yeye alisoma Bibila yake. Na wakati wa kufanya hayo, askari wenzake walimfanyia mzaha na dhihaka.

Siku moja afisaa mkuu aliyekuwa na cheo cha Kanali aliwaita wote ili wakaguliwe. Mwizi alikuwa amepatikana katika hema makao yao Bill na Holt. Hii haikuwa mara ya kwanza mwizi huyu kutenda uovu huo. Akiwa mwenye hamu ya kumpata mwizi huyo, Kanali msimamizi alitoa amri hii: onyo langu la hapo awali halijatiliwa maananai. Jana usiku mwizi huyu ameiba tena! Leo hii nataka mwizi huyu ajitokeze, na ajitoe kulipia uovu wake kama mwanaume. Kama mwizi huyu hajitokezi, basi kila moja katika kikundi hiki atalipia uovu huu. Atapokea viboko kumi kwenye kitako chake. Kama mwizi huyu atajitokeza, basi ninyi wenzake mtapona.”

Willie alisonga mbele na kuuliza: “Umesema kama mmoja wetu atajitoe ili alipie uovu huu kwa kukubali kuadhibiwa, wengine watapona?” Akaendelea: “Mimi najitoe kuwa mwanamume huyo”.

Akiwa na hasira, yule Kanali alimkemea mwizi huyo ambaye alikuwa amekataa kujitokeza. “Unawezaje kumuacha huyu kijana asiye na makosa aadhibiwe kwa ajili ya makosa yako?”

Hakuna yeyote aliyesikika kujitokeza. Akaendelea: “Sasa mtatazama kijana huyu akiadhibiwa kwa ajili ya makosa ya mwenzake.”

Sawa na agizo la Kanali huyu aliamuru kwamba kitako chake Willie kiwekwe wazi, akaanza kuchapwa viboko. Na pale Willie alipokuwa anaanza kuzidiwa na uchungu wa viboko Bill alijitokeza na kusema: “Acheni! Mimi ndiye mwizi huyo. Nakubali kuadhibiwa.”

Hapo Willie akaamka kutoka hali ile ya kuzirai kwa ajili ya viboko, na kusema kwa sauti ya chini, “Achana na hayo, Kanali hatakubali kusimamisha kutolewa huku kwa adhabu. Niche niendeleo kuadhibiwa kwa ajili yako.”

La ajabu ni kwamba, kijana huyu aliendeleo kuadhibiwa kwa ajili ya mwenzake Bill.

Willie hakuweza kupona kutokana na majeraha aliyoyapata wakati wa kuadhibiwa. Lakini kabla ya kuaga dunia, na bila shaka kwenda mbinguni, Bill alitokwa na machozi kando ya kitanda chake huku akisema: “Mbona awe wewe Willie, mbona wewe? Mbona ukafanya haya kwa ajili yangu, sistahili wema huu!”

Naye Willie akamjibu: “Bill, nimejaribu kukueleza jinsi vile Mungu anakupenda, nawe umekuwa ukiyachukua kuwa ni mzaha. Niliona ikiwa nitakubali kuadhibiwa kwa ajili yako, hii itakusaidia ili uweze kujua ni jinsi gani Mungu anakupenda pale alipokufa msalabani kwa ajili ya dhambi zako.”

Kabla ya Willie kuaga dunia na bila shaka kwenda mbinguni, Bill alimkubali Kristo kuwa Mwokozi wa

maisha yake. Nao wokovu huu unaopatikana bila gharama kutoka kwake Kristo.

Kupitia Kristo, mbingu zilitimiza mpango wa kumuokoa mwanadamu aliyepotea, ni kwa ajili ya upendo, upendo kwetu sisi wanadamu ndio uliomfanya Kristo akubali kuteswa na kusulubiwa msalabani.

Mwanadamu asiye na kosa

Misalaba tatu ilitundikwa milimani Golgotha. Katika misalaba miwili, wezi walisulubiwa. Kati ya hawa wezi wawili alikuwa Kristo ambaye alichomwa misumari kwenye mikono, na hapo akafa. Wakati wa maumivu haya makali, mmoja wa wezi hawa alijito keza kutoa maoni yake kuhusu kazi ya mahakama iliy-owahukumu kifo. Lirilomhusu hivi sasa ni jinsi vile mahakama hii ya kirumi ilivyokosa pale ilipo mhukumu Kristo. Sawa na wezi wawili. Yeye alitambua kwamba haki zake Mwokozi wetu zilikuwa zimekiukwa. Kwa moyo wa upole, na kwa njia inayoeleweka vyema, mwizi huyu alitoa maombi aina tatu dakika zake za mwisho. Huu ndio utaratibu wa maombi haya.

Kwanza: *Tunapokea kile tunachostahili kupokea kwa ajili ya matendo yetu.* Katika matamshi haya mafupi na ya unyenyekevu, mwizi huyu alisema wazi kwamba alistahili kuhukumiwa na kuteseka. Kwa ajili ya makosa yake. Yeye alikiri makosa yake.

Pili: *Na tunakufa kwa haki...* Katika enzi hii ambapo wizi mdogo na ule wa mabavu umezidi kuenea, ni vigumu kuelewa kwamba hapo zamani

makosa kama haya yalikuwa yakichukuliwa na uzito mkubwa. Hata hivyo, katika matamshi yake haya mafupi, mwizi huyu alipokuwa anaaga dunia alieleza jinsi vile alikuwa na imani kwamba hukumu yake ya kifo ilikuwa sawa na ya haki, na alistahili kuhukumiwa hivi.

Tatu: *Mtu huyu hajafanya kosa lolote.* Ingawa ni jambo la ajabu kusoma kwamba mwizi huyu alikiri makosa yake, na kwamba alikubali hukumu iliyotolewa, na jinsi vile mahakama hii ilivyoendesha mambo yake; ni jambo la ajabu kusoma kwamba yeye alionea Kristo huruma. Kristo ambaye alikuwa pale msalabani karibu kufa kifo bila kosa, na haikuwa haki yeye kusulubiwa.

Na akiwa tayari amehukumiwa kwa ajili ya makosa yake, akiwa pale msalabani, mwizi yule hakuwa na la kufanya, ila kuwa na ombi kwake Kristo: *Yesu nikumbuke utakapofika ufalme wa mbinguni.* Sawa na jinsi vile yeye huwajibu wenye kukiri makosa yao Yesu alimjibu hivi: *Leo hii utakuwa pamoja nami peponi (Lk. 23:39-43).*

Siku hiyo, mwizi huyu ambaye alikuwa anakaribia kufa, sawa na wote wanaokiri makosa yao na kuja kwake Mungu, yeye alipewa hakikisho la maisha ya milele. Yeye alikuwa amekuja kwake yule aliye na uwezo wa kumuokoa. Aliomba msamaha msalabani ambapo Kristo alikufa.

Siku hii mbele ya wezi waliokuwa wanakaribia kifo, Yesu alikuwa bila kosa. Na baadaye wafuasi wake wawili walieleza wazi haya yote. Wao walishuhudia kwamba Yesu hakuwa na kosa. Kila mmoja wa

wafuasi hawa pamoja na mtume Paulo waliandika kuhusu jinsi vile Kristo hakuwa na kosa lolote. Hebu tuangalie kwa undani yale walio yasema kuhusu mwokozi wetu.

PETRO: Alikuwa ni rafiki mkubwa wa Yesu. Alijulikana kuwa mtu wa haraka, na wa kufanya mambo fulani bila kufikiria. Alipokuwa anaeleza jinsi vile Kristo hakuwa na dhambi wala kosa, yeye alitumia matamshi yaliyo sawa kabisa na mienendo yake kimaumbile. Alisema hivi: *Yeye hajatenda dhambi (1 Pet. 2:22)*.

YOHANA: Yeye pia alikuwa na urafiki wa karibu sana na Yesu. Na hii ndio sababu yeye aliweza kumuangalia kwa karibu sana. Wakati ule Yesu alipokuwa yuko mbali na vikundi vya watu, Yohana alishuhudia hivi: *Yeye hakuwa na dhambi (1 Yoh. 3:5)*.

PAULO: Yeye alikuwa ni msomi wa sifa kuu. Kuhusu mwokozi wetu Yesu Kristo, alisema: *Hakujua dhambi (2 Kor. 5:21)*.

Matamshi kama haya kutoka kwa Petro, Yohana na Paulo ni ushuhuda kamili kwamba kweli Yesu aliishi maisha yasiyo ya dhambi. Hata hivyo wako wale ambao wanaweza kuwa na hamu ya kutupilia mbali ushuhuda huu kwa kusema: “Aha, mwizi anayekaribia kuaga dunia, mtume Petro, Paulo na Yohana hawawezi kuwa mashahidi wa ukweli. Mwizi aliyekuwa anakaribia kufa alikuwa na wasi wasi, watume nao walikuwa wafuasi halisi wa Yesu kwa

Je, Kweli Mungu Anipenda?

hivyo yale walio yasema hayawezi kuchukuliwa kuwa ukweli kamili!”

Hebu nawe mkumbuke Pilato ambaye alikuwa ni gavana wa Rumi Yudea. Bila shaka yeye hakuwa rafiki wa Kristo. Hata hivyo pale alipokuwa anawajibu wale waliokuwa wanamfanyia mashtaka Kristo wakikusudia kwamba auwawe, alisema hivi:

Mtu huyu mmemleta kwangu kana kwamba anapotisha watu; nami tazama nimeamua mambo yake mbele yenu, ila sikuona kwake kosa lolote katika mambo hayo mliomshtaki (Lk. 23:14).

Lakini kuna haja gani kutilia manaani haya yalioyosemwa na wanadamu, tukifikiria kuhusu yale ambayo Mungu Baba mwenyewe alisema kutoka kiti chake cha enzi juu mbinguni. Pale mtu anapokuwa anajiandaa kuhutubia umati wa watu katika mkutano wa hadhara, ni jambo bora na la muhimu huyu mwenye kutoa hotuba akaribishwe na upole. Sawa na haya pia, pale Kristo alipokuwa anaanza huduma yake Mungu Baba ndiye aliyemkaribisha huyu ambaye ni mtoto wake mpendwa. Kwa sauti ya juu kutoka mbinguni, yeye alisema: *Huyu ni mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye (Mt. 3:17).*

Baba yetu aliye juu mbinguni alijua kwamba Yesu aliishi hapa duniani akiwa kama mwanadamu, na kwamba aliishi kulingana na matarajio yake pale alipomuumba mwanadamu kuishi duniani. Ni wazi kila mwanadamu amepungukiwa na utukufu wa Mungu (Rum.3:23). Lakini sivyo na Yesu. Yeye alikuwa bila dosari lolote la dhambi. Kwa hivyo pale

alipokuwa anaanza huduma yake kwa watu wote, Baba yake aliye juu mbinguni ndiye aliyemkaribisha kwa watu wa kupokea huduma hiyo (Yn. 17:11).

Na yeye alieleza vile alivyokuwa amependezwa na jinsi mtoto wa huyu alikuwa ameishi hapa duniani.

Sawa ni jinsi vile tumeeleza hapo mbeleni, Kristo hakuwa katika kiwango cha chini kuliko Mungu. Kwa hivyo ni jambo la uzito sana kuelewa kwamba Mungu alijipunguza uzito na kukubali azaliwe na mama bikira, Awe kama sisi wanadamu. Hata hivyo, kama Kristo hangejipunguza na kuwa mtiifu kwa Baba yake, hangempendeza Baba yake kwa njia hii. Hata hivyo, katika kazi yake yote hapa duniani, Kristo alimtii na kutegemea Baba yake, kwa hivyo maumbile yake ya kibinadamu ni kielelezo cha utukufu, na mapenzi ya Baba yake aliye juu mbinguni.

Sawa na wanadamu, Yesu alitembea hapa duniani akiwa Mungu. Pia wakati huo akiwa ni yeye aliyeumba dunia hii. Ingawa yeye hakuwa wa kiwango cha chini na Mungu kwa muda wa miaka 33. Yeye aliwaonyesha wanadamu jinsi vile Mungu anataka waishi. Hakuna lolote katika utu wa Yesu ambalo laweza kuchukuliwa kuwa kinyume cha mapenzi ya Mungu kuhusu yale amewatakia wanadamu.

Katika miaka hiyo yote, yeye alikuwa tayari kumtumikia Mungu Baba aliye mbinguni. Kwa hivyo Baba huyu aliye mbinguni alimfurahia mwanawe ambaye aliishi kwa njia bora kabisa.

Kwa yule mwizi ambaye alikuwa anakaribia kifo, na hata kwa Pilato, Yesu hakuwa na kosa. Nao Petro,

Je, Kweli Mungu Anipenda?

Yohana na Paulo walimchukuwa Yesu kuwa hana dhambi. Kwa Baba yake aliye na utukufu mbinguni Yesu hakuwa na dhambi wala kosa. Isitoshe, yeye alikufa kwa ajili yetu alikufa kwa ajili ya mapenzi yake kwetu.

Upendo usio na kipimo

Katika mawazo yako, hebu jaribu kuwaza kuhusu yale waliyoyaona wale walioshuhudia matukio yale ya kuhuzunisha ya ijuma njema ya kwanza. Karibu na msalaba, mkusanyiko ya watu waliyatazama yale yaliokuwa yakiendelea na mshangao na huzuni.

Kando na Mwokozi wetu, msalabani walikuwa wezi wawili. Hawa wawili walikuwa na makosa mbele ya wale waliokuwa pale. Pia wao walikuwa wamekiri makosa yao hata mbele ya Mungu muumba wao. Kwa ajili ya uzito wa makosa yao, sheria ilihitaji kwamba wahukumiwe kifo.

Akiwa kati kati ya hawa wezi wawili, Kristo alitungikwa msalabani. Yeye, mbali na wezi hawa hakuwa na kosa. Hakuwa na dosari la dhambi mbele ya mwanadamu. Yeye alikuwa hana lolote baya hata mbele ya Mungu yaani, *Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao; naye ametia ndani yetu neno la upatanisho (2 Kor. 5:19)*. Yeye alienda msalabani akiwa hana kosa *bali kwa damu ya thamani, kama mwana kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani ya Kristo (1 Pet. 1:19)*. Mungu alikubali kwamba Kristo afe badala yetu sisi wenye dhambi kwa ajili ya upendo wake.

Ilikuwa ni lazima wezi wale wafe. Lakini Kristo hakustahili kufa. Alipokuwa akizungumzia juu ya wale waliomkosoa, Yesu alisema: *Ndiposa Baba anipenda kwa sababu nautoa uhai wangu ili niutwae (Yn. 10:17,18)*. ANa alipokuwa akiwaeleza wafuasi wake juu ya upendo wake, yeye alisema: *Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake (Yn. 15:13)*.

Ni baada ya kufa na kufufuka ndipo mtume Paulo alipoeleza kwamnba Mungu alikuwa naye Kristo: *Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye (2 Kor. 5:21)*. Baada ya karne nyingi, ukweli wa Kristo kufa na kuchukua mauti kwa ajili yetu wanadamu ulielezwa na maneno haya:

Wewe una utukufu
Mimi ni dhambi yako
Umechukuwa yale yaliokuwa yangu
Na ukanipa yale ambayo ni yako
Umekuwa kile ambacho haukustahili kuwa
Ili niwe kile ambacho sikustahili kuwa

Mbegu ya Ngano

Akiwa anajua kifo chake kimekaribia, Yesu alisema wazi:

*“Sasa roho yangu imefadhaika, na niseme nini?
Je, niseme: ‘Baba, usiruhusu saa hii inifikie’?
Lakini ndiyo maana nimekuja ili nipite katika saa*

Je, Kweli Mungu Anipenda?

hii. Baba, ulitukuze jina lako.” Hapo sauti ikasema kutoka mbinguni, “Nimelitukuza, na nitalitukuza tena” (Yn. 12:27,28).

Labda hivi sasa unajiuliza inawezekanaje Mungu kutukuzwa kwa njia hii ya kusulubiwa?

Kabla ya Bwana wetu Yesu kuomba Baba wetu, yeye alikuwa tayari amewakumbusha wafuasi wake kwamba kulikuwa na haja mbegu ife kabla ya kupata mavuno. Tunasoma hivi:

Amin Amin nawaambia chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa hukaa hali hiyo peke yake; bali ikifa hutoa mazao mengi (Yn. 12:24).

Akiwa mwanandamu asiye na kosa, kifo hakikuwa na haki juu ya Yesu Kristo. Hata hivyo aliamua kufa kifo cha huzuni kwa ajili yako na mimi. Kifo chake kilichukua mahali ya kifo changu na chako. Kupitia njia hii, basi yeye akawa anaweza kujishindia wokovu wengi. Kwa hivyo Yesu hapa anatufahamisha kuhusu mpango wake huu wa kutuokoa na pia, na kwa kila yule anayemuamini, yeye pia anampa ahahdi hii ya wokovu.

[Mpango wake ni huu] *nalitoka kwa Baba, naminimekuja hapa ulimwenguni; tena nauacha; nakwenda kwa Baba (Yn. 16:28).* [Ahadi yake ni hii] *Basi mimi nikienda na kuandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu: ili nilipo mimi, nanyio muwepo (Yn. 14:3).*

La ajabu ni kwamba wako wale ambao wamechagua kutupilia mbali wokovu kutoka kwa Mwokozi wetu Yesu kristo. Nao wengine wameamua kutokuwa na msimamo halisi juu ya kujitoa kwa mwokozi wetu kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Hawatilii maanani kwamba haya yote ni kwa ajili ya mapenzi yake kwetu sisi wanadamu. Ikiwa mtu atamkana yesu, ama aamue kutofanya lolote kuhusu ujumbe wake Kristo, matokeo ni sawa: yeye amejitenga na chanzo cha maisha cha pekee, mwanga na upendo. Hali hii ya kutisha imeelezwa kwa undani kwa njia hii:

Kufa utakufa
Utakufa kifo kikubwa
Unaendelea kufa,
lakini bado hujakufa.

Hata hivyo, Bwana wetu Yesu Kristo alikufa sio tu ili uepuke jehenamu na badala yake uingie mbinguni, lakini pia kifo hiki kilimtoa Mungu mbinguni ili aje kwako!

Hata hivyo maisha ya milele sio hakikisho la kuingia mbinguni. Ni utukufu wako hata hivi sasa; kwa ajili ya kila mmoja ambaye ataweka imani yake na kumpenda Mwokozi wetu Yesu Kristo. Kwa wale kama hawa Mungu anasema.

Na huu ndio ushuhuda, ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo ndani katika Mwanawe. Yeye aliye naye mwana, anao huo uzima, asiye naye Mwana wa Mungu hana huo uzima wa Mungu hana huo uzima (1 Yoh. 5:11,12).

Je, Kweli Mungu Anipenda?

Uzima wa milele unapatikana katika Yesu Kristo. Na pale anapopata makao katika maisha ya mwanadamu, maisha ya milele huwa yameanza.

Bei Ghali

Jinsi vile tayari tumegusia, kama tunataka kuishi na Mungu milele, lazima tutafute na tupate suluhisho la shida yetu ya dhambi. Suluhisho lenyewe la dhambi lapatikana katika kifo cha Yesu Kristo. Hapa utukufu wake umewekwa. Haki imeonekana na upendo wa Mungu ukawakumbatia watu walio wenye dhambi kama wewe na mimi.

Katika kitabu chake *My Utmost for His Highest*, Oswald Chambers alitoa onyo hili:

“Jihadhari na wazo la kupambaza kwamba Mungu ni mwingi wa rehema, na mwenye upendo hivi kwamba atakusamehe kila jambo. Wazo hili halipatikani katika agano jipya. Sababu kuu ambayo yaweza kumfanya.” Mungu atusamehe dhambi zetu na kutuchukuwa kuwa wake ni kupitia msalaba wa Yesu Kristo. Hata tukielewa haya kuwa kweli, bado kuna uwezekano wa kuchukua msamaha wa dhambi kuwa jambo lisilo la muhimu na kusahau jinsi msamaha huu ulivyopatikana, na gharama yake ambayo ni ya juu.

Hapo mbeleni tumetaja mengi kuhusu jinsi vile kijana Willie Holt alijitoa kwa ajili ya wenzake. Hata hivyo lazima tutaje hapa kwamba hakuna

mfano wa kibinadamu unaoweza kufanana na jinsi vile Mungu alivumilia mateso pale msalabani kama mfano wa mapenzi yake kwetu sisi wanadamu. Na kupitia maneno yaliyo tamkwa na uwezo wa Roho Mtakatifu katika Maandiko Matakatifu Biblia, Mungu mwenyewe ametufungulia pazia ili tuweze kuona vyema yote yanayohusu upendo wake na kujitoa kwake kwa ajili yetu wanadhambi. Hata hivyo kiwango cha upendo wake kinazidi uwezo wetu wa kuelewa. Haya yote yanatusaidia kuweza kuona urefu, upana na ukubwa wa mapenzi yake Mungu.

Kristo alipokufa msalabani, aliumia kwa ajili ya dhambi zetu kwa njia tatu.

Alipokufa msalabani, mwili wake ulipata maumivu yaliyotokana na majeraha aliyoyapata. Maumivu haya yalifanya upendo wake ufikie karibu ukingoni. Na isitoshe, akiwa pale msalabani; yeye alitenganishwa na nuru utukufu na amani aliyofurahia daima katika umoja wake na baba.

Kwa kweli, mateso aliyoyapata na kuvumilia pale msalabani yanazidi ufahamu wetu sisi wanadamu. Hata hivyo tunapowaza kuhusu mateso aliyoyapitia, na hata yale ya kiroho, tunaweza kufahamu vyema kiwango cha upendo wake kwetu sisi wanadamu walio na dhambi.

Maumivu ya Mwili: Ni vigumu kulinganisha kuharibiwa au kuraruliwa kwa mchoro wa thamani ya mamillioni ya pesa kwa mfano mchoro wa

Je, Kweli Mungu Anipenda?

mwanasanaa mashuhuri sana kule ulaya Rembrandt na kuharibiwa au hata kuraruliwa kwa karatasi yenye uchafu. Mchoro ni wa thamani kubwa; karatasi chafu nayo labda haina thamani.

Sawa na mfano huu, kifo cha yeye aliye mkamilifu, Yesu Kristo hakiwezi kulingana au kufananishwa na kifo cha mwanadamu wa kawaida.

Katika Agano la Kale, tunasoma habari kuhusu unabii na utabiri uliohusu mateso ya Mwokozi wetu Yesu Kristo. Tunasoma kuhusu jinsi vile alivyovumilia haya yote. Hapa tunaelezwa kwamba kujitokeza kwake kutatatizwa na *kama vile wengi walivyokuustajabia, uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu yeyote, na umbo lake zaidi ya mwanadamu (Isa. 52:14)*. Hata hivyo tafsiri ya maneno haya katika lugha ya kiingereza haitoi wazi na kwa uzito unaostahili maana kamili ya maneno haya katika lugha ya Kiebrania. Katika maandiko haya ya Kiebrania Mungu alisema wazi kwamba mwanawe mpendwa angeteswa na kuumizwa kiasi kwamba hangefanana na mwanadamu. Mateso haya yalitajwa katika unabii wake kristo mwenyewe:

Angalieni tunapenda kwenda Yerusalemu; na mwana wa Adamu atatiwa mikononi mwa wakuu wa makuhani na waandishi, nao watamhukumu afe, watamtia mikononi mwa mataifa nao watamdhihaki, na kumtemea mate, na kumpoiga mijeledi, na kumuua; na baada ya siku tatu atafufuka (Mk. 10:33,34).

Kwa kweli haya ndiyo yalitokea baadaye, Marko alieleza kwa undani yale yeye mwenyewe aliyaona. *Wakampiga mwanzi wa kichwa, wakamtemea mate, wakapiga magoti, wakamsujudia. Hawa wakiisha kumdhihaki, wakamvua lile vazi la rangi ya zambarau, wakamvika mavazi yake mwenyewe; wakamchukua inje ili wamsulubishe (Mk. 15:19,20).*

Kiboko cha Warumi ambacho kilitumiwa kumchapa Kristo kilikuwa kimetengenezwa na ngozi wenye ncha zake kukawa na sehemu yenye uzito kama mfupa au timazi. Hizi zote zilirarua ngozi yake kabisa mgongoni na hata sehemu ya mbele kifuani Na hii ndio sababu hata zaburi tunasoma: *Wamenizuia mikono na miguu. Naweza kuihesabu mifupa yangu yote; wao wananitazama na kunikondolea macho (Zab. 22:16,17).* Kwa kweli kabisa Yesu mkamilifu katika kila njia alipitia kifo cha uchungu sana. Yale aliyotendewa yalishusha utu wake, na kumharibu sura.

Je haya yote yanakusaidia kuelewa jinsi vile Mungu alivyokupenda?

Maumivu Ya Kihisia: Ingawa maumivu aliyopata kimwili pale msalabani yanapita kiwango kile ambacho tunaweza kuelewa, sisi wanadamu, maumivu nayo ya kimwili yalikuwa ni sehemu ndogo tu ya maumivu aliyokumbana nayo kwa jumla.

Akiwa juu mslabani, yeye pia alipitia huzuni kuu ya maumivu ya kihisia. Mtume Yohana anafafanua zaidi kuhusu maumivu haya:

Lakini walipomjia Yesu kuona ya kuwa amekwisha kufa, hawakumvunja miguu; lakini askari

Je, Kweli Mungu Anipenda?

*mmojawao alimchoma ubavu kwa mkuki; na mara
ikatoka damu na maji (Yn. 19:33,34).*

Nimewasikia wataalam wa mambo ya afya wakisema kwamba ile damu na maji ilikuwa ishara kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya kupasuka kwa moyo. Wataalamu wa moyo hupiga hatua mbele nakusema pale maumivu yale yalipomvunja moyo, damu yake ilitoka na kuenea katika sehemu za ngozi iliyoleta damu na maji kutoka pale askari mmoja alipomchoma na mkuki katika ubavu. Katika Zaburi 69 ambapo kuna maono yanayohusu kifo cha mwokozi wetu, tunasoma haya kuhusu maumivu ya kihisia aliyokumbana nayo: *Laumu imenivunja moyo, nami ninaugua sana. nikangoja aje wa kunihurumia, wala hakuna; na wa kunifariji, wala sikumuona mtu (Zab. 69:20)*. Ajabu! Maumivu ya kihisia yalivunja roho ya Mwokozi wetu mwenye upendo.

Katika moyo wake wa upendo yeye aliyapokea maumivu ya taabu na dhiki kwa ajili ya wanadamu. Pia katika nafsi yake ambayo haikuwa na dosari lolote la dhambi zetu (*Ebr. 7:26*). Hapa ndipo Mwokozi wetu alikufa akiwa amevunjika moyo.

Je, tukio hili limekusaidia kuelewa vyema jinsi vile Kristo anavyokupenda?

Maumivu ya Kiroho: Watu wengi huweza kuelewa maumivu ya kimwili na maumivu ya kimawazo aliyoumia Mwokozi wetu Kristo lakini hawaelewi maumivu ya kiroho aliyokumbana nayo pale uhusiano na ushirika wake Kristo na Mungu Baba, na Roho Mtakatifu ulipovunjika.

Kwa muda wa masaa tatu ya dhiki kuu na giza kutoka saa sita mchana hadi saa tisa jioni, Kristo alikuwa ameachwa na Mungu Baba na Roho Mtakatifu. Akiwa msalabani, Yesu alilia: “*Mungu wangu, Mungu wangu mbona waniacha?*” (Mt. 27:46).

Siku hii ya ajabu, utatu wa Mungu, yaani Mungu Baba, Mungu mwana na Mungu Roho mtakatifu ulivunjika. Uhusiano huu katika utatu ulivunjika kwa ajili ya dhambi yako na yangu. Matokeo ni kwamba alipokuwa pale juu msalabani, Mungu Baba hangeweza kuishi akiwa pamoja na dhambi, ambayo ilikuwa sasa imejingiiza katika mwili wake ambao haukuwa na dhambi. Na yeye alichukua mzigo huu wa dhambi: “*Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye...*” (2 Kor. 5:21).

Kwa hivyo si ajabu kwamba pale Yesu alipokufa, dunia hii ya uovu ilifunikwa na kivuli cha giza la kutisha kwa muda wa saa tatu.

Katika jua tunaweza kungoja giza tujifiche na kufungia utukufu wake, Pale Kristo, muumba mkuu, alipokufa kwa ajili ya dhambi ya kiumbe mwanadamu.

Isaac Watts (1674–1748)

“*Na hii ndio habari tuliyosikia kwake, na kuihubiri kwenu, ya kwamba Mungu ni nuru, wala giza lolote hamna ndani yake*” (1 Yoh. 1:9). Mwanga unaotokana na utukufu wa Mungu, na giza lile linalotokana na dhambi ya mwanadamu haviwezi kuwa pamoja. Jinsi vile giza hupotea unapowasha taa. Giza nalo litatandaa

Je, Kweli Mungu Anipenda?

pale taa hii inapozimwa. Ni giza lilijitpokeza na kutnada kila mahali pale Kristo alipoebeba mzigo wa dhambi za mwanadamu.

La kuhuzunisha ni kwamba giza hili la kiroho ndilo linamngoja yule ambaye anatupilia mbali mwangaza unaotokana na upendo wa Mungu. Giza ambalo ni zito kuzidi usiku wa manane, giza lenye upweke wa jela ya muda mmoja, na pia giza ambalo litadumu kwa muda unaozidi kipimo cha kawaida cha muda. Katika Yohana 3:19, tunasoma hivi: “... na hii ndio hukumu; ya kuwa nuru imekuja ulwenguni na watu wakapenda giza kuliko nuru. Kwa maana matendo yao yalikuwa maovu” (Yn. 3:19). Kumuacha Yesu kutakuletea giza kuu la kiroho na kifo cha kiroho na kifo cha milele. Kumkubali Yesu kutakuletea uhai wa kiroho na maisha ya milele.

Kilio Cha Mshindi

Habari njema ni kwamba pale saa zile tatu za dhiki zilikuwa zakaribia kikomo, Kristo hakulia na kusema kwamba ameshindwa. Tendo hili la upendo la kumuokoa mwanadamu lilikuwa limekamilika. Kwa hivyo, yeye akalia kwa sauti ya juu na kusema “***Imekwisha***” (Yn. 19:30).

Gharama ya kuokoa nafsi yako na yangu imelipwa, Na sasa yote yamekwisha. Imekwisha!

Kwa hivyo, baada ya kumaliza kazi ya kumuokoa mwandamau, ushirika wa mwanga ambao Kristo alikuwa nao na Mungu Baba ulirudia hali yake ya pale mwanzo (Yn. 17:5). Kwa hivyo, hakuna lile ambalo

wewe au mimi tunastahili kufanya kama gharama ya kulipia dhambi zetu. Pia, hakuna lile shetani anaweza kufanya ili aondolee mbali yale Mungu alikutimizia kupitia kifo cha Kristo pale Msalabani. Sumu ya shetani, sumu hatari kama ile ya nyoka imetolewa machungu yake.

Kifo Chashinda Ukuu wa Mauti

Sababu iliyomfanya Mungu ajivishe vazi lilimofanya awe sawa nasi sisi wanadamu ambao wana mwili na damu ni kwamba kwa kufanya hivyo, ndipo angeweza kufa kama sisi wanadamu. Na sababu ingine ni kwamba akiwa na mwili sawa na wetu sisi wanadamu, kupitia kifo chake yeye: “...*kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, ibilisi...*” (Ebr. 2:14).

Sawa na jinsi vile Daudi alitumia upanga wake Goliathi kumuua yeye Goliathi, Kkristo naye alichukua chombo chae shetani ambacho ni kifo ili amshinde huyu shetani. Kristo ndiye wapekee aliye na uewzo wa kuwakomboa wanadamu wote; wake kwa waume. Yeye ndiye anayetumiwa na mungu kuwaokoa wanadamu. Ni yeye anayewaweka huru wanadamu wawe huru kutoka kwa kifo na kifungo. Shetani alikuwa amepanga iwe hivi ili mwanadamu amuasi Mungu ambaye alimuumba huyu mwanadamu kwa mfano wake yeye mwenyewe.

Akiwa katika mwili wake hali wa kibinadamu kristo aliweza kumshinda shetani pale alipofufuka

Je, Kweli Mungu Anipenda?

na kutoka kaburini. Na hapa tunasoma kuhusu jinsi alivyoingia mbinguni. “...alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu...” (Ebr. 6:20). Kwa mara ya kwanza, mwanadamu ambaye **hakuwa na kosa**, wala **dhmabi**, mwanadamu aiye na **dosari** aliingia mbinguni. Kwa ajili yake kufa msalabani, yeye ametufungulia njia ili nasi pia tuifuate.

Nyakati zake Charles Wesley, yeye aliamini kabisa kwamba Mungu alimpenda na ndio sababu aliweza kuandika wimbo wake maarufu katikaingereza “Amazing love: how can it be; that Thou, my God; should die for me?” (Itakuwaje upendo wa kiasi hiki kwamba Mungu akanipenda kiasi hiki cha kuweza kufa kwa ajili yangu?)

Na Sasa Kristo Amefufuka!

“Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala. Maana kwa kuwa mauit ililetwa na mtu” (1 Kor. 15:20-21).

Marehemu Daktari Sangster ni mmoja wa wale watu maarufu ambao nimewahi kusikiliza hotuba zao. Yeye alipenda sana kutumia kipawa chake hiki kushuhudia kuhusu wema wa Mungu. La ajabu ni kwamba kabla ya kifo chake, yeye hakuweza kutumia kinywa chake kwa ajili ya maradhi yaliyodhuru mdomo wake. Kabla ya kifo chake, alimwita binti yake, akamuomba kalamu, akaandika hivi: “Ni heri ukose ulimi, lakini uwe na hamu ya kumtaja Mungu kwa sauti ya juu na kushuhudia kwamba amefufuka,

kuliko kuwa naulimi na kukosa hamu ya kushuhudia kwamba Kristo amefufuka.”

Mtume Paulo aliposimama mbele ya mfalme Agripa ili ajibu mashtaka aliyofanyiwa ya uongo, yeye aliwakumbusha mateso ya kifo na kifo na baadaye kufufuka kwa Kristo: *“Ya kwamba Kristo hana budi kuteswa na ya kwamba yeye kwanza kwa kufufuliwa katika wafu atatangaza habari za nuru kwa watu wake na kwa watu wa mataifa”* (Mdo. 26:23).

Hata hivyo, kabla ya Kristo kufufuka, jinsi ilivyoandikwa katika Agano Jipya, tunasoma habari kuwahuu watu fulani ambao walifufuliwa kutoka wafu. Moja wao ni Lazaro. Na pia bintiye Yairo. Na pia mtoto wa mama wa Naine. Na ingawa Yesu aliwafufua hawa waliokufa, miaka michache baadaye, wao waliaga dunia tena. Mwokozi wetu alikufa, akazikwa. Lakini sasa yeye yuko hai. Leo hii, yeye hayuko tu hai kimwili; yeye pia yu hai kiroho; na uhai wake huu ni wa milele. Ni yeye wa kwanza kufufuka. Ingekuaje kaburi liweze kumfunga yeye aliyumba na kuleta uhai. Kwa vile Kristo katika hali ile ya kuwa Mungu, ni yeye aliyumba vyote vilivyoko duniani, yeye hawezi akashikwa na kufungwa kaburini.

Kwa vile Kristo ni sawa na mwandamu asiye na lolote lenye dhambi, yeye alileta uhai kutoka kaburini, na akatufungulia njia ya kwenda mbinguni; nayo njia hii iko wazi kwake yeyote atakayeamua kufuata, kupitia kumpokea kwa imnai. Kwake yule takayempokea, kuna ahadi hii:

“Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata

Je, Kweli Mungu Anipenda?

wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhisha pamoja; yaani tumeokolewa kwa neema. Akatufuufa pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu” (Efe. 2:4-6).

Alipokuwa anawaandikia walio na imani katika mji wa Korintho, mtume Paulo aliwakumbusha kwamba walikuwa wameokolewa kutka madhara ya dhambi zao kwa ajili ya kupokea ukweli kwamba Kristo alikufa. “*Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya ttau, kama yanenavyo maandiko maandiko” (1 Kor. 15:3,4).* Leo hii, kila mwenye imani ana aamini kambya Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zake; na kwamba, baada ya kifo chake, amefufuka, na kupitia kufufuka kwake, amemwezesha kupokea maisha mapya ambayo yametokana naye kuzaliwa mara ya pili.

Siku ya Kwanza Hadi ile Ya Tatu

Labda hivi sasa unjiuliza ni nini kilitokea toka pale Kristo aliposulubiwa, akafa, hadi siku ya tatu alipofufuka. Mungu alijua swali hili litajitokeza, na hapo akwa na jibu hili:

Basi neno hilo, Alipaa, maana yake kama siyo kusema kwamba yeye naye alishuka mpaka pande zilizo chini ya nchi? Naye aliyeshuka nduye aliyepaa juu sana kupita mbingu zote, ili avijaze vitu vyote (Efe. 4:9,10).

Maandiko Matakatifu yanatueleza wazi kwamba kabla kwenda mbinguni, Kristo alienda chini kabisa kule ambako hakufai. Na alipotoka huko, ndipo akaingia juu mbinguni ambako aliwaongoza wateule wa tangu siku a nyakati za Agano la kale (Ambao walikufa wakiwa na imani) Leo hii, yeyote anayeshikilia imani hii ana hakikisho kwamba kifo ni lango la kupitia kuelekea maisha yaliyo bora, maisha ambayo ni uzima wa milele. Kristo mwenyewe ameshinda kifo cha mwili na roho kwa ajili, na kwa niaba yetu sisi. Katika wakorintho wa kwanza tunasoma hivi:

Ku wapi, Ewe mauti, kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti uchungu wako Uchungu wa mauti ni dhambi, na nguvu za dhambi ni torati. Lkaini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo (1 Kor. 15:55-57).

Je, Kweli Mungu Anipenda?

La Ziada—Zawadi ya Upendo

Ni jambo la kutia moyo sana Kristo ametutangulia kwenda mbinguni. yeye amefungua njia, nasi tunaweza kufuata njia yake hiyo ya ushindi. Pia ni jmabo la kutia moyo kwamba kabla ya kifo chake, Kristo aliahidi kwamba baada ya kwenda mbinguni, angemtuma roho wake awe na walio na imani hapa duninai. Yey aliwaambia wafuasi wake haya:

“Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake Na neon hilo alilisema katika katika habari ya Roho ambaye wale wamwaniye watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatakuzwa” (Yn. 7:38-39).

Lakini sasa mimi naenda zangu kwake yeye aliyenipeleka, wala hakuna mmoja wenu aniulizaye, unakwenda wapi? Nami nitamwomba Baba, naye atawapa msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele. Ndiye Rogho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyo mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu. Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu. Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo ynagu na kuwapasha habari (Yn. 16:5;14:16,17;16:7,14).

Tayari tumeona jinsi Mungu alivyojitukuza kupitia kifo cha mwanawe wa pekee, Kristo. Sasa huenda ukwa unajiuliza, “Kristo anaweza kujitukuza kwa njia ipi pale anapomtuma Roho Mtakatifu kwako na kwangu?”

Jibu la swali hili ni kwamba Kristo anatakukuka katika maisha ya kila yule aliye na imnai, na hasa kupitia maisha ya huyu aliyeamini ambaye ndani yake kuna upendo wa Mungu. Katika Warumi tunasoma hivi: *Na tumaini halitahayrishi; kwa maana pendo la Mungu limekwisha kimiminwa katika mioyo yenu yetu na roho Mtakatifu tuliypewa sisi (Rum. 5:5)*. Upendo wa Mungu ambao unajitokeza na kujidhihirsha kupita Roho Mtakatifu ni kilele cha wema wa mwanadamu. Kupitia imani, wewe uliye na imani unitikia wito ulijitokeza na kuonekana pale msalabani aliposulubiwa mwokozi wetu Kristo. Kupitia Roho Mtakatifu, kazi hii iliyofanyika pale msalabani inatuwezesha sisi pia kuwa na upendo huu wa ajabu. Nasi tunaweza kuelekeza upendo huu kwa wenzetu. Ni upendo wa ajabu!

Kuamini kwamba Kristo alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zako, na baada ya kuamni hivyo na kuwa na roho ile ya kushukuru Mungu kwa ajili ya tukio hili; hii ni njia moja ya kuwa na hakikisho maishani kwamba umepokea msamaha wa dhambi na pia umepokea wokovu.

Na pale unapoyafanya maisha yako yawe chombo ambacho Kristo yuko hai ndani yake; hii ni sawa na kuwa chombo ambacho atakitumia kuleta duniani iliyojaa chuki upendo.

Je, Kweli Mungu Anipenda?

Mtaalamu wa mabo ya dini ambaye alikuwa na sifa kuu sana kule Ujerumani aliwahi kuulizwa hivi: “Je, unapowaza kuhsu Mungu, ni wazo gani ni la maana sana kwako?” Naye akajibu sawa na jinsi vile watoto wadogo hujibu. Akasema: “Yesu aanipenda: nami najua kwamba anaipenda kwa vile Biblia inanieleza hivyo.”

Ni kweli kabisa: Mungu anipenda mimi. Yeye pia anakupenda.

Ni upendo huu uliandaa mpnago wetu sisi
kupokea wokovu,
Ni kwa ajili ya neema zake zimetuwezesha
kupokea wokovu huu,
Kulikuwa na utengano mkuu kati yetu sisi
wanadamu na Mungu,
na ni kupitia pale mslabani utengano huu
umeondolewa!
Ni rehema nyingi zimetuwezesha kupokea
wokovu, na neema tele,
Tumesamehewa dhambi,
Na ni pale msalabani mzigo wa dhambi
umeondolewa.



Barua kutoka nchini Iraq

*“Mimi nilishikilia imani ya kiislamu katika jumba la schel-
tey. Familia ynagu ilinifunza jinsi ya kuomba na kukosa chakula
kwa ajili ya kuomba. Mavazi ynagu yalikuwa yale ya asili ya kina
mama katika dini yetu.*

*“Nilihakikisha nafunika uso wangu ili mwanamume yeyote
asitende dhambi pale anapouona uso wangu. Kwa ajili ya haya
yote, nikawa na wakati mwingi ambapo si kuwa na jmabo la ku-
fanya. Kwa hivyo, nikatumia muda wangu huu kusikiliza vipindi
nmbali mbali vya redio. Na katika vipindi hivi nikaksikiliza vingi
vya dini. Siku moja nilimuona dada mkwe akiwa na vijibandiko
vingi vyenye rangi mbali mbali za kupendeza. Basi nikaandika
barua nikitumia anunai ya dada yangu huyu.*

*Na katika majibu ya barua hii, nikapokea kitabu hiki Kiu
Cha Kumtafuta Mungu.*

*“Nilijaribu kuelewa maana ya jina la kitabu hiki. Katika
ukurasa wa saba kuna swali: ‘Je, Mungu kweli anipenda?’ Nili
tilia maanani sana sehemu ya ukurasa huu iliyosema hivi:
‘Mungu ameonyesha upendo wake kwao kupitia yale ambayo
aliyafanya pale msalabani. Unapoelewa maana ya msalaba,
basi hakuna haja ya kutafuta ushaidi zaidi kwamba MUn-
gu anakupenda...’*

*“Nilisoma ukurasa huu zaidi ya mara mia moja. Na hapo
niakelwa wazi kwamba kweli msalaba ndio mjia yanmgu ya
kweli...”*

– Barua hii imetoka Trans World Radio

Je, Kweli Mungu Anipenda?

Hebu Fikiria

1. Je, unawezaje kumonyesha mwenzako kwamba unampenda?
Je, ni kupitia yale utakayosema?
Au je, ni kupitia yale unayotenda?
2. Je, Mungu alitumia njia gani kudhihirisha kwamba anakupenda?
3. Je, utatumia njia gani kama kuonyesha kwamba umepokea wokovu?

*Katika enzi hii ya mitambo ya kisasa
inayotumiwa katika vyumba vya upasuaji
mahospitalini, kila daktari anafunzwa
kutambua kwamba damu ni uhai. Damu
na uhai haviwezi vikatengwa: moja
ikikosa basi, nyingine haiwezi kuwako.*

DR. PAUL BRAND

Ni Wapi Nitapata Maisha

*S*likuwa inakaribia usiku wa manane; na tulikuwa tunajiandaa kabla ya safari ya reli ya masaa 18.

Mimi na mke wangu tulikuwa pamoja na wasafiri wenzetu katika stesheni ya gari ya Gare St. Lazare mjini Paris. Tulikuwa tuna subiri kwa hamu tuingoja afisa wa kituo hicho atufungulie lango la kutuwezesha kufikia gari ambalo tulitaka kutumia. Idadi kubwa ya wale waliokuwa pamoja nasi walikuwa vijana.

Tulipokuwa tunatembea kati yao, ilionekana kana kwamba kila taifa la ulaya lilikuwa lina wakilishi hapa. Kati ya vijana hawa kulikuwako na, wale ambao walikuwa wanajaribu kupata usingizi wakitumia mifuko ya mizigo yao kuwa kama sehemu ya kulalia vichwa. Nao wenzao ambao walikuwa macho walishika doria pale, huku wakikula vyakula walivyovibeba wengine wakinywa maji ya chupa.

Tukiwa tunangoja pale, tulianzisha mazungumzo na baadhi ya vijana hawa. Na jambo moja ambalo lilijitokeza ni kwamba ingawa walionekana kuwa wenye furaha, ilikuwa wazi wao walikuwa hawajapata kile ambacho walikihitaji na hamu sana maishani.

Baada ya muda mfupi, mazungumzo yetu yalielekea kwake yule ambaye tulikuwa tumeandamana naye: huyu ni mwokozi wetu Yesu Kristo!

Na tulipokuwa tunaendelea na mazungumzo yetu, baadhi ya vijana hawa ambao hawakuwa na utulivu walianza kusema jinsi vile wana hamu ya kupata maisha kamili. Kati yao waliamini kwamba maisha haya watayapata katika mji ulio karibu na hapo. Nao wenzao wakawa waanamini kwamba maisha halisi yatapatikana katika urafiki wa baadaye. Wengine nao wakasema wanatarajia maisha bora katika matumizi ya madawa ya kulevywa na ulevi. Na kati yao wako wale ambao hofu yao kuu ilikuwa huenda wakaambukizwa maradhi hatari.

Nao wataalamu wanaita virusi vinavyoleta maradhi haya, virusi viletavyo upungufu wa kinga mwilini (*Human immuno-Deficiency virus, HIV*). Pale maradhi hujitokeza kabisa katika mwanaume, mwanamke, kijana au msichana; maradhi haya huitwa ukimwi. Pale mtu anapogunduwa kwamba ana maradhi haya matokeo huwa hofu na kuvunjika moyo. Kote duniani, watu wanajuwa kwamba ukimwi ni maradhi ambayo viini vyake hupatikana katika damu. Pale mishipa huwa chombo kinachobeba viini, basi chombo hiki sasa ni kama mto unaobeba kifo.

Ningependa kutaja hapa kwamba ingawa damu ndio uhai wetu wanadamu; ninapooni damu, mimi hushikwa na woga. Damu ni kitu ambacho sipendi kukiona. Siku moja nilijitolea kwenda kushuhudia upasuaji katika hospitali moja mjini London. Na pale

kisu cha daktari kiliposhika ngozi ya mgonjwa tayari kukata, karibu ni poteze fahamu.

Daktari rafiki yangu huyu aliona jinsi vile nilivyokuwa natokwa na jasho, na jinsi vile rangi ya ngozi yangu ilivyokuwa imebadilika. Hapo akanisihii niondoke mle chumbani, niende zangu. Sikuhitaji ushawishi zaidi. Niliondoka nikaenda zangu mara moja. Sikuweza kustahaimili yale yanayoendelea katika chumba cha upasuaji.

Na hata kama wewe unaogopa damu, ukiwa mgonjwa, unaweza ukapeuka madhara makuu pale tu unapo ongezwa damu mwilini. Kwa ajili ya hatua kuu ambazo zimepigwa katika nyanja ya utabibu, damu yaweza kutolewa kwa yule aliye na afya nzuri akaongezewa yule ambaye hali yake si nzuri. Damu hiyo ambayo ameongezewa ndio itakayo muokoa.

Na hapo mbeleni kabisa, miaka mingi kabla utaalamu wa kutoa na kuongeza damu mwilini haujagunduliwa, Mungu alisema hivi katika Maandiko Matakatifu:

Kwa kuwa uhai wa mwili u katika hii damu; nami nimewapa ninyi hiyo damu juu ya madhabahu, ili kufanya upatanisho kwa ajili ya nafsi zenu; kwani ni hiyo damu ifanyayo upatanisho kwa sababu ya nafsi (Law. 17:11).

Daktari Brand anaisistiza kwamba damu ina kile ambacho hasa ndicho uhai. Katika mazingira yale ya kisasa ya upasuaji hospitalini, kila dakatari hufunzwa kutambua kwamba damu ndio uhai. Ni damu huwa na uhai: hivi viwili ni sawa na kimoja – damu na uhai.

Hata hivyo, wengi hawajatambua kwamba ingawa maradhi yanayodhuru damu kama ukimwi, humdhuru yule aishiye kwa namna ya kujileta karibu na maradhi hayo yenyewe, kuna maradhi mengine ya damu yanayodhuru kila mwanadamu.

Ni kwa sababu, *Mungu alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja (yaani damu moja), wakae juu ya uso wa nchi yote (Mdo. 17:26).*

Uchafuzi huu hatari umeenea kwa wanadamu wote. Katika Biblia chanzo chake kinarudi nyuma hadi wakati ule wa Adamu ambaye ni mwanadamu wa kwanza duniani. Cha kuchafuliwa huku kwa damu ni Adamu, baba wa vizazi vyote vilivyomfuata. Wakati mtu wa kwanza, Adamu alipotenda dhambi, vizazi vyote vilivyofuata (*1 Kor. 15:45*).

Vya kila aina na rangi, kote duniani viliwekwa chini ya hukumu ya kifo. Biblia inasema wazi kwamba: katika Adamu, wote hufa (*1 Kor. 15:22*).

Na katika maradhi kama haya ya ukimwi, kifo kinaingia mwilini kupitia virusi ambavyo hubebwa na kustawi katika damu. Sawa na maradhi haya, kifo kinatokana na uchafu wa wanadamu unaonea kizazi hadi kingine tokea wakati ule wa Adamu. Na kama haingekuwa hivi, basi wanadamu wangeingia moja kwa moja hadi mbinguni pasipo kupitia njia ile ya kufa.

Ni jambo la kushukuru Mungu kwamba pale Kristo alipozaliwa, basi damu yenye uhai iliingia pia katika jamii hii ya Adamu. Nayo haya yalifanyika kwa njia hii: Malaika Gabrieli akamuambia Mariamu kwamba atapata mimba na kuzaa mtoto wa kiume, na

kwamba jina lake ataitwa Yesu. Malaika alimweleza mama huyu bikira jinsi vile haya yote yangetokea.

Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo, hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, mwana wa Mungu (Lk. 1:35).

Muujiza ulitokea pale mbegu ya mama ilipokutana na Mbegu baba ambaye alikuwa ni Roho Mtakatifu. Na kupitia muujiza huu, maisha ya Mungu yaliingia kuwa pamoja na maisha ya mwandamu. Na pale mtoto alipoanza kukua katika tumbo la mzazi Mariamu, nayo damu ikaanza kupitia kwenye mishipa humo ndani, damu yake ya dhamana kubwa haikuwa na uchafu wala kubeba magonjwa. Damu ya Kristo ilikuwa na uhai kamili.*

Damu yetu sisi wanadamu ni kitu kigumu kuelewa. Hata hivi sasa, wako wengi wanaoendnelea kufanya utafiti na wanajigundulia mengi ambayo ni mapya kabisa kuhsu damu.

Kwa kifupi, tunaweza tukaita damu kiungo cha kusafisha mwili, au kiungo cha kuleta uhai, au sehemu ambayo ni kinga ya kuzuia maradhi na kadhalika.

*Katika kitabu, THE CHEMISTRY OF BLOOD, mwandishi Daktari De Haan anataja wataalamu ambao wamechapisha matokeo ya utafiti ya utafiti wao katika majarida yanayosema kwamba mama hutoa nyumba na chakula ambacho mtoto hula. Nayo damu yote hutoka katika sehemu ya nyumba ya uzazi ya mama. Tangu siku ile mbegu za uzazi hukutana, hakuna hata tone moja hutoka kwa mama na kumfikia mtoto. Naye mwandishi Daktari Robert Coleman akigusia maoni ya De Haan, aliyatilia mkazo. Pia anasema kwamba kwa vile Kristo alitoka kwa Mungu moja kwa moja, hii inafutilia mbali hoja ile kwamba dhambi hutokana na kizazi.

Haya yote ni maajabu, hata hivyo la kufurhaisha ni kwamba Mungu ametupatia mto wa damu ya Kristo ambayo inaweza kutenda maajabu kuliko yote ambayo tayari tumetaja. Damu hii yaweza ikawa yako endapo una hamu ya kuwa hai. Kwa yule ambaye ana dhambi, damu hii yaweza kusafisha na kuondoa dhambi hiyo. Kwa yule ambaye amekufa kiroho. Damu hii ya Kristo yaweza kuwa kizuizi cha kukuondoa katika hatari hii ya kufa kiroho. Damu hii yaweza kuwa kinga ili usishambuliwe na shetani. Kuhusu damu, Maandiko Matakatifu yanasema hivi: *Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usifaa mlioupokea kwa baba zenu; Bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo* (1 Pet. 1:18,19).

Damu: Uwezo wa Kuosha

Juzi, vyombo vya habari vilitangaza kwamba shirika moja la usafishaji, kwa ajili ya hamu ya kupata pesa lilikuwa limekosa kudumisha hali ya usafi inayostahili. Katika harakati ya kutaka kupata mapato zaidi, shirika hili lilitumia gari kubeba mizigo iliyokuwa na sumu. Na katika safari ya kurudi, shirika hili lilibeba vyakula vya maji maji. Matokeo ni kwamba wale waliovila vile vyakula wakaanza kuugua.

Katika miili yetu sisi wanadamu, Mungu ameumba njia ya usafiri iliyo ajabu sana. Barabara hii ya usafiri hubeba chakula katika chembechembe zikitwazo *cells*, na pia kutoa uchafu kutoka chembe chembe hizi.

Kwa ajili ya uhodari wake katika kutuumba sisi wanadamu hakuna wakati utaweza kupata kwamba uchafu au sumu imejiingiza katika barabara inayobeba damu. La ajabu ni kwamba hakuna hata chembe chembe moja ambayo ukubwa wake ni zaidi ya ule wa nywele moja. Na kama uchafu hautatolewa kutoka damu, basi kuna hatari kubwa.

Kwa kweli, haya ndiyo Mungu angausia anapoeleza jinsi ya kuondoa uchafu unaotokana na dhambi katika maisha yetu. Kuosha huku ni kupitia damu ya thamani ya Yesu, Maandiko yanasema hivi: *bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote (1 Yoh. 1:7).*

Na isitoshe, Mungu anasema hakuna njia tofauti ya kutuwezesha kupata msamaha wa dhambi.

Na katika torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo (*Ebr. 9:22*).

Damu: Uwezo wa Kuleta Maisha

Kazi nyingine ya damu ni kubeba maji na chakula kote mwilini. Ni kupitia njia hii damu huendeleza uhai. Damu ikikosa kufika kwenye chembe chembe za nyama katika mwili, sehemu hizi hufa. Kwa hivyo, mwili huaga dunia pale damu inapokosa kuzunguka. Ni wazi basi uhai wa mwanadamu unapatikana katika damu.

Na hapa tunakumbushwa kuhusu yale mwokozi Kristo alisema, yaliyowashtua wengi kuhusu damu yake. Yeye alisema hivi:

Amin amin nawaambieni, msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu. Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho. Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinywaji cha kweli (Yn. 6:53-55).

Hata hivyo, Yesu aliendelea kufafanua maana ya matamshi yake haya. Alisema: *Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake (Yn. 6:56).*

Ni furaha jinsi gani kuelewa ni wapi unaweza kupata maisha ya kiroho? Damu ya Kristo ilimwagika ili wenye dhambi wapate wokovu. Na kwa ajili ya kumwaga damu yake sasa tunaweza kuishi naye. Yesu alieleza maana halisi ya kunywa damu yake aliposema: Mimi niko ndani yake!

Baada ya kujitambua, na pia kujua nguvu za kufufuka kwa Kristo, na uwezo alio nao, wale waaminio wanaweza kushuhudia kwamba: “Kristo aliyefufuka anaishi ndani yangu. Kwao watu kama hawa, kwenda kwenye meza ya Bwana na kushiriki divai na mkate ni jambo la kumshukuru Mungu na la kupendeza.*

Uwezo wa kutoa maisha unaopatikana katika damu ya Yesu Kristo ni muujiza ambao anapewa

* La kuskitisha ni kwamba wako watu mamilioni bado wanaamini kwamba mkate na divai ambavyo hutumiwa katika meza ya Bwana wakati fulani hubadilika na kuwa sawa na damu na mwili wa Kristo. Divai na mkate ni vyombo ambavyo ni ishara ya damu na mwili wake mwokozi wetu Kristo.

mwenye imani kupitia nguvu za Roho Mtakatifu pale anapozaliwa upya mbinguni. Kwa hivyo, kwa yeyote aliye na hamu ya kuishi, ni sharti akubali kuongezewa damu hii inayodumisha uhai!

Damu: Nguvu ya Kulinda

Kuna kazi ya mwujiza ya damu ya mwanadamu. Nayo kazi hii ya damu ni ile ya kulinda mwili.

Juzi, hofu kuu ilitandaa duniani pale maradhi ya uvimbe wa manenani au makwapani yalipojitokeza nchini India. Hofu ilifanya wanaofanya kazi ya uchukuzi kuwa wanoasha ndege kubwa za abiria kabla ya kutoka humo nchini. Hata ilifikia wakati wasafiri walikuwa wanafanyiwa uchunguzi kabla ya kukubaliwa wasafiri. Wasafiri wengi walizuliwa wasiende India kwa ajili ya maradhi haya.

Ingawa maradhi haya yaliweza kukabiliwa kwa njia hiyo, bado yako maradhi ya aina aina ambayo yanazidi kuwasumbua wanadamu. Miili yetu bado hudhuriwa na uchafu wa aina aina. Hata hivyo, damu yetu sisi wanadamu ina uwezo wa kupiga vita maradhi na hata kuondoa viini hatari. Damu pia ina uwezo wa kutukinga tusidhuriwe na maradhi.

Na pale viini vya maradhi vinapovamia miili yetu, kuna sehemu fulani za damu ambazo huwa tayari na jukumu la kupiga vita viini kama hivi. Na sehemu ya kupiga maradhi vita ni chembe chembe nyeupe za damu. Chembe chembe hizi hujitokeza mara moja na kuanza kupiga vita maradhi. Kwa hivyo chembe chembe hizi ni kinga ya kuzuia maradhi ya aina mbali mbali.

Damu ya mwokozi wetu Kristo nayo ina uwezo wa kutuinga dhidi ya maovu ya shetani. Ni damu yake Kristo inayomkinga Mkristo asishambuliwe na adui shetani. Na katika kutabiri juu ya vita vya mwishho kati ya shetani na wana wa Mungu, tunasoma hivi katika maandiko Matakatifu: *Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa (Ufu. 12:11)*. Wewe pia unaweza kushinda mashambulio yake shetani kwa kutumia nguvu kutoka kwa damu ya Kristo.

Ushindi huu wa Kristo ulitabiriwa mara moja pale shetani alipowadanganya Adamu na Hawa. Na hapo Mungu akaamua kwamba ni uzao wa mwanamke utakaomwangamiza shetani. *Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uazo wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino (Mwa. 3:15)*. Mbegu ya mwanamke ndiyo itaangamiza kichwa chake shetani, lakini sio kabla ya nyoka huyu kuuma kisigino cha Masihi. Ni Yesu Kristo mwenyewe, mbegu ya mwanamke aliye mwaga damu pale msalabani ili kupitia kifo chake,

basi kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani Ibilisi (Ebr. 2:14).

Tofauti kabisa na wanafunzi wale tulikutana nao pale Gare St. Lazaire mjini Paris, wengi wameshagundua chanzo halisi cha maisha.

Hapo nyuma, tukiwa na Dorothy, tulikutana na wenyeji kutoka nchi ya Uganda. Umati wa Waganda mia moja hivi walikuwa na uhakika kwamba wamegundua maisha ya kweli. Kupitia damu ya Kristo, wao walikuwa wamepokea nguvu kamili kusafisha dhambi, maisha ya kweli, na nguvu za kuwawezesha kumpinga shetani na hila zake.

Na ingawa tulikuwa tumeshawishiwa na maafisa wa Ubalozzi nchini Kenya tusitembelee Uganda kwa ajili ya usalama, mimi na Dorothy tulijikuta tumesukumwa na Roho Mtakatifu mpaka kwenda nchi hii. Mungu mwenyewe ndiye aliyeandaa mikutano hapa Uganda. Mikutano hii iliwaleta pamoja makasisi pamoja na wake zao.

Na kando mipango ya mikutano, Mungu pia alikuwa ameshughulikia usafiri wetu. Ndege tuliyotumia kutoka Entebbe humo nchini ilikuwa ya mwisho kabla ya mapinduzi yaliyomng'oa kiongozi mmoja kutoka mamlaka. Wakati wa kuingia humo, mara tu baada ya kutua, tulihisi hali ya wasi wasi hewani. Hali ya kutoelewana na uchafu wa aina mbali mbali ulikuwa kila mahali. Barabara tuliyopita ilikuwa imejaa mashimo ya mabomu. Baada ya safari ya muda mfupi, tulikutana na askari waliokuwa na silaha. Hatukujua kama walikuwa ni askari wa serikali ama waasi, ama magaidi wa kawaida ambao wamevaa mavazi ya kijeshi.

La ajabu ni kwamba waligundua mara moja dereva wetu alikuwa mtu wa kabila lao na hapa wakatukubalia twendelee na safari yetu bila kutudhuru kwa vyovyote.

Tulipofika tulikokuwa tunaenda, mimi na mke wangu tulipata ukumbi wa mkutano wetu huu kuwa ni mahali ambapo kuna giza kuu. Wenyeji hapa walikuwa watu waliokuwa na hofu kuu. Hata hivyo pale washiriki wa mkutano ambao walikuwa wachungaji walipofika, sisi sote tulisahau hali ile ya kuogofya. Tuliweza kuona Mungu akiwa kati yetu, na kutuondolea hali ile ya woga.

Mikutano ya wakati ule nchini Uganda ni baadhi ya matukio ambayo sisi hatuwezi kuyasahau. Katika mikutano hii tulijionea kwa macho yetu yale ambayo yalitufanya tujione kuwa kama watu ambao wamekutana na Mungu juu mlimani. Washiriki kwenye mikutano hii ambao walikuwa ni makasisi pamoja na wake zao walikaa kwenye viti vigumu kwa zaidi ya masaa 8 wakisikiliza kwa makini yale mimi na Dorothy tulikuwa tumewaandalia huku nikifunza Dorothy naye aliyaandika yale niliyokuwa na taja kwenye ubao. Nao washiriki wakawa wanayaandika yote kwenye vijikaratasi vidogo vidogo. Baada ya muda mfupi kukatokea zogo mlangoni. Ingawa moja wa walevi waliokuwa na bunduki alikuwa ameshikwa mlangoni, mwenzake alikuwa ameweza kuingia chumbani, na kuelekeza bunduki yake upande wa Dorothy. Naye Dorothy akasema hivi: “tuombe ili mtu huyu aweze kupokea wokovu” baada ya muda mfupi mkalimani akasema yale mlevi huyu alikuwa amesema: nataka kumjua Mungu wa mama huyu. Na wakati huu, niliweza kuona yale ambayo sijawahi kuyaona maishani. Sijui kama alikuwa malaika, au ni uwepo wa Mungu ulioelekeza tendo lile kutokea.

Sijui kama ni upole wake Dorothy mtu huyu aliamua kutenda kitendo kile, kile najua ni kwamba, bunduki ile ilitoka kutoka mikono ya mtu yule ikaanguka na kishindo sakafuni, naye akapiga magoti ghafla. Naye Dorothy akasema mara moja: “Omba pamoja nami ombi hili.” na hapo akamwongoza askari huyu katika ombi la kukiri imani yake kwa Kristo na kupokea wokovu hapo hapo.

Mbona nataja kisa hiki wakati huu? Sababu ni kwamba yale ninayotaka kuyataja hapa yana uhusiano wa karibu sana na kisa hiki. Katika mkutano huu, sina shaka lazima kulikuwa na wengi ambao walishikwa na chuki na hata huzuni kwa ajili ya kitendo cha yule mlevi. Kulikuwa na wengi katika mkutano ule ambao tayari walikuwa wamesumbuliwa na walevi wa aina hii. Yu ko hata kasisi mmoja ambaye alikuwa amepoteza kidole chake baada ya kushambuliwa na askari aliyenuia kumuua. Lakini kwa ajili yeye alikuwa mtu mwenye imani, aliye na wokovu; nao wote waliokuwa katika chumba kile walikuwa watu walio na imani pia, wote walimzingira huyu aliyepokea wokovu, wakamkumbatia na kuomba pamoja naye baada. Na jinsi vile ilivyo desturi ya waafrika wengi, kundi lile lilianza kuimba na kumsifu Mungu kwa ajili ya muujiza ule wa mtu kupokea wokovu. Wimbo waliouimba ulikuwa:

Damu ya Yesu,
Damu ya Yesu,
Damu ya Yesu
Husafisha kabisa

Laiti kama viongozi kutoka mataifa yetu wangekuwa nasi katika mkutano ule! Kwa kweli nao pia wangeona jinsi vile Mungu anavyoweza kutatua migogoro ya ki-kabila na ya rangi inayokumba sehemu nyingi duniani.

Na kwa yeye kuvipatanisha vituvyote kwa nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye; ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi au vilivyo juu mbunguni na ninyi, mliokuwa hapo kwanza mmefarikishwa, tena adui katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha sasa (Kol. 1:21).

Ni wale tu ambao wamepatanishwa na Mungu kupitia wokovu ambao ni kutoka kwake yesu Kristo mwana wa Mungu ndio watapokea wokovu wa kweli.

Basi zaidi sana tukisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye. Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya mwana wake, wala si hivyo tuu ila pia twajifurahisha katika Mungu kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye sasa tumepokea huo upatanisho (Rum. 5:9,10).

Hebu Fikiria

1. Je, una hamu ya kuwa na uhai wa kweli yaani uhai ule Kristo alitaja aliposema *mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele?* (Yn. 10:10).
2. Katika Biblia, ni wapi katika mwili wamwanadamu utapata uhai wa kweli? (Soma Law. 17:11).
3. Je, katika maisha ya milele, damu ya Yesu Kristo ina umuhimu gani?

Umeweka imani yako katika uwezo wa damu hii kusafisha na kukuondolea dhambi?

Ninamini kwamba damu hii yaweza kukupatia maisha ya milele?

Je unamini katika uwezo wa damu hii kukinga na kuzuia usishambuliwe na adui?

Yesu alisema hivi: *Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi ajapokufa atakuwa anaishi; naye kila aishie na kuniamini hatakufa kabisa hata milele* (Yn. 11:25,26).

*Umaridadi wa mchoro wa
mwanasanaa, umaarufu wa jinsi vile
mwanasanaa anavyoweza kuchora
mfano wa uso wa mwanadamu, hata uka,
ilifu wa mchoro wa umbo la nchi: haya
yote haywaezi yakelezwa na matamshi
yetu yanayotamkwa. UNahitaji uewzo w
akutumia macho kuelewa haya yote.*

Nawezaje Kujiunga na Jamii ya Mungu?

*M*namo mwanzo wa 1940, utalaamu wa kisayansi wa mambo ya afya ulipiga hatua kubwa sana mbele katika upasuaji wa macho. Mengi yalikuwa yametimizwa hivi kwamba ilikuwa inawezekana hata kutoa sehemu ya macho inayoitwa *cornea* kutoka kwa yule ambaye ameaga dunia na kuweka katika macho ya yule ambaye hawezi kuona. Daktari Sangster aliwahi kutueleza jinsi vile alivyoshuhudia matokeo ya kutolewa kwa sehemu hii ya *cornea* kutoka kwa macho ya mtu mmoja na kupachikwa katika macho ya mtu mwingine.

Asubuhi moja na mapema kabla jua halijachomoza, Daktari Sangster akiwa pamoja na watu wawili waliandamana katika sehemu ya kupendeza Uingereza iitwayo Surrey Down. Mmoja wao alikuwa ni mama ambaye alikuwa amezaliwa kipofu, naye mwenzake akawa ni daktari wa macho. Siku kadhaa baada ya upasuaji kulikuwa na benedeji zimewekwa machoni

kuzuia mwanga wa jua usimzidi. Baadaye, bendeji hizi zilitolewa.

Tayari mama huyu alikuwa ameanza kuhisi nguvu za mwanga kupitia macho yake; na hii ilikuwa tayari inamuweka furaha na hamu kubwa. Kabla jua halijachomoza, bendeji ya mwisho ilitolewa katika macho ya mama huyu.

Mwanga wa jua hauwezi ukawa na utukufu unaozidi ule wa siku hiyo. Jua lilichomoza kwa umbali kwa njia iliyo maridadi kabisa.

Sehemu yenye kivuli, na hata sehemu yenye kijani kibichi katika miti na kadhalika vilibadilika na kuwa na rangi iliyo maridadi sana katika mwanga wa jua asubuhi hiyo.

Ndege waliruka-ruka bustanini hapo karibu katika kazi ile ya kujitafutia chakula asubuhi na mapema. Yote aliyoyaona yalikuwa ya kufurahisha na kulisimua sana mama huyu ambaye alikuwa hajawahi kuona chochote tangu azaliwe. Na huku akibubujikwa na machozi, mama huyu alisema; “Ni kweli mumejaribu kunieleza jinsi vile vitu vinavyokaa, lakini sijawahi kufikiri kuwa yote mnyotaja yanaweza kuwa maridadi jinsi hii.”

Na hapa akakaa kimya akitafakari kuhusu umaridadi wa vitu ambavyo Mungu ameviumba.

Je, unawezaje kumweleza mtu ambaye hajawahi kuona jinsi vile rangi nyekundu inavyofanana? Ama jinsi vile rangi ya jua hubadilika pale wakati wa kutua jioni? Kwa kweli, ni vigumu sana. Maneno yanayoelezea umaridadi wa vile vitu ambavyo tunaviona na macho huwa hayana maana kwa yule

Nawezejje Kujiunga na Jamii ya Mungu?

ambaye hana uwezo wa kutumia macho yake. Uzuri wa mchoro wa mwanasanaa, umaridadi wa uso wa mwanadamu, ama ule wa nchi hauwezi kuelezwa na matamshi. Yote yanahitaji uwezo wa kuona kueleweka vyema.

Shida kama hii tena hujitokeza pale yule ambaye ana imani anapojaribu kumweleza asiye na imani uzuri na utamu wa imani.

Wakati mmoja nilipokuwa najaribu kumweleza mwanafunzi daktari katika hospital ya Guy mjini London, nilijaribu kumjulisha ajabu ya upendo wa mungu.

“Mimi siwezi kuona upendo huo na macho yangu” mwanafunzi yule akanijibu.

Nilielewa ni kwa nini amenijibu hivyo, lakini nikaendelea na kusema: “Sina shaka kwamba una shida hiyo ya kuelewa kwa sababu wewe ni sawa na mwanadamu anayeishi katika nyumba iliyo na giza. Naelewa hali hiyo vyema. Nimewahi kuishi katika giza la kiroho na sasa niko nje katika mwangaza wa jua la upendo wake mungu. Nikaendelea, “Daudi,” ikiwa ungependa kuelewa upendo wa Mungu, ni sharti utoke katika giza hivi sasa na uje katika mwangaza.

Siku hiyo Daudi alipiga magoti na kumsihi Kristo amsamehe makosa yake. Kamwe sitasahau yale kijana huyu aliyasema alipoamka kutoka pale alipokuwa amepiga magoti. Yeye alisema hivi: “Sikufikiria kwamba itakuwa ajabu kiasi hiki!”

Sawa na jinsi vile uwezo wa kuona na macho unavyosisimua na kuwa kielelezo cha umaridadi wa vyote ambavyo Mungu aliumba, uwezo wa kuona

utukufu wake Mungu huonyesha wazi ukweli kamili wa kuwepo kwa Mungu, nguvu zake na upendo wake kwa mwanadamu.

Baada ya kwenda juu mbinguni, Kristo, kupitia mtume Yohana alipeana kielelezo cha kutisha kuhusu hali ya kiroho ya wenyeji wa mji wa Laodikea.

Alisema hivi: *enyi hamfahamu kwamba nyinyi hamna macho... na kwamba nyinyi ni vipofu (Ufu. 3:17)*. Hebu fikiria hali ya mtu ambaye ni kipofu, na huku hajui kwamba yeye hana uwezo wa kuona na macho. Bila wokovu hali yetu ni sawa na ya mtu kama huyu. Baada ya kukagua hali yetu ya kiroho, na kuona jinsi vile hatuna uwezo wa kujichunguza kiroho na kuona jinsi vile tunakosa uwezo wa kuona kiroho, Kristo ametupatia njia ya kujiondoa kwenye hali hii ya upofu. Amesema: *Nakupa shauri, ununue kwanngu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho kujipaka macho yako upate kuona (Ufu. 3:18)*. Ushauri huu ni wa muhimu kiasi gani? Kuwa kipofu wa kiroho ni shida inayohitaji matibabu ya kiroho. Yule anayeweza kutusaidia ni Roho Mtakatifu.

Ulipozaliwa mara ya kwanza, tukio hili ilikuwa la kimwili, na halikuwapatia uwezo wa kuona na macho ya kiroho. Ukitaka kutoka katika giza la kiroho na kuingia katika nuru ya kufahamu utukufu wa Mungu (2 Kor. 4:6), inakubidi uzaliwe mara ya pili. Kristo alimwambia Nikodemu:

Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa roho ni roho. Usistajabu kwa kuwa nilikuambia,

Naweza je Kujiunga na Jamii ya Mungu?

*Hamna budi kuzaliwa mara ya pili (Yn. 3:6,7) ...
amin amin nakuambia, mtu asipozaliwa mara ya
pili hawezi kuona ufalme wa Mungu (Yn. 3:3).*

Kwa hivyo, ikiwa unataka kuona ufalme wa Mungu, Unahitajika kuzaliwa mara ya pili.

Sawa na kila mwanadamu, umezaliwa na sehemu iliyo tupu. Yule ambaye anaweza kujaza sehemu hii ni Mungu peke yake.

Sehemu hii iliyo tupu inaweza kujazwa tu wakati Kristo aliyefufuka atakapoinjia na kuweka makao yake ndani yako. Unapomkubali aingie katika maisha yako na kuwa Mwokozi wako, yale yaliyomfanya afe pale msalabani huwa yametimizwa maishani mwako. Yeye hakufa ili uweze kupokea msamaha wa dhambi zako. Yeye alikufa ili moyo wako uweze kusafishwa na kuwa safi, na uwe mahali ambapo yeye mwenyewe anaweza kuyatengeneza kuwa makao yake. Kwa hiyo kuna haja kwamba upokee msamaha wa dhambi kabla hajaja kuishi katika moyo wako.

Wakati mmoja, nilikuwa ninazungumza na kijana mmoja mwafrika mwaminio na hamu ya kueneza injili. Wakati wa mazungumzo yetu, nilihisi mara moja kwamba alikuwa na hamu ya kuwaeleza vijana katika nchi yake habari njema ya wokovu. Wiki iliyofuata nilikuwa nimepanga kuendeleza mafunzo ya Biblia kwa zaidi ya wachungaji 200; kwa hivyo nikamwalika ajiunge nasi. Na kwa vile tulikuwa mbali na mahali pa mafunzo, nilimshawishi atumie basi katika barabara mbaya yenye mashimo kuja pale ambapo tungekutana

kwa ajili ya mafunzo. Kijana huyu ambaye jina lake lilikuwa ni William alifika akiwa mchovu sana, lakini mwenye furaha kwamba amekuja kujifunza mengi yaliyohusu Mungu na Neno lake. William hakutumia basi lile lililojaa watu kwa ajili ya kuwa kama mtalii wa kufurahia safari. Ilikuwa ni lazima apige safari hii ndefu na ya kuchosha ili aje kuhudhuria mkutano huu wa kujifunza Neno la Bwana. Ilikuwa sharti afunge safari hii ili aweze kupata kile alichokitaka.

Sawa na jinsi hii Kristo alijua kwamba njia pekee ya kumwezesha kuingia katika roho yako, kukaa ndani yako na kuwa na ushirika wa karibu sana na wewe ni kupitia kuondoa dhambi katika moyo wako. Ingawa kulikuwa na haja kuondolewa kwa dhambi zako, maisha mapya katika Kristo, na uwezo wa kuwa na ushirika na Mungu; ndivyo ilivyokuwa hamu yake kuu. Je, unaweza kutosheka na lolote lililo chini ya haya? Kwa kweli, uhusiano huu na Mungu ndio sababu halisi ya kuumbwa kwako.

Kujua kwamba Kristo yuko ndani ya moyo wako, ni sawa na kuelewa kwamba umeyanza maisha ya milele. Kristo akiwa ndani yako hali hii inakuletea uhai wake Mwokozi wetu katika maisha yako.

Na huu ndio ushuhuda ya kwamba Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu uko katika mwanawe. Yeye aliye naye mwana, anao huo uzima; asiye naye mwana wa Mungu hana huo uzima (1 Yoh. 5:11-12).

Na hii ndio sababu si ajabu kwamba wakati rafiki yangu Daudi alimuomba Mungu amsamehe dhambi

zake na aingie katika maisha yake, yeye alisema:
“Sikujua itakuwa ajabu kiasi hiki.”

Haya yatawezekanaje?

Wakati watu walipomsikia Petro akihubiri kuhusu maisha, kifo na kufufuka kwake Yesu, Mungu aliwapa hamu ya kutaka kumjua mwokozi wetu. Roho Mtakatifu aliwatendea yale ambayo anakutendea wewe. Wao walimskiliza Petro akiwaeleza kwamba Yesu ni Mungu na pia Masihi wa Mungu. Haya waliyoyasikia yaliwafanya wafahamu vyema makosa yao, na ni kwa nini walihitaji wokovu. Na pale walipowaza kuhusu jinsi vile walivyokataa wokovu, na kukosa kutilia maanani tukio lile la kusulubiwa, maandiko matakatifu yanatuambia matamshi yake yaliwachoma moyo mpaka wakauliza: *Tutendeje, ndugu zetu? (Mdo. 2:37).*

Jibu lake la kwanza lilikuwa kuwasihwa watubu dhambi zao. Pasipo kutubu, imani iliyoko si imani ya kweli. Imani hii ni ya “kujisingizia” au “kujifurahisha.” Imani inayookoa ni ile iletayo tumaini na pia mabadiliko katika nia na moyo wa mtu.

Unapomshukuru Yesu kwa ajili ya yale aliyokutendea alipokufa msalabani, msimamo wako kuhusu Mungu na dhambi huwa una badilika kabisa. Ni hapa Roho Mtakatifu hufanya ile kazi ya upasuaji katika macho yako na kukuwezesha kuona mengi kwa njia iliyo tofauti. Kwa kweli neno toba lina maana ya kubadili maoni. Kwa hivyo, kuzaliwa upya kiroho kuwahusu kubadilika kwa mawazo ya yule aliye na imani kumhusu Mungu na dhambi.

Kuhusu Mungu: Toba kamili hukataa kabisa yote ambayo si ya kweli kuhusu Mungu. Nimewaona watu fulani katika bara la Afrika ambao wamepigana vita vikali wakijaribu kuondolea mbali njia zao za hapo awali, na hata mila za mbeleni. Kati ya hawa nimewaona hata wengine wakichoma vyombo vyao vya uchawi baada ya kumkubali Kristo kuwa mwokozi wao. Nimekuwa na marafiki ambao wamelazimika kuvumilia vikwazo vingi vya kijamii ambavyo vimewajia baada wao kumkubali Kristo kuwa Bwana na mwokozi. Wa ko wale ambao wamevumilia vitisho na hatari mbali mbali baada ya kujiondoa kutoka vikundi vya kidini na hata kijamii ambavyo mienendo yao sio sawa na ile inayohitajika kutoka kwa Mungu wa Bibilia. Imani inayookoa lazima iwe na msingi wake katika wazo moja kuu: kwamba Kristo ndiye Mwokozi wa pekee.

Kuhusu dhambi: Unapopata wokovu wako kwa imani, wewe mwenyewe utagundua dhambi zako kwa huzuni na aibu. Mabadiliko katika mawazo yako, yaani kutubu dhambi kunahitaji kwamba hutaendelea kujitafutia sababu ya kuendelea katika hali ya dhambi yako. Pia hii inamaanisha kwamba hutaendelea kuamini kwamba wokovu wako pekee unatosha kukuondolea dhambi. Kwa maana sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu, na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi; *sisi sote twanyauka kama jani, na maovu yetu yatuondoa, kama upepo uondoavyo (Isa. 64:6)*. Lakini unapogeuka na kumjia Kristo, utakuwa na hamu ya

kuacha vyote ambavyo umekuwa ukifanya maishani ambavyo havimfrahishi Mungu.

Hebu fikiria hali ya afisa wa jeshi mwenye cheo cha Koplo ambaye yuko likizoni. Siku moja, afisa huyu anapokea barua mbili: moja kutoka kwa rafiki yake, nayo ya pili ni kutoka kwa kamanda wake. Katika barua ya kwanza, kuna ombi linalomtaka ahudhurie arusi ya rafiki yake. Nayo ya pili inamtaka aripoti mara moja kazani. Kuna tofauti kwa kati ya ombi na “amri.” “Ombi” au “mwaliko” waweza kukataliwa; lakini amri ni sharti ijibiwe kwa utiifu. Isipotiiwa basi hii huchukuliwa kuwa sawa na ausi.

Mungu anakupenda. Anajua dhambi itakuangamiza, yeye hatoi mwaliko kwako utubu. Yeye anakuamuru utubu. Mtume Paulo alipokuwa akikamilisha mahubiri yake ya injili kwa wahitimu wa filofia na wapita njia katika chuo kikuu kilichokuua katika mji mkuu wa taifa la Wayunani, alisema hivi: *bali sasa anawagiza watu wote wa kila mahali watubu (Mdo. 17:30).*

La ajabu ni kwamba unapobadili jinsi vile unavyomfahamu Mungu na wakati huo kuacha dhambi zako, na kwa njia hiyo kuja kwake Kristo na kukiri kwamba yeye ni Mwokozi; Roho Mtakatifu atakuongoza maana “*ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kwa kutimiza kusudi lake jema*” (Flp. 2:13). Kwa hivyo Mungu anawa ahidi wale ambao wako tayari kutubu dhambi zao atawapa hamu na nguvu za kuweza kutimiza yale yalio mapenzi yake. Ni baada ya hapo maisha ya yule aliye na imani yatabadilika na kufikia kiwango ambacho Mungu amepanga afikie.

Wewe ni rafiki, nami nakusihi umpokee Kristo haraka bila kuchelewa. Tafuta mahali ambapo hakuna kelele, upige magoti mbele ya Mungu na uombe. Kwa kweli ukirudia rudia matamshi fulani fulani kama kasuku, haya hayataweza kukusaidia kwa vyovyote. Lililo la muhimu ni kwamba ukubali kwa njia ya imani yale Kristo amesema juu yake mwenyewe katika Yohana 14:6 kwamba, *“Mimi ndimi njia na ukweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi”* (Yn. 14:6).

Wakati huu ukipenda unaweza kufunga macho yako na kuomba moja kwa moja ombi ambalo litatoka katika moyo wako. Kama sivyo huenda ukapata kwamba ombi hili ni la msaada kwako.

Ombi Langu

Mungu wangu, sijakujua wala kukupenda. Hata hivyo nakupa ahsante kwa sababu umenijua na kunipenda.

Mimi ni mwenye dhambi, na kwa uwezo wangu sina lile ambalo naweza kufanya kupokea wokovu. Na kwa imani, hivi sasa naja kwako Bwana Yesu na kukuomba msamaha. Nakubali kwamba mimi nimetenda dhambi, na pia natubu dhambi zangu. Ahsante sana Kristo kwa sababu ulikufa kwa ajili yangu. Na isitoshe, umenipa damu yenye thamani kubwa na yenye uwezo wa kuondoa dhambi. Kupitia imani, naweka maisha yangu chini ya ulinzi wa ko; ulinzi wa damu yako.

Nakusihi ingia katika moyo wangu Kristo, yachukue maisha yangu na uyasimamie.

Nawezaje Kujiunga na Jamii ya Mungu?

Ahsante sana Yesu; kupitia Roho Mtakatifu nimezaliwa mara ya pili. Ni jambo la kunifurahisha sana kujua kwamba kupitia nguvu zako wewe uliye fufuka, mimi ni mtoto wa Mungu na nitaishi na wewe milele kwa kuwa imeandikwa katika maandiko ... na kila amwaminiye, hatatahayarika (1 Pet. 2:6).

Pia imeandikwa ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu (Rum. 10:9,10).



Barua Kutoka Slovakia

“Wapendwa, nimekamilisha shighuli ya kusoma kitabu kizuri sana: sijawahi kusoma kitabu kizuri kiasi hiki. Kitabu chenyewe ni hiki: Kiu Cha Kumtafuta Mungu. Najua wazi kwamba sitarudi kuwa jinsi nilivyokuwa kabla ya kusoma kitabu hiki. Bwana wetu Yesu amenikubali; nami nimempa maisha yangu. Ningependa furaha hii ambayo niempata baada ya kutoa maisha yangu kwake iwe yako pia. Ni furaha ambayo ni ya kila mtu. Nami hapa nawasihii mmitumei nakala mbili za kitabu hiki ili niwape wenzangu.

“Nawashukuru sana kw ajili ya kutuletea Injili na pia zawadi ya wokovu. Sisi hutukujua kwamba kuna kitabu kizuri kama hiki.”

– Mwandishi ni J.A.

Hebu Fikiria

1. Je, unawezaje kuonyesha kwamba umefurahia zawadi kuu ambayo umepokea?

Je, ni kupitia kusema kwamba, “nipe hiyo zawadi au la?”

Je, ni kupitia kutamka matamshi ya kushukuru?

2. Je, ni nini ambacho wakichukua kuwa hakikisho kwamba imani uliyo nayo ni imani inayokufaa?

Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu (Efe. 2:8).

3. Je, imani yako katika Kristo inahusisha toba, shukrani na hamu ya kumtegemea yeye aliyekuokoa?

Chukua nafasi hii kushukuru kwa ajili ya kukuokoa, na kumsifu Bwana Yesu, sio tu kwa lile amefanya, bali pia kwa jinsi alivyo.

Na Je, ni kupitia roho ile ya kujiona kwamba umefanya makosa na unastahii msamaha?

Ama ni kupitia kuwa na ile roho ya kushukuru kwa ajili ya wema ambao umekujia?

Ama ni kupitia ile roho ya utiifu na kumtegemea Mungu?

4. Na sasa Mshukuru Mungu kwa ajili ya kukuokoa, pia mshukuru sio tu kwa ajili ya yale amekutendea, lakini pia kwa ajili ya Uwezo wake.



Hakuna lolote, hali, au shida au jaribu ambalo laweza kunifikia kabla halijapitia kwa Kristo. Na kama lolote baya litanifikia, basi litakuja kutoka mbali kabisa na kuna sababu kuu ya kunifikia; sababu ambayo sielewi wakati huu. Na kwa ajili sitaki kushikwa na hofu, wala kubabaika pale ninapoyainua macho yangu kwake yeye aliye juu, nayakubali yote, kuwa yametoka kwake aliye kwenye kiti cha enzi kwa ajili ya sababu kuu, ya kuibariki roho yangu. Hakuna huzuni utakaoweza kunisumbua, wala majaribu kuniondolea nguvu; wala hali ya kunifanya nining'unike. Nitatulia kwa furaha ya kufahamu jinsi Mungu wangu alivyo. Huu ndio ushindi wa imani.

ALAN REDPATH

Nini Kitafuata?

*W*o kovu ni kitu cha bure. Hakuna lolote binadamu anaweza kufanya ili apate wokovu. Kristo ndiye anayetimiza yote.

Bali wote walimpokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu (Yn. 1:12).

Sina shaka hivi sasa unajiuliza, ni nini ninachostahili kufuata baada ya kupokea wokovu? Kabla Yesu hajawaacha wanafunzi wake akiwa safarini kupigana na baadaye kushinda kifo, yeye alitoa agizo hili: *kaeni ndani yangu, nami ndani yenu (Yn. 15:4)*. Katika matamshi haya, Yesu alieleza maana hasa ya maisha ya

Mkristo. Kupitia macho yake Mungu mwenye imani anakaa ndani yake mwanawe, na hapo ndipo anapopata utunzi na ulinzi mpaka pale atakapofika juu mbinguni. Hata hivyo, katika macho yao wanadamu, kwa ajili Kristo aliyefufuka yumo ndani ya wale walio na imani halisi, katika jamii yao, katika marafiki na katika wahudumu wenzake, maisha yao yanaweza kueleweka kama yale ambayo Mwokozi Yesu yu ndani yake mwaminio.

Hebu waza kuhusu chuma yenye moto ambayo iko katika moto unaowaka. Ukitazama kwa makini, ni wazi chuma ile iko katika moto; na pale chuma hii inaposhika joto kamili na ikawa na rangi sawa na ile ya moto ule, basi waweza hata ukachukuwa kwamba moto unapatikana ndani ya chuma. Waza pia kuhusu kikombe ambacho kimewekwa ndani ya ndoo ya maji. Kikombe kimewekwa katika maji; pia maji yako katika kikombe.

Pale ulipozaliwa mara ya pili, Roho mtakatifu alikuweka ndani ya mwili wake Kristo. Maisha yako ni kama chuma iliyo katika moto, au kikombe kilicho ndani ya maji: yeye yuko ndani yako nawe uko ndani yake!

Bibilia inasema, ...*na uhai wenu umefichwa pamoja na kristo katika Mungu (Kol. 3:3)*. Naam! Kwa maana umezaliwa mara ya pili, wewe u ndani ya Yesu. Ajabu! Pia, ulipozaliwa mara ya pili, maisha ya ndani katika kristo aliyefufuka yalifanywa kuwa kweli na nguvu zake Roho Mtakatifu katika maisha yako. Sasa unaweza kufurahi kwa ajili *Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu (Kol. 1:27)*. Kwa ajili umezaliwa mara ya pili Kristo aliyefufuka sasa yu hai ndani yako. Ajabu!

Na sasa hebu tuangalie kwa undani yale Bibilia inayosema kuhusu uhuru unaopatikana kupitia ukweli huu kwamba mimi niliyepokea wokovu niko ndani yake Kristo; naye Kristo yuko ndani yangu.

Nini Kitafuata?

Niko Ndani ya Kristo

Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja (1 Kor. 12:13).

Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima (Rum. 6:3,4).

Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu (Kol. 3:3).

Hapo mbeleni nilimjua kijana mmoja mdogo aliyekuwa akiugua maradhi ya **Leukamia**. Wakati huo, kijana huyu alikuwa na umri wa miaka saba. Ilikuwa ni sharti aende kwa daktari kila baada ya miezi mitatu ili apate shindano kwenye uti wa mgongo. Siku moja, daktari alitaka kujua ni kwa nini kijana Daryl hakuwa akilia kwa uchungu pale shindano inapopenyeza uti wake wa mgongo kama watoto wenzake. “Je, wewe husikii uchungu,” daktari alimuuliza.” Kwa kweli mimi husikia uchungu,” kijana Daryl alijibu. “Lakini daktari, kuna jambo moja hujaelewa, nalo ni kwamba shindano hii inapitia mkononi mwa Kristo kabla haijanigusa.

Ni jambo la ajabu kujua kwamba, kwa ajili hivi sasa uko ndani ya Kristo, yeye anauwezo wa kuangalia na kuchunguza kila kitu ambacho kinagusa kila sehemu ya mwili wako. Hiyo ndiyo imani.

Na jinsi vile ulivyompokea Kristo kwa njia ya kuwa na imani, ni kupitia msingi huu wa imani utaweza kuelewa na kumchukua kuwa aliye na uwezo wa kutimiza mahitaji yote ya maisha yako. Lile tunalosema hapa ni kwamba tendo lako lile la imani la kumpokea Kristo limefungua mlango ili uweze kuendelea kuwa na imani. *Basi kama **mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni** vivyo hivyo katika Yesu (Kol. 2:6).*

Na ingawa umezaliwa mara ya pili, Mungu hatarajii kwamba utaishi kwa kujaribu kuiga maisha ya Kristo. Mamilioni ya wakristo wamevunjwa moyo wanapojaribu kuiga maisha ya Kristo bila kufanikiwa. Mungu anatumbeza kuhusu yale aliyotuwekea tayari yakutusaidia katika maisha yetu ya kikristo.

Tayari tumekufa katika Kristo. Na tukiwa wafu, hatuko tena chini ya amri na mamlaka ya dunia. Na jinsi ilivyokuwa hapo mbeleni ndivyo ilivyo hivi sasa na hata siku za baadaye, tumekufa kabisa na hatuna imani kwamba twaweza kutumia nguvu zetu kuishi maisha ya kiroho. Lakini Bwana asifiwe, sisi tu hai katika utukufu ulio na uwezo wa kutulinda na kututunza; uwezo unaopatikana katika Kristo aliyefufuka. Shida hutokea tunapojaribu kukumbana na majaribu na hata shida mbili mbali tukitumia nguvu zetu wenyewe.

Yule amempokea Kristo atagundua kwamba ni vigumu kujaribu kuishi jinsi mkristo halisi anavyostahili kuishi kwa kutumia nguvu na uwezo

Nini Kitafuata?

wake. *Kristo mwenyewe alituonya hivi: pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote (Yn. 15:5).*

Akigusia jambo hili la upumbavu wa mtu kujaribu kupata wokovu kupitia bidii yake mwenyewe, Mtume Paulo alitumia matamshi makali alipowaandika Wagalatia. Akiwa anawakosoa kuhusu kutoka kuputoka kutoka msingi wa Mungu wa kuishi kwa njia ya imani, mtume Paulo aliuliza swali hili:

Enyi wagalatia msio na akili, ni nani aliyewaloga, ninyi ambao Yesu Kristo aliwekwa wazi mbele ya macho yenu ya kuwa amesulubiwa? Nataka kujifunza neno hili moja kwenu, je, mlipokea roho kwa matendo ya sheria, au kwa kusikia kunakotokana na imani? (Gal. 3:2-3).

Ukweli ni kwamba walianza maisha yao mapya katika Kristo sawa na jinsi vile hata wewe umefanya kupitia njia ya kuwa na imani. Ni kupitia njia ya kutegemea imani wanaweza kuwa na tumaini na kutarajia *kutawala pamoja na Kristo katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo (Rum. 5:17).*

Katika eneo la Galatia, nguvu na moto wa imani waliokuwa nao ulikuwa sasa umetoweka. Badala yake kulikuwa na mambo walioyafanya ya kisheria ambayo waliyafuata badala ya imani ya kweli. La kushukuru Mungu ni kwamba ikiwa utazidi kuishi ukimtegemea yeye ambaye umemkubali maishani, haya ya kuhuzunisha ambayo twayaona Galatia hayatakuumba.

Na Kristo ndani yangu

*Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali **Kristo yu hai ndani yangu** (Gal. 2:20).*

*Na **Kristo akiwa ndani yenu**, mwili wenu, umekufa kwa sababuya dhambi; bali roho yenu i hai, kwa sababu ya haki. Lakini, ikiwa roho yake yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafuataihusisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, ka roho wake anayekaa ndani yenu (Rum. 8:10-11).*

*Ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii katika mataifa, nao ni **Kristo ndani yenu**, tumaini la utukufu (Kol. 1:27).*

Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na msingi katika upendo (Efe. 3:17).

Unaweza kukiri imani yako kupitia matamshi haya “ahsante sana Bwana, wewe ni kila kitu ambacho siwezi nikawa. Nakupa ruhusa uwe kile ambacho mimi mwenyewe siwezi nikawa.”

La ajabu ni kwamba Mungu mwenyewe amechukua jukumu la kukuendeleza katika imani yako, naye akampa jukumu hili Mwokozi wetu Yesu Kristo. Ni Yesu ndiye aliye na uwezo wa kukumbana na majaribu ambayo yatakufikia katika maisha yako ya kikristo. Hata inawezekana kuwa wewe ni mtaalamu wa Teolojia huku ukiwa huna Kristo ndani yako. La muhimu ni kwamba huwezi kuwa Mkristo ikiwa Kristo hayumo ndani yako. Ni Yesu pekee anayeweza kuishi

Nini Kitafuata?

maisha ya Kikristo kupitia uwezo wa Roho Mtakatifu. Ni kwa ajili wa uwezo huu ameweza kujenga makao yake katika moyo wako. Sasa anaweza kufanya mengi akikutumia, hata yale ambayo wewe huwezi kufanya kwa nafsi yako. Yeye aliye msafi ndiye anayekufanya uwe safi katika dunia hii chafu ya uovu na usherati. Yeye ndiye atakaye kushindia katika dunia hii ya majaribu. Yeye aliye upendo ndiye atakaye kujaza na upendo katika dunia hii ambapo watu wanajipenda na kushugulikia nafsi zao. Yeye aliyefufuka amefufuka katika roho yako na kukufanya uwe mkristo halisi.

Unaponyenyekea na kujiweka katika Yesu ambaye aliyekuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea (Lk.19:10), wewe pia unaweza sasa kuamini kwamba yeye atakutumia kuwatafuta na kuwaokoa wale waliopotea. Maisha yanakuwa yakusisimua wakati mwaminio anapogundua kwamba yeye pia anaweza kutumiwa na Mwokozi wetu kuwaokoa wale waliopotea.

Kumbuka ingawa Kristo amerudi juu mbinguni, kamwe hajajitoa kwako. Alipokuwa akiwaacha wafuasi wake hapa duniani, yeye aliwaambia hivi:

*Bali ninyi mnaniona. Na kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai. Siku ile ninyi nanyi mtatambua ya kuwa mimi ni ndani ya **Baba yangu, nanyi ndani yangu, nami ndani yenu** (Yn. 14:19-20).*

Labda sasa unajiuliza, je uwezo huu wa kufanya haya yote ambayo yametajwa naweza kufanya nini ili niweze kuutumia maishani? Hili ni swali zuri. Swali

laonyesha wazi kwamba unatambua tofauti iliyoko kati ya imani katika mawazo tu, na imani ambayo ni ya vitendo vinavyonekana wazi. Swali hili pia ni ishara kwamba una hamu ya kuwa na imani ambayo ni ya matendo. Jibu ni kwamba maisha ya Kristo hujitoa na kuonekana katika yule aliye na imani kama jibu linalo fuata ombi na shukrani. Imani ya kweli kila wakati huwa ni ya kusesitiza usemi huu, “ahsante!”

Kwa mfano, njia moja ya kumshukuru Mungu ni kupitia kusema *ahsante* kwa ajili ya kukuokoa. *Pasipo imani, huwezi kumfurahisha Mungu (Ebr. 11:6)*. Na sasa waweza kumshukuru kwa vile yeye anaweza akakutimizia yale ambayo ungependa kuyapata kutoka kwake, yote yawezekana.

Petro alipowaandikia wakristo ambao walikuwa wanapata mateso kwa ajili ya imani yao, yeye alisema hivi: *Muwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu (1 Pet. 3:15)*.

Na hapa kuna siri kuu iliyo wazi kuhusu jinsi ya kukumbana na mateso yanayokuja kwa ajili ya imani yako. Kuwa na hakikisho kwamba kweli Kristo ni Bwani wa maisha yako.

Labda unaweza kukumbuka kwamba jina mojawapo la Mungu katika Agano la kale ni Adonai. Jina hili lina maana bwana, aliye bwana wa huduma. Ni wazo hili, kwamba Mungu ni “*Bwana anayetuhudumia*”, ambalo Petro alitumia katika kuandika hivi: “*Mungu atakaswe katika mioyo yenu.*”

Kristo akiwa Bwana wa maisha yako, utafurahia ushirika ulioko kati yake na wewe. Ni hapa utaweza

Nini Kitafuata?

kujisikia kuwa huru kumuamini na kuweka tumaini lako ndani yake katika kila hali unayokumbana nayo maishani. Sawa na yale mtunzi wa nyimbo George Matheson aliandika:

Nifanye mfungwa, Bwana
ili niwe huru;
nilazimishe kuweka chini upanga wangu
na hapo ndipo nitakapokuwa mshindi.

Kinyume na imani ambayo imeenea sana ya kwamba tuko huru, uhuru haimaanishi kuwa na haki ya kufanya lolote utakalo. Kuwa na uhuru kuna maanisha, kuwa na uwezo wa kufanya kulingana na mapenzi ya Mungu. Kukumbuka maneno yake Mtume Paulo katika waraka kwa wafilipi *nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu (Flp. 4:13)*.

Wakati wa uamsho mkuu katika taifa la Ireland mwaka wa 1859, maelfu ya watu walimkubali Kristo kuwa Mwokozi wao. Hawa ambao walimkubali Kristo waliweka hakikisho la imani yao kupitia njia ya kuweka sahihi “azimio la imani.” Wakati huo, kulitokea mabadiliko makubwa katika maisha ya watu wengi sana kupitia wao kumkubali Kristo kiasi kwamba taifa hili lilibadilika.

Ingawa si jambo kubwa sana katika kuweka sahihi kwenye karatasi, labda ingekuwa jambo la msaada kwako kuthibitisha imani yako katika Mungu kwa kutia sahihi yaliyo katika kurasa zifuatazo:

*Basi Mungu wa amani aliyemleta tena kutoka
kwa kwa wafu mchungaji mkuu wa kondoo, kwa*

damu ya agano la milele, yeye Bwana yetu Yesu, awafanye ninyi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kufanya mapenzi yake naye akiyafanya ndani yetu lipendezalo mbele zake, kwa Yesu Kristo, utukufu una yeye milelena milele, Amina (Ebr. 13:20-21).



Barua kutoka Hungary

“Nawashukru sana kwa ajili ya kunitumia kitabu cha maandiko Matakatifu ambacho ni Biblia, pamoja na kitabu chake ndugu Richard A. Bennett: Kiu cha Kumtafuta Mungu.

“Nimesoma na nikakamilisha kitabu hiki: na baada yakufanya hivyo, nikatazama Maandiko yaliyo nukuliwa kutoka Biblia.

“Kiu cha Kumtafuta Mungu kimenisaidia kuelewa vyema ni nini nastahili kuamini na ni kwa sababu gain nastahili kushikia imani hii. Sisi mimi nina imani baada ya kupokea usaidizi kutoka kitabu hiki na nimechukua uamuzi wa kuwa na imani ya Kikristo.”

– Ripoti hii imeandaliwa na kutafsiriwa na Trans World Radio

**Sasa huu ni msaada wa kukuwezesha
kuchukua uamuzi wa kushikilia
imani halisi.**

***Maandiko Mtakatifu*
zimenukuliwa ukurasa
156 na 157.**

Uamuzi Wangu

Nimeamua kwamba Mungu Baba ni Mungu wangu

Kwa kuwa wao wenyewe wanatangaza habari zetu, jinsi kulivyokuwa kuingia kwetu kwenu; na jinsi mliyomgeukia Mungu mkaziacha sanamu, ili kumtumikia Mungu aliye hai, wa kweli.

(1 The. 1:9)

Nampokea Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi wangu

Mtu huyo Mungu amemtukiza kwa mkono wake wa kuume, awe mkuu na mwokozi, awape waisraeli toba namsamaha wa dhambi.

(Mdo. 5:31)

Nampokea Roho Mtakatifu anijaze na Upendo wa Mungu

Kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho Mtakatifu tuliypewa sisi.

(Rum. 5:5)

Nachukua neno lake Bwana kuwa sheria ya kufuata

Kila andiko, lenye punzi ya Mungu, la faa kwa mafundisho, na kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.

(2 Tim. 3:16,17)

Nawachukuwa watu wa Mungu kuwa watu wangu

Naye Ruthu akasema, usinisihini nikuache, nirejee nisifuatane nawe; Maana wewe uendako nitakwenda, na wewe ukaapo nitakaa. Watu wako watakuwa watu wangu, na Mungu wako atakuwa Mungu wangu.

(Rut. 1:16)

Naitoa nafsi yangu kwako Mungu

Kwa sababu hakuna mtu miongoni mwetu ashiye kwa nafsi yake, wala hakuna afaye kwa nafsi yake. Kwa maana kama tukiishi, twaishi kwa Bwana, au kama tukifa, twafa kwa Bwana. Basi kama tukiishi ama kama tukifa, tu mali ya Bwana.

(Rum. 14:7,8)

Uamuzi Wangu

Nafanya haya kwa kukusudia

Nanyi kama mkiona vibaya kumtumikia BWANA, mkanitumikie kwa unyofu wa moyo na kwa kweli; na kiweka mbali miungu ambayo baba zenu walitumikia ng'ambo ya mto, au kwamba ni miungu ya wale waamori ambao mnaaka katika nchi yao; lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana.

(Yos. 24:15)

Na kwa weupe wa Moyo

Kwa maana kujisifu kwetu ni huku, ushuhuda wa dhamiri yetu, ya kwamba kwa utakatifu na weupe wa moyo utokao kwa Mungu; si kwa hekima ya mwili, bali kwa neema ya Mungu; tulienenda katika dunia na hasa kwenu ninyi.

(2 Kor. 1:12)

Na kwa kujitoa kwa hiari

Watu wako wanajitoa kwa hiari, siku ya uwezo wako, kwa uzuri; kwa uzuri wa utakatifu, tokea tumbo la asubuhi, unao umande wa ujana wako.

(Zab. 110:3)


Daima milele

Who shall separate us from the love of Christ? Shall tribulation, or distress, or persecution, or famine, or nakedness, or peril, or sword?

(Rum. 8:35)

Sahihi: _____

Tarehe: _____



**Baada ya kusoma
kitabu hiki, nakushihi
jitahidi usome pia**

*Kuza
Imani
Yako*

Sawa na jinsi vile mtu anavyoweza kufurahia taratibu mbali mbali za kupika jinsi taratibu zilivyoelezwa katika kitabu cha mapishi, na kando na kufurahia utaratibu huu, yeye afe na njaa; asomaye Maandiko Matakatifu anaweza kuyafurahia w akati huo huo akawa anakufa kwa ajili ya njaa ya kiroho.

Kuza Imani Yako kina utaratibu wa kukusaidia usome Maandiko Matakatifu uyaelewe na kuyatilia maanani.

Kitabu hiki kimechapishwa na huduma ya kimataifa ya

Cross Currents International Ministries

www.ccim-media.com

Anuani yetu ni:

Mkurugenzi

Trans World Radio

P. O. Box 21514 Code 00505

Nairobi, Kenya

e-mail: twr@twr.co.ke

tel: 020-2679842